

**RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA  
HESABU ZA SERIKALI KUHUSU TAARIFA ZA  
FEDHA ZA SERIKALI KUU KWA MWAKA  
ULIOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2010**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI**

Telegramu: "Ukaguzi"  
Simu: 255 22 2115157/8  
Faksi: 255 22 211  
**Barua pepe: [ocag@nao.go.tz](mailto:ocag@nao.go.tz)**  
Tovuti: [www.nao.go.tz](http://www.nao.go.tz)  
Kwa majibu tafadhali taja  
Kumb CA.4/37/01/2009/10



Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa  
Hesabu za Serikali,  
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,  
Samora Avenue/Mtaa wa Ohio  
P.O. Box 9080,  
DAR ES SALAAM.

Tarehe

26 Machi, 2011

**Kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa  
Hesabu za Serikali juu ya Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa  
mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2010**

Mh. Dkt. Jakaya M. Kikwete,  
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,  
S.L.P. 9120,  
Ikulu,  
Dar es Salaam.

**Yah: Kuwasilisha Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa  
Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa za Fedha za Serikali Kuu  
kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2009**

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano  
wa Tanzania (iliyorekebishwa 2005) na Kifungu cha 34 (1)(c) cha  
Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008, ninawasilisha  
kwako ripoti iliyotajwa hapo juu.

Nawasilisha.

Ludovick S. L. Utouh  
**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI.**

## YALIYOMO

YALIYOMO .....	iii
Ilianzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano .....	vii
Dira.....	vii
Dhamiri .....	vii
Vifupisho .....	ix
DIBAJI.....	xi
SHUKRANI .....	xv
MUHTASARI WA MAMBO MUHIMU KATIKA RIPOTI YA UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA ZA SERIKALI KUU KWA MWAKA 2009/2010 .....	xvii
A: Utangulizi .....	xvii
B: Hati za Ukaguzi zilizotolewa .....	xvii
SURA YA 1 .....	1
UTANGULIZI .....	1
1.1 Ukaguzi wa Taarifa za Hesabu za Umma .....	1
Majukumu na wajibu wa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali .....	2
1.3 Muundo wa kazi za ukaguzi .....	2
1.4 Majukumu na maslahi ya watumishi .....	3
1.5 Mawanda na viwango vya Ukaguzi vinavyotumika .....	4
1.6 Sera ya Kihisibu .....	5
1.7 Wajibu wa Kisheria .....	5
1.8 Mfumo wa Udhhibiti wa Ndani .....	6
1.9 Kutayarisha na kuwasilisha taarifa za fedha .....	6
SURA YA 2 .....	9
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO ..YATOKANAYO NA HOJA ZA UKAGUZI KWA MIAKA ILIYOPITA .....	9
2.0 Utangulizi .....	9
2.1 Majibu kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) .....	9
SURA YA 3 .....	19
MAKUSANYO YA MADUHULI NA MCHANGANUO WA FEDHA	

ZA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO .....	19
3.1 Utangulizi .....	19
SURA YA 4 .....	31
MATOKEO YA UKAGUZI WA AWALI WA MALIPO YA UZEENI .....	31
4.0 Utangulizi .....	31
4.1 Madhumuni ya ukaguzi wa awali .....	31
4.2 Mawanda ya ukaguzi wa awali .....	32
4.3 Matokeo ya ukaguzi na mapendekezo .....	32
SURA YA 5 .....	39
MAMBO MUHIMU YALIYOJITOKEZA KATIKA UKAGUZI WA WIZARA, IDARA, WAKALA NA SEKRETARIETI ZA MIKOA .....	39
5.1 Manunuzi yaliyofanywa bila kuwa kwenye mpango wa manunuzi wa mwaka .....	39
5.2 Matengezezo ya magari katika karakana .....	39
5.3 Malipo ya mishahara kwa wastaafu .....	40
5.4 Ununuzi wa samani kwa maafisa wasiokuwa na stahili .....	41
5.5 Malipo yenye nyaraka pungufu .....	42
5.6 Mali na vifaa visivyopokelewa .....	44
5.7 Malipo yaliyofanyika kutoka katika vifungu .....	44
5.8 Malipo yenye shaka .....	45
5.9 Kukosekana kwa orodha ya waliolipwa .....	46
5.10 Ukaguzi wa Usimamizi wa Manunuzi .....	47
SURA YA 6 .....	55
UCHAMBUZI WA HESABU JUMUIFU ZA TAIFA .....	55
6.1 Utangulizi .....	55
6.2 Masuala ya miaka iliyopita yasiyojibiwa .....	55
6.3 Matokeo ya ukaguzi ya mwaka kuhusu Hesabu Jumuifu .....	56
SURA YA 7 .....	75
7.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UKAGUZI .....	75
7.1 Utangulizi .....	75
7.2 Aina ya hati za ukaguzi .....	76
7.3 Hati inayoridhisha isiyo na mambo ya msisitizo .....	80
7.4 Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo .....	80
7.5 Hati yenye shaka .....	80
7.6 Hati isiyoridhisha .....	80
7.7 Hati mbaya .....	80

7.8.	Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa . . . . .	81
7.9	Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa zilizopewa Hati mbaya . . . . .	81
	SURA YA 8 . . . . .	151
8.0	Tathmini ya Mfumo Unganifu wa Usimamizi wa Fedha (IFMS) 151	
8.1.	Utangulizi . . . . .	146
8.2.	Madhumuni ya Tathmini iliyofanyika . . . . .	152
8.3.	Muhtasari wa Matokeo ya ukaguzi . . . . .	153
8.3.1	Udhibiti dhaifu wa habari na Usalama . . . . .	153
	SURA YA 9 . . . . .	159
	MAJUMUISHO NA MAPENDEKEZO . . . . .	159
9.1	Majumuisho . . . . .	159
9.2	Mapendekezo . . . . .	159
	VIAMBATANISHO I . . . . .	181
	VIAMBATANISHIO II-VII . . . . .	185-209



Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,  
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,  
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ilianzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano

Madaraka na wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yameelezwa kwenye Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (iliyorekebishwa 2005) na kufafanuliwa zaidi katika Kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008.

#### **Dira**

Kuwa kituo cha ufanisi katika ukaguzi wa hesabu za Serikali na taasisi za umma.

#### **Dhamiri**

Kutoa huduma ya ukaguzi wa hesabu yenye tija ili kuimarisha uwajibikaji na thamani ya fedha katika kukusanya na kutumia rasilimali za umma.

Katika kutoa huduma zenye ubora, ofisi hii inaongozwa na vigezo vya msingi vifuatavyo:

- 1) **Uadilifu:** sisi ni asasi adilifu inayotoa huduma kwa namna isiyo na upendeleo.
- 2) **Ubora:** sisi ni wanataaluma wanaotoa huduma zenye ubora kwa kuzingatia viwango kubalifu vya ukaguzi
- 3) **Uaminifu:** tunahakikisha kuwa na kiwango cha juu cha uaminifu na kuzingatia utawala wa sheria.
- 4) **Mtazamo wa watu:** tunatazama na kukazia zaidi katika matarajio ya wadau wetu kwa kujenga utamaduni mzuri wa kuhudumia mteja na kuwa na watumishi wataalamu na wenye motisha ya kazi.
- 5) **Uvumbuzi:** sisi ni asasi ambayo wakati wote inahamasisha utamaduni wa kupokea na kuendeleza mawazo mapya kutoka ndani na nje ya asasi.
- 6) **Matumizi bora ya rasilimali:** sisi ni asasi inayothamini na kutumia rasilimali za umma ilizokabidhiwa kwa umakini mkubwa.





## Vifupisho

A/C	Akaunti
ACGEN	Mhasibu Mkuu wa Serikali
Act	Sheria ya Fedha za Umma Na.6 ya 2001 kama ilivyorekebishwa mwaka 2004
CAG	Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
CDTI	Taasisi ya Maendeleo ya Jamii na Mafunzo
CFS	Taarifa Jumuifu za Fedha
CPO	Ofisi Kuu ya Malipo
FDCS	Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi
HIV	Upungufu wa Kinga Mwilini
IFMS	Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha
INTOSAI	Taasisi ya Kimataifa inayojumuisha Asasi kuu za Ukaguzi wa Hesabu
ISA	Viwango vya Ukaguzi wa Hesabu vya Kimataifa
JKT	Jeshi la Kujenga Taifa
LART	Mfuko wa Kusimamia Mikopo na Ufuatiliaji wa Madeni
LGAs	Mamlaka za Serikali za Mitaa
MDAs	Wizara, Idara na Wakala
NAO	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu
PFA	Sheria ya Fedha za Umma Na. 6 ya 2001
PFMRP	Programu ya Marekebisho ya Usimamiaji Fedha za Umma
PFR	Kanuni za Fedha za Umma
PMG	Mlipaji Mkuu wa Serikali
PPA	Sheria ya Manunuzi wa Umma Na. 21 ya 2004
RAS	Sekretarieti za Tawala za Mikoa
RCCB	Daftari la Kukusanyia Maduhuli
Reg.	Kanuni
Sect.	Kifungu
SUMA	Shirika la Uchumi na Maendeleo
TANSORT	Shirika la Kuchambua Almasi la Serikali ya Tanzania
TCAA	Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania
UNESCO	Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa
URT	Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
USD	Dola za Kimarekani
TRA	Mamlaka ya Mapato Tanzania
IFAC	Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu
SNAO	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Sweden
PAA	Sheria ya Ukaguzi wa Umma



## DIBAJI

Ninayo furaha kuwasilisha Ripoti ya Ukaguzi ya mwaka 2009/2010 kuhusu taarifa za fedha za Serikali Kuu (Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa) nchini kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2010. Ripoti hii inalenga kuwapatia wadau wetu muhtasari wa matokeo ya ukaguzi wa taarifa za hesabu za Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha 2009/2010 ambapo maelezo ya kina yanapatikana katika ripoti za Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa zilizopelekwa kwa kila Afisa Masuuli mhusika.

Ripoti hii ya Ukaguzi inawasilishwa kwa Mheshimiwa Rais kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kifungu 34(1)(c) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008.

Kwa mujibu wa Ibara 143 (2) (c) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa angalau mara moja kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa Hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano, hesabu zinazosimamiwa na watumishi wote wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na hesabu za Mahakama zote za Jamhuri ya Muungano na hesabu zinazosimamiwa na Katibu wa Bunge.

Kutungwa kwa Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008 kumeongeza mawanda ya ukaguzi wetu kwa kunipa madaraka ya kufanya kaguzi nyingine zaidi ya ukaguzi wa kawaida wa taarifa za fedha ambazo ni ukaguzi wa ufanisi, utambuzi na mazingira na kaguzi maalum. Ni matumaini yangu kwamba, kwa kuanzishwa kwa sheria mpya ya Ukaguzi wa Umma, Ofisi yangu itaweza kuimarisha udhibiti wa fedha na kuisaidia Serikali kuimarisha uwajibikaji. Kwa hiyo, sheria itaniwezesha kuwa huru na kulihakikishia Bunge masuala yanayohusu uwajibikaji, uwazi na matumizi bora ya rasilimali hasa kuona kwamba rasilimali hizo zimetumika vizuri kwa kuzingatia uchumi, ufanisi na kama ilivyotarajiwa na kupitishwa na Bunge.

Hata hivyo, uhuru kamili wa kiutendaji unahitajika ili kuniwezesha kudhibiti rasilimali za ofisi zilizopo zikihusisha rasilimali watu na fedha zitakazoweza ofisi yangu kutimiza majukumu yake bila kuingiliwa na Mamlaka yoyote.

Ni vyema kutambua kuwa wakati ofisi yangu inatoa taarifa kuhusu ukiukwaji wa sheria, taratibu na kanuni mbalimbali na udhaifu katika mifumo ya udhibiti wa ndani kwenye taasisi za Umma na hasa Serikali Kuu, lakini wajibu wa kuhakikisha kuwepo kwa mifumo thabiti ya udhibiti wa ndani ni jukumu la Maafisa Masuuli.

Ni matarajio ya Bunge kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi watahakikisha utoaji wa taarifa za fedha na usimamizi wa rasilimali katika Serikali Kuu kuhusiana na ufanisi na ubora na usimamizi wa mipango iliyowekwa. Kwa njia ya ukaguzi, ofisi inachangia katika kutoa mapendekezo kuhusu uimarishaji na uboreshaji wa sekta ya Umma. Kwa msingi huu, Serikali Kuu na Ofisi yangu zina mchango mkubwa wa kutoa kwa Bunge katika kujenga imani kwa Umma katika usimamizi wa rasilimali za Umma.


Ingawa majukumu yanatofautiana, matarajio ya usimamizi bora ya rasilimali yanafanana.

Ili kukidhi matarajio ya Wabunge na yale ya Umma kwa mapana zaidi, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imeendelea kufanya uchambuzi wa njia bora zaidi za kufanya ukaguzi na kuongeza wigo wa masuala yanayokaguliwa na hivyo kuimarisha utendaji wa uwajibikaji katika sekta ya Umma. Aidha, tunahakikisha ukaguzi wetu unalenga kuyapa kipaumbele maeneo muhimu ili kuchangia katika sekta ya Umma. Kwa kuwa kazi ya ukaguzi ni chachu katika usimamizi wa fedha, tutaendelea kujadili masuala yanayoathiri utawala/uongozi katika sekta ya Umma, hasa katika utoaji wa taarifa za usimamizi wa fedha na masuala ya utawala bora.

Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali Kuu (PAC) imefanya kazi kubwa ya kuboresha utendaji wa Maafisa Masuuli wa Serikali Kuu ambao utendaji wao haukufikia matarajio ya Kamati hiyo. Pamoja na jitihada hizo, ninaamini kuwa Serikali Kuu ina jukumu muhimu katika kuboresha usimamizi wa fedha za Umma.

Napenda kutambua mchango wa wafanyakazi wa Ofisi yangu kwa juhudi kubwa walizofanya katika kutimiza malengo tuliyojipangia licha ya kufanya kazi katika mazingira magumu ambayo ni pamoja na kukosa fedha za kutosha, kukosa vitendea kazi, mishahara duni na upungufu wa watumishi hasa wale wa kutimiza majukumu yetu ya msingi ya ukaguzi.

Natarajia kuwa Bunge litaona taarifa hii kuwa ni muhimu katika kuiwajibisha Serikali kwa jukumu lake la usimamizi wa fedha za Umma na utoaji wa huduma kwa Watanzania. Hivyo, nitafurahi kupata taarifa ya jinsi gani nitaweza kuboresha taarifa yangu hii kwa siku zijazo.



Ludovick S. L. Utouh  
**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

---

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,  
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,  
S.L.P. 9080,  
Dar es Salaam,  
29 Machi, 2011



## SHUKRANI

Napenda kutoa shukrani kwa wote walioniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kikatiba. Kwa mara nyingine, napenda kutoa shukrani zangu kwa wafanyakazi wote wa Ofisi yangu kwa kuniwezesha kutoa ripoti hii kwa wakati. Ninawajibika kutoa shukrani zangu za pekee kwa familia yangu na familia za wafanyakazi wa Ofisi yangu kwa kutuvumilia kwa kutokuwa nao kwa muda mrefu wakati tukikamilisha majukumu haya ya kikatiba.

Vilevile, natoa shukrani zangu za dhati kwa wafadhili hasa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Sweden, Serikali ya Sweden kupitaaguzi Shirika la Kimataifa la Misaada la Maendeleo la Sweden, Benki ya Dunia kupita Mradi wa Kusimamia na Kuboresha Sekta ya Fedha za Umma (PFMRP) na wote wenye mapenzi mema ambao wamechangia kwa kiasi kikubwa kuboresha Ofisi yangu. Mchango wao umekuwa na manufaa makubwa katika kuendeleza na kukuza raslimali watu, nyezo za kazi (magari), mifumo ya teknolojia ya mawasiliano na vitendea kazi. Hata hivyo, bado misaada zaidi inahitajika kwa ajili ya kuboresha kazi za ukaguzi katika sekta ya umma kwa kuzifanya kuwa za kisasa zaidi. Jambo hili lingewezwa kwenda haraka endapo angepatikana mfadhili wa kugharamia ujenzi wa Kituo cha Mafuzo ya Ukaguzi kitakachojengwa Gezaulole katika Manispaa ya Temeke.

Aidha, natoa shukrani zangu kwa Hazina, Mlipaji Mkuu wa Serikali, Maafisa Masuuli, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Ununuzi wa Umma, Mhakiki Mali Mkuu na wadau wote kwa taarifa mbalimbali muhimu walizonipatia ili kukamilisha kazi hii. Pia namshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuniwezesha kutoa ripoti kwa wakati.

Mwisho, lakini sio kwa umuhimu, nawashukuru wafanyakazi wote wa Umma popote pale walipo wawe ni wa Serikali Kuu au Halmashauri bila ya kuwasahau walipa kodi ambao ndio walengwa wa ripoti hii. Michango yao imekuwa msaada mkubwa katika ujenzi wa Taifa ambao hauwezi kupuuzwa hata kidogo.

Naomba Mungu awabariki wote.





**MUHTASARI WA MAMBO MUHIMU KATIKA RIPOTI YA UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA ZA SERIKALI KUU KWA MWAKA 2009/2010**

Taarifa ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ihusuyo Taarifa za Fedha za Serikali Kuu imelenga maeneo yafuatayo:

- (A) Utangulizi
- (B) Hati za ukaguzi zilizotolewa
- (C) Udhaifu katika mfumo wa udhibiti wa ndani
- (D) Mapungufu katika mchakato wa manunuzi
- (E) Masuala ya kodi
- (F) Masuala yahasuyo malipo ya uzeeni
- (G) Hitimisho na mapendekezo

**A: Utangulizi**

Sehemu hii inaeleza kwa muhtasari matokeo ya ukaguzi wa Taarifa za Fedha katika Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2010. Mawanda ya ukaguzi katika Serikali Kuu yanajumuisha Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala na Sekretarieti za Mikoa, Ofisi za Balizi na Miradi inayogharamiwa na wafadhili

**B: Hati za Ukaguzi zilizotolewa**

Matokeo ya ukaguzi kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2010 yanaonyesha kutoboreka kwa hati zilizotolewa kwa Serikali Kuu na Taasisi zake ikilinganishwa na mwaka uliopita kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini:

Category of entities	Unqualified opinions		Qualified opinions		Adverse Opinions		Disclaimer of Opinion		Total	
	2008/9	2009/10	2008/9	2009/10	2008/9	2009/10	2008/9	2009/10	2008/9	2009/10
MDAs	46	42	5	13	1	1	-	-	52	57
RAS	18	12	2	7	1	1	-	1	21	21
Embassies/Missions	27	29	4	2	1	-	-	-	32	31
Total	91	83	11	22	3	2	-	-	105	108
% age	87%	77%	10%	20%	3%	2%	NIL	1%	100%	100%

Jedwali linaonyesha kwamba hati za kuridhisha zimepungua kutoka asilimia 87 hadi asilimia 77 wakati hati zenye Shaka zimeongezeka kutoka asilimia 10 hadi asilimia 21 Matokeo ya

ukaguzi kwa mwaka huu yamebaini hati 2 zisizoridhisha ikilinganishwa na hati 3 zilizotolewa mwaka 2008/2009. Aidha, matokeo ya ukaguzi yanaonyesha kuwepo kwa hati mbaya 1 mwaka kwa mwaka 2008/2009 haikutolewa hati yoyote ya aina hiyo.

Vile vile katika mwaka 2009/2010, kulikuwa na mazingira ya kushindwa kutoa hati kwa Sekretarieti ya Mkoa wa Dodoma kutokana na jengo la ofisi kuungua moto na nyaraka na taarifa za fedha zilizotakiwa kukaguliwa kuteketea kabisa. Kwa mwaka 2008/2009, hapakuwa na mazingira yaliyonifanya kushindwa kutoa hati

Kwa kuwa mwelekeo wa hati za ukaguzi umeonyesha kutoboreka ikilinganishwa na mwaka jana, natoa ushauri kwa uongozi katika Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa pamoja na Balozzi kutorejea katika hali ya miaka ya nyuma na badala yake kuendeleza mafanikio yaliyokwishapatikana katika usimamizi wa fedha na mali.

#### **C: Dosari tulizozikuta wakati wa ukaguzi**

Wakati wa ukaguzi wa mwaka huu tumekutana na dosari mbalimbali ambazo maelezo ya kina yametolewa katika sura husika. Masuala muhimu yanayohusiana na dosari hizo ambayo yako katika ripoti yangu ni haya yafuatayo:

- Mafungu mawili (2) yalifanya vibaya na hivyo kupewa hati isiyoridhisha. Mafungu hayo ni Wizara ya Maliasili na Utalii - Fungu 69 na Sekretarieti ya Mkoa wa Lindi - Fungu 76. Mafungu haya yametolewa hati hii kwa miaka miwili mfululizo
  - Kutofuatwa kikamilifu kwa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika sekta ya Umma (IPSAS)
  - Kutofuatwa kikamilifu kwa Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 na kanuni zake za 2005
  - Kutotekeleza mapendekezo ya ukaguzi kwa miaka iliyopita.
  - Malipo ya zaidi ya Sh. 382,000,000,000 yalifanywa bila nyaraka sahihi wala taarifa za kuthibitisha uhalali wake

- Bidhaa zilizonunuliwa na kulipwa kwa lakiri lakini hazijapokelewa hadi wakati wa kuandika taarifa hii.
- Ununuzi wa samani kwa maafisa wasio na stahili wanaokaa katika nyumba zao binafsi
- Mishahara ya jumla ya Shs. 1,842,607,565.29 ililipwa kwa watumishi hewa
- Madai mara mbili ya malipo ya uzeeni (pensheni na mafao ya mikataba) kinyume na sheria za pensheni.
- Ongezeko la deni la Taifa kwa asilimia 38 kutoka Shs.7,621,286,730,033.80 mwaka 2008/09 hadi Shs.10,503,806,011,884.90 mwaka 2009/2010
- Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2010, Hesabu Jumuifu za Taifa zilionyesha kuwa dhamana za Serikali zilifikia kiasi cha Shs.711, 804,989,096. Kwa wastani, kiasi hiki cha dhamana ni sawa na asilimia 96.8% ya mikopo yote iliyotolewa. Hii ni ukiukaji wa Kifungu cha.13 (1) (b) cha sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana za Serikali ya 1974 (iliyorekebisha 2004), ambayo inatoa kiasi kisichozidi 70% ya fedha zote zilizokopwa.
- Kiasi cha Sh. 160,756,067,190 kiliripotiwa katika Hesabu Jumuifu za Taifa kikiwa ni madeni yasiyolipwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2010. Kiasi hiki kinawakilisha ongezeko la asilimia 50.2 ikilinganishwa na kiwango cha mwaka uliopita cha Sh. 107,063,198,140. Kwa hiyo, matumizi ya jumla kwa mwaka yalionyesha pungufu kwa kiasi sawa na madeni hayo. Huu ni ukiukwaji wa msingi wa uhasibu unaotambua mapato na matumizi kwa fedha taslimu
- Kiasi kilichoonyeshwa katika Hesabu Jumuifu za Taifa kama thamani ya uwekezaji uliofanywa na Serikali haukuhusisha taasisi 9 ambazo hesabu zake hazikuwasilishwa Hazina kwa ajili ya majumuisho.
- Hakuna daftari la mali za kudumu za Serikali linaloonyesha mali zenye thamani ya Shs. trillion 7.981 zilizoripotiwa katika Hesabu Jumuifu za Taifa. Hii

inamaanisha kuwa ni vigumu kuhakiki uwepo wa mali hizo.

- Serikali kupitia Hazina ililipa kiasi cha Shs.48,000,270,000 katika Benki ya Tanzania kama mchango wake katika kuchochea ukuaji wa uchumi kufuatia mtikisiko wa uchumi ulioikumba dunia. Hata hivyo, Hazina haikutoa orodha ya makampuni au watu binafsi walionufaika na fidia hiyo au malipo ya madeni yao kuahirishwa. Aidha, utaratibu wa kurekodi malipo na marejesho ya fedha hizi haukuwekwa bayana na hivyo kushindwa kujiridhisha endapo yalikuwa ni malipo halali dhidi ya fedha za umma

**D: Dosari zilizobainika katika mchakato wa manunuzi**

Matokeo ya ukaguzi uliofanya na Mamlaka ya Udhubiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) umeonyesha wastani wa kiwango cha uzingatifu wa sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004 kufikia asilimia 55. Kiwango hiki kimekokotolewa kutokana na vigezo 13 vya uzingatifu ambavyo maelezo yake yako katika Sura ya III ya ripoti hii. Wastani wa viwango vya uzingatifu wa Sheria ya Manunuzi katika Wizara, Idara, Mashirika ya Umma (PAs) na Halmashauri za Wilaya kilikuwa 57%, 59% and 50%.

Kwa upande mwingine, uzingatifu wa Sheria ya Manunuzi katika Taasisi za manunuzi (PEs) zilizokaguliwa na PPRA kilikuwa chini ya wastani (chini ya 50%). Matokeo haya yanatokana na vigezo vitano vilivyoangaliwa ambavyo ni: Kuwepo kwa Kitengo cha Manunuzi na uwiano wa wataalam wenye sifa stahiki; Kuandaliwa kwa mipango ya mwaka ya manunuzi; Kutangazwa kwa zabuni zilizotolewa; Utunzaji nyaraka na Udhubiti wa ubora. Kwa upande mwingine, kiwango cha uzingatifu kiklikuwa juu ya wastani (50% na zaidi) katika vigezo nane vifuatavyo: Kuanzishwa kwa bodi za zabuni na muundo wake; Utendaji wa Maafisa wahasibu, Bodi za Zabuni na Vitengo vya Manunuzi; uzingatifu wa viwango vya uidhinishaji wa manunuzi; Utangazaji wa Zabuni; Muda wa kuandaa tangazo la zabuni; Utumiaji njia sahihi ya kufanya manunuzi; Matumizi ya nyaraka sahihi za

zabuni kama zilivyoielezwa katika Kanuni za Manunuzi za mwaka 2005; na Utekelezaji wa mikataba.

#### E: Masuala ya Kodi

Matokeo ya ukaguzi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania yamejumuishwa katika Hesabu Jumuifu za Taifa katika Sura ya IV ya taarifa hii. Mambo muhimu yaliyojitokeza ni kama ifuatavyo:

- Kumekuwepo na masuala ya nyuma yasiyoshughulikiwa yenye thamani ya kiasi cha Sh. 220,292,054,615 na Dola za Kimarekani 47,255,243.
- Hesabu za Mamlaka ya Mapato Tanzania Bara zimeonyesha makusanyo ya kiasi cha Sh. 4,637,513,963,999 ikilinganishwa na makadirio ya Sh. 5,028,922,100,000 na kusababisha makusanyo pungufu ya Sh. 391,408,136,001
- Taarifa za mapato ya Mamlaka ya Mapato Tanzania zilionyesha misamaha iliyotolewa kwa Taasisi mbalimbali yenye thamani ya Sh. 680,667,900,000 sawa na asilimia 14 ya makusanyo yote. Katika hali halisi, kama kiasi cha Sh. 680,667,900,000 kisingesamehewa, Mamlaka ya Mapato Tanzania ingekusanya Shs. 5,318,181,863,999 ambazo ni sawa na Shs. 325,920,005,259 zaidi ya kiasi kilichokadiriwa kukusanywa.

Kwa upande wa Hesabu Jumuifu za Taifa, matokeo muhimu yalijumuisha masuala yafuatayo:

Items	Amount (Shs.)
Increase in Public Debt	2,882,519,281,851
Mikopo iliyotolewa na Serikali ambayo haijarejeshwa	424,087,766,124
Mihadi isiyolipwa	93,860,806,990
Madeni yamkini	26,276,785,317
Dhamana za Serikali	711,804,989,096
Madeni yasiyolipwa	160,756,067,190
Uwekezaji wa Serikali	8,718,182,145,310
Malimbikizo ya hasara ilizopata Serikali	78,014,807,604
Malimbikizo ya deni katika akaunti ya benki	1,331,073,630,470.30
Kutorejeshwa kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali fedha ambayo haikutumika	31,821,562,811

Aidha, pamekuwepo na udhaifu katika kuhifadhi taarifa zinazohusiana na uwekezaji na dhamana za Serikali.

**F: Masuala yahasuyo malipo ya uzeeni**

Kwa vile madaraka yangu yanahusisha ukaguzi wa mafao ya wastaafu, Sura ya tisa ya ripoti hii inaonyesha matokeo muhimu ya ukaguzi wa awali niliyofanya katika kipindi husika. Ukaguzi ulibaini kwamba:-

- Kiasi cha malipo kwa wastaafu kingelipwa zaidi ya kile kilichostahili kwa Sh. 301,506,150.5 kama malipo hayo yasingehakikiwa
- Wastaafu wangelipwa malipo pungufu kwa kiasi cha Sh. 167,430,608.06 kama madai yao hayangehakikiwa.

Matatizo makubwa yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi wa mafao ya wastaafu ni kama ifuatavyo:

- (i) Matatizo ya kiuendeshaji
- (ii) Tafsiri isiyokuwa sahihi ya sheria za pensheni. Kanuni zake na sheria nyingine
- (iii) Matatizo ya kiutawala

Masuala muhimu yaliyojitokeza kutokana na ukaguzi huo ni haya yafuatayo:

- Kutotumia viwango sahihi katika ukokotoaji wa mafao ya wastaafu.
- Kuchanganya masharti ya ajira za kudumu na za mikataba
- Maamuzi yanayokinzana kwa baadhi ya watumishi yanayopingana na sheria za pensheni.
- Kutozingatiwa kwa sheria za pensheni
- Ucheleweshaji wa kuwasilisha madai ya pensheni kwa ajili ya ukaguzi
- Nyaraka zisizokamilika
- Kutokuwa na stahili za kulipwa mafao
- Utoaji idhini zenye utata (unaokinzana)

## Hitimisho na mapendekezo

Mwisho, kwa mujibu wa madaraka niliyopewa chini ya Kifungu cha 10 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008, nimetoa mapendekezo kadhaa katika Sura ya 9 ya ripoti hii ambayo kama yatatekelezwa yatasaidia kuimarisha usimamizi wa rasilimali za Umma katika nchi yetu. Mapendekezo hayo yanajumuisha:-

- Utekelezaji wa mapendekezo yangu ya miaka ya nyuma kwa wakati
- Serikali ijiepushe kuingia katika mihadi wakati ikijua kuwa hakuna fedha. Aidha, wakati umefika kwa Serikali kuwachukulia hatua Maafisa Masuuli wanaoshindwa kuzingatia mfumo wa bajeti Serikalini unaoaka mapato na matumizi kutambuliwa na kuandikwa vitabuni pale yanapopokelewa au kulipwa.
- Madeni ya jumla ya Sh. 21,630,000,000 yatambuliwe na kuingizwa katika Taarifa Jumuifu za Fedha.
- Kuhakikisha ufuataji wa sheria pamoja na mfumo wa utoaji taarifa.
- Kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani na kuboresha nidhamu katika matumizi ya Serikali.
- Kuimarisha michakato ya manunuzi kwa kufuata Sheria za manunuzi
- Uboreshaji wa taratibu za malipo ya mwisho ya wastaafu

### G. Mapitio ya Mfumo Jumuishi wa Usimamizi wa Fedha (IFMS)

- Imebainika kuwepo kwa usimamizi dhaifu katika matumizi ya mfumo wa IFMS na udhibiti mdogo usioweza kuhakikisha usiri wa taarifa zilizoko katika mtandao. Imeonekana pia kuwa wasimamizi wa anwani za IFMS wameweza kufanya mabadiliko mbalimbali pasipo kutumia programu ya IFMS. Aidha, mfumo wa IFM unaruhusu waingiza 'data' kubadili na kuidhinisha maelezo yaliyoko katika fomu ya kuagiza mali (LPO) na maelezo ya wateja. Udhaifu huu umefanya waingiza

'data' waweze kuandaa na kuidhinisha LPO pasipo Mhasibu Mkuu kujua; utaratibu ambao sio kubalifu.

- Imebainika kuwa hakuna mpango wowote wa kuhakikisha kuwa taarifa zilizopo katika mfumo wa IFMS zinapatikana endapo janga litatokea. Hapakuwa na chapisho lolote rasmi linaloeleza jinsi ya kurejesha shughuli za mtandao wakati wa maafa. Aidha, hapajawahi kufanyika majaribio ya kujihami (simulation) ili kujenga uelewa wa namna ya kujihami endapo maafa yatatokea. Vilevile, wakaguzi waligundua kuwa Mhasibu Mkuu wa Serikali aliingia katika mkataba na Benki Kuu ya Tanzania wa kuwa na kituo katika Jiji la Dare es Salaam kwa ajili ya kuweka kituo cha pamoja cha kuchakata data wakati wa majanga katika mfumo wa IFMS. Hata hivyo, kituo hicho hakijawahi kutumika katika shughuli za majanga
- Imeonekana kuwa baadhi ya maboresho yaliyofanyika katika mfumo wa IFMS hayakuhitaji uingiwaji mkataba. Hata hivyo kuna marekebisho yanayoendelea au yaliyokamilika katika maeneo mawili (EFT interface na GFS 2001) ambayo hayakuingiwa mkataba rasmi.
- Bila kuwepo mkataba rasmi wa maboresho yanayofanyika katika mtandao, itakuwa vigumu kupima uwezo wa mtoa huduma katika kutekeleza jukumu hilo. Vilevile, upo uwezekano wa kuongezeka kwa mawanda ya kazi na gharama kusikotarajiwa.
- Imeonekana kuwa mazingira ya mfumo wa IFM yamegubikwa na kutoingwa mikataba au kuwepo kwa mikataba dhaifu kati ya Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali (ACGEN) na muuzaji programu za mtandao huu.
- Mikataba isiyosimamiwa vyema inaweza kusabisha kuwepo kwa ongezeko la gharama za uendeshaji wa mtandao kwa Serikali.
- Kulikuwa na kadhia nyingi za benki zisizosuluhishwa za tangu mwaka wa 2000. Hii ilisababishwa na mtandao



kutokuwa na uwezo wa kubeba kiasi kikubwa cha tarakimu rejea (reference number) katika fomu yake ya mapokezi ya fedha taslim itumikayo kusuluhisha kadhia hizo na zile za Benki Kuu. Pia kulikuwa na tarakimu rejea zilizoingizwa kimakosa na watumiaji wa mtandao na hivyo kuchangia kuwepo kwa kadhia zisizosuluhishwa.

- Imeonekana kuwa, wakati wa kuhama kutoka Platinum SQL kwenda EPICOR mwaka 2000, daftari la fedha lililopo katika toleo la Platinum SQL halikuhamishwa kwenda EPICOR. Matokeo yake, kumekuwepo malipo katika vitabu vya benki ambayo hayapo katika daftari la fedha kwa kipindi cha kuanzia Julai hadi Disemba, 2000. Malipo hayo hayajasuluhishwa hadi wakati wa kuandika taarifa hii. Mchakato wa usuluhisho wa benki umesisitizwa katika taarifa hii kwani ninaamini kuwa unaweza kuwa na athari kwa taarifa za fedha kwa Serikali na kwa hali hiyo, hatua za haraka zinapaswa kuchukuliwa.

# SURA YA 1

## UTANGULIZI

1.0 Taarifa hii inatolewa kufuatia ukaguzi wa hesabu na kumbukumbu nyingine za Wizara, Idara, Wakala, Sekretarieti za Mikoa na Balozi kwa mujibu wa Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebisha 2005) na Kifungu cha 34(1) (c) cha Sheria ya Ukaguzi Na. 11 ya mwaka 2008 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2010.

### 1.1 Ukaguzi wa Taarifa za Hesabu za Umma

Kutokana na Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninapaswa kukagua kumbukumbu za taarifa zote za hesabu za fedha katika Ofisi zote za Umma, Mahakama na Mamlaka zote za Serikali ya Muungano wa Tanzania na kutoa taarifa kwa Mheshimiwa Rais ambaye atahakikisha zinawasilishwa mbele ya Bunge.

Katika kutimiza wajibu huu, kutokana na Kifungu Na. 10 cha Sheria Na 11 ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008, ninatakiwa kujiridhisha kwamba:-

- Tahadhari inachukuliwa ili kuhakikisha kwamba fedha za Umma zinakusanywa na kutunzwa kwa mujibu wa sheria na miongozo iliyowekwa.
- Fedha zote kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali zimeidhinishwa na kutolewa kufuatana na Sheria ya Matumizi ya Bunge ya mwaka husika.
- Fedha zote zinazotolewa Mfuko Mkuu zinatumiwa kulingana na matumizi yaliyokusudiwa na kwa mujibu wa sheria na kanuni za fedha na ugavi.

Aidha, kutokana na Kifungu kilichotajwa hapo juu ninawajibika kumtanabaisha Rais au Bunge juu ya uwepo wa matumizi mabaya ya fedha na mali za Umma.

### **1.2 Majukumu na wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa na Balozi**

Wajibu wa kisheria wa Ofisi yangu katika kukagua hesabu za Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa na Balozi umebainishwa chini ya Kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008. Kutokana na Sheria hiyo, ninawajibika kuchunguza, kukagua na kutoa taarifa juu ya hesabu za Wizara na Idara za Serikali na Maafisa Masuuli, na watu wote waliokabidhiwa jukumu la kukusanya, kupokea, kutunza, kutoa au kuuza, kuhamisha na kutoa stakabadhi, dhamana, vifaa au mali nyingine za Umma. Pia, jukumu langu linahusu Mashirika yote ya Umma na Taasisi nyingine, Mamlaka yoyote au Taasisi inayopokea fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali, au Taasisi yoyote ambayo imeruhusiwa kisheria kukaguliwa na Ofisi yangu.

### **1.3 Muundo wa kazi za ukaguzi**

Taarifa hii inatoa kwa muhtasari matokeo ya mwisho ya zoezi la ukaguzi ambalo lilifanywa na Ofisi yangu nchini kote katika mwaka huu. Ili Ofisi yangu iweze kushughulikia kikamilifu kazi hii kubwa ya kukagua Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa nchini kote, kuna Ofisi katika Wizara na Mikoa yote Tanzania Bara ili kurahisisha utendaji wa ukaguzi wa Umma.

Ofisi hizi za Mikoa na Wizara zinasimamiwa na Wakaguzi Wakazi ambao wanawajibika kwa Wakaguzi wa Kanda. Tumeona ni vyema kugawa wakaguliwa wetu katika Kanda ambazo zinaongozwa na Wakaguzi wa Kanda ili kurahisisha usimamizi wa kaguzi zinazofanywa chini yao. Wakaguzi wa Kanda wanawajibika kwa Wasaidizi Wakaguzi Wakuu ambao nao wanawajibika kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

#### 1.4 Majukumu na maslahi ya watumishi

Majukumu ya Ofisi yangu yameongezeka kwa kiwango kikubwa yakilinganishwa na ya miaka ya nyuma.

Majukumu yamekuwa makubwa zaidi baada ya madaraka ya kifedha kwenda hadi ngazi ya Tarafa, vijiji na hivyo kuwepo na haja ya msingi ya Ofisi yangu kuwa na matawi ngazi ya Wilaya. Pamoja na kuongezeka kwa wigo na ukubwa wa majukumu, uwezo wa kifedha na maslahi kwa watumishi yamekuwa madogo.

Ningependa kutambua juhudi za Serikali katika kuboresha hali za wafanyakazi katika Ofisi yangu iwapokuwa juhudi zaidi zinatakiwa kuboresha maslahi hayo yaendane na mazingira halisi ya kazi inayofanywa. Nimewasilisha mapendekezo ya muundo mpya wa Ofisi yangu ambao umepitishwa na Mh. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 26 February 2010. Juhudi za kuanza kutumia muundo huu zinaendelea; hii ni pamoja na kutoa mafunzo ya taaluma ya uhasibu ili kupata watumishi wenye sifa stahiki kujaza nafasi zilizopo. Pia, nimewasilisha mapendekezo ya mishahara katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa watumishi wa Ofisi yangu miaka miwili iliyopita. Mapendekezo hayo yalikataliwa kwa maelezo kuwa marekebisho ya mishahara yaliyofanywa kwa watumishi wa sekta ya umma yaliwahusu pia watumishi wa ofisi yangu.

Kwa sasa ofisi yangu imepanua mawanda ya ukaguzi kwa kiasi kikubwa. Nia ya ofisi ni kupanua shughuli za ukaguzi hadi ngazi ya wilaya ambako fedha nyingi za maendeleo zinaelekezwa na Serikali na Wafadhili. Juhudi hizi zitahitaji Serikali kuridhia maombi ya mapendekezo ya marekebisho ya mishahara pamoja na kutenga bajeti kwa ajili ya upanuzi wa mawanda ya ukaguzi unaokusudiwa.

Pia ni nia yangu kuhakikisha kwamba wakaguzi wanafundishwa mbinu mbalimbali za ukaguzi ikiwa ni pamoja na ukaguzi wa mazingira, jinsia, ukaguzi wa mifumo ya teknolojia ya kisasa, (mbinu za ukaguzi

zinazotekelezwa kwa kutumia teknolojia ya kompyuta - CAATs ).

## **1.5 Mawanda na viwango vya Ukaguzi vinavyotumika**

### **1.5.1 Mawanda ya ukaguzi**

Mawanda ya ukaguzi kwa kifupi yanahusisha ukusanyaji wa maduhuli, uidhinishaji wa matumizi kwa kufuata sheria ya Bunge, utekelezaji wa miradi, utendaji wa Hazina, Mamlaka ya Mapato Tanzania na ukaguzi wa fedha katika Balozi.

Ukaguzi ulifanyika ili kujiridhisha kwamba kulikuwepo na uzingatiaji wa kanuni zilizopo, kuongeza ufanisi na kupunguza gharama za uendeshaji na kubainisha kasoro zilizojitokeza, ingawaje siyo zote.

Wakati wa ukaguzi, Maafisa Masuuli wanataarifiwa kuhusu hoja zilizojitokeza na kupewa muda wa kujibu hoja hizo. Kwa kawaida maswala ambayo hayajajibiwa kikamilifu ndiyo yanayokuwa kwenye ripoti ya mwaka. Kuanzia mwaka uliopita wa fedha nilianzisha utaratibu mpya wa kutoa barua ya ukaguzi pamoja na ripoti ya ukaguzi. Barua ya ukaguzi ni kwa ajili ya hoja mbalimbali pamoja na ushauri kwa Afisa Masuuli mhusika na ripoti inapelekwa kwa vyombo vinavyowasimamia Maafisa Masuuli na Umma kwa ujumla.

### **1.5.2 Viwango vya Ukaguzi vinavyotumika**

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu ni mwanachama wa Taasisi ya Kimataifa inayojumuisha Asasi Kuu za Ukaguzi Kimataifa (INTOSAI). Pia Ofisi ni mshirika wa Taasisi inayojumuisha Ofisi za ukaguzi za nchi za Kiafrika zinazotumia lugha ya Kingereza (AFROSAI -E) Hivyo, Ofisi inatumia Viwango vya Ukaguzi vya ISSAI pamoja na Viwango vya Kimataifa (ISA) vinavyotolewa na Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu (IFAC).

## 1.6 Sera ya Kihisibu

Kwa mujibu wa Kanuni ya 53 ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 (zilizorekebishwa 2004), Serikali imeweka taratibu za kihisibu ili kuhakikisha kwamba raslimali zinazoidhinishwa na Bunge zinatumiwa kwa usahihi. Kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Umma Na.6 ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004), Maafisa Masuuli wanapaswa kuhakikiksha kwamba mapato yote ya Umma yanaingizwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Pia malipo kutoka kwenye Mfuko huo yataidhinishwa kwa Sheria ya Bunge ya Matumizi kwa mwaka husika.

Taarifa za Fedha za Serikali kwa mwaka wa tatu zimetayarishwa kwa Viwango vya Kimataifa vya kutayarisha Taarifa za Fedha katika Sekta ya Umma [(IPSAS) - cash basis of accounting]. Katika mfumo huu, fedha inapopokelewa au matumizi kufanyika ndipo yanaingizwa vitabuni. Kadhalika, kwa vile mfumo huu hauna mizania, mali za kudumu zinaorodheshwa kwenye jedwali linaloambatana na taarifa ya fedha haziingizwi kwenye taarifa za fedha za Serikali. Hizi zinaingizwa kwenye vitabu kama matumizi kutokana na makisio ya mwaka mara vinaponunuliwa.

Kifungu cha 25(i) hadi (j) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004) inatoa ufafanuzi wa wa hesabu na taarifa zinazotakiwa kuandaliwa na Maafisa Wahasibu na kuwasilishwa kwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya ukaguzi

## 1.7 Wajibu wa Kisheria wa Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa na Balozi

Maafisa Masuuli ni wasimamizi wa rasilimali za Umma kwenye maeneo yao ya kazi kulingana na matakwa ya Kifungu Na. 8 cha Sheria ya Fedha za Umma Na. 6 ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004). Katika kulinda

rasilimali zilizo chini yao, suala la kuweka mifumo madhubuti na udhibiti wa ndani ni la umuhimu mkubwa.

## 1.8 Mfumo wa Udhibiti wa Ndani

Udhibiti wa ndani unamaanisha namna zote ambazo rasilimali za Serikali zinaelekezwa, zinasimamiwa na kupimwa. Udhibiti wa ndani unayo nafasi kubwa katika kuzuia na kugundua ubadhirifu/matumizi mabaya na kulinda rasilimali za Umma zilizo dhahiri na zisizo dhahiri. Kuangalia uzingatiaji wa udhibiti wa ndani ni jukumu la Mkaguzi wa Ndani ikimaanisha kwamba udhaifu katika utendaji wa kitengo cha ukaguzi wa ndani, ni sawa na udhaifu katika udhibiti wa ndani kiutendaji. Kanuni ya 34 ya Fedha za Umma inaonyesha majukumu yanayotakiwa kufanywa na Mkaguzi wa Ndani kuhusiana na mfumo wa udhibiti wa ndani. Vile vile, Kanuni ya 35 (2) ya Kanuni za Fedha za Umma inatilia mkazo wajibu wa menejimenti katika kuzuia na kugundua ubadhirifu.

## 1.9 Kutayarisha na kuwasilisha taarifa za fedha kwa kaguzi

Jukumu la kutayarisha na kuwasilisha hesabu za mwaka kwa Udhibiti wa Ndani wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni wajibu wa Maafisa Masuuli wa Serikali Kuu (Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa). Kifungu cha 25 cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebisha mwaka 2004); inataja aina ya hesabu mbalimbali anazotakiwa kutengeneza Mhasibu Mkuu wa Serikali, Maafisa Masuuli na Maafisa wengine wa Serikali waliokasimiwa Mifuko Maalumu iliyoanzishwa kisheria. Pia, Kifungu cha 25(4) cha sheria hiyo hiyo kinataka taarifa za fedha ziandaliwe kulingana na mifumo ya kihesabu iliyokubalika kimataifa na ni lazima misingi ya kihesabu iliyotumika iwekwe bayana. Kwa mwaka wa pili katika historia, taarifa za fedha za Wizara, Idara, Sekretarieti za Mikoa zimeandaliwa kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya kutayarisha taarifa za fedha katika sekta ya Umma ambayo inlandana na matakwa ya

kanuni Na. 53 ya Kanuni za Fedha za mwaka 2001 (zilizorekebisha 2004). Aidha, utaratibu huo umeanza katika Balozi kwa mara ya kwanza mwaka huu wa fedha.

Kanuni ya 8 (5) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 (zilizorekebisha 2004) inataka kila Wizara, Idara, Sekretarieti za Mikoa na Balozi kutengeneza na kutoa kwa Umma taarifa ya utekelezaji ya mwaka inayoeleza mikakati ya bajeti, aina na malengo ya kila mpango/programu, tathmini ya matokeo na mafanikio yakilinganishwa na malengo yaliyowekwa. Pia, Maafisa Masuuli wanatakiwa kutengeneza muhtasari wa matokeo ya matumizi ya fedha, kwa mwaka wa fedha unaohusika na kwa mfumo ulioidhinishwa na Mhasibu Mkuu wa Serikali, mipango ya mwaka ujao kama ilivyoidhinishwa na Bunge na mipango ya muda wa miaka miwili inayofuata. Baadhi ya Wizara, Idara, Sekretarieti za Mikoa na Balozi hazikutimiza wajibu huu.





## SURA YA 2

### MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YATOKANAYO NA HOJA ZA UKAGUZI KWA MIAKA ILIYOPITA

#### 2.0 Utangulizi

Serikali inawajibika kujibu kwa wakati hoja na mapendekezo yanayotolewa na Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kaguzi zote zinazotakiwa kufanywa chini ya Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 (iliyorekebisha 2005) na Sheria ya Ukaguzi Na. 11 ya 2008.

Sura hii inalenga kueleza matokeo ya mapitio ya utekelezaji wa mapendekezo yatokanayo na hoja za ukaguzi yaliyotolewa kwa Wizara, Idara, Sekretarieti za Mikoa na Balozi.

#### 2.1 Majibu kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)

Maafisa Wahasibu na Maafisa Wahasibu Wasaidizi wa Wizara, Idara, Sekretarieti za Mikoa na Balozi wanatakiwa kuandaa majibu ya ripoti ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Serikali kwa taarifa za fedha za Serikali Kuu na kuziwasilisha kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali.

Kwa mujibu wa kifungu cha 40(2) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 na Kanuni ya 38 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009, baada ya Mlipaji Mkuu wa Serikali kupokea majibu na mipango ya utekelezaji wa mapendekezo, atayajumuisha pamoja na kuyawasilisha kwa Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndani ya kipindi cha miezi mitatu.

Majibu jumuiifu ya Ripoti ya Serikali Kuu yalipokelewa na Ofisi yangu tarehe 30<sup>th</sup> July, 2010 yakiwa yamecheleweshwa kwa mwezi mmoja baada ya muda wa miezi 3 unaotakiwa kisheria. Aidha, mapendekezo mengi yaliyotolewa kwa

ripoti ya Serikali Kuu kwa miaka iliyopita hayakutekelezwa; hii ni dalili ya Serikali kutokuwa makini katika kutekeleza mapendekezo hayo.

Mapendekezo yafuatayo ambayo ni zaidi ya asilimia 50 ya mapendekezo yote yaliyotolewa kwa Serikali Kuu yalikuwa hayajatekelezwa kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini:-

S/No	Mapendekezo ambayo hayajatekelezwa
10.2 (i)	<p><b>Mapitio ya utaratibu wa kubakiza maduhuli yaliyokusanywa</b></p> <p>Makusanyo ya maduhuli katika Balozi zetu yanapaswa kudhibitiwa na Wizara ya Fedha, ikiwepo kuweka viwango vya kubakiza maduhuli. Kwa hali hii, ninamsisitiza Mlipaji Mkuu wa Serikali kuzingatia Ibara ya 135 ya Katiba ya Jamhuriya Muungano ya (1977) na Kifungu cha.11 cha Sheria ya Fedha ya 2001 (iliyorekebishwa 2004) ambayo inataka maduhuli yote ya Serikali kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali</p>
10.2(ii)	<p><b>Madeni na Mihadi isiyolipwa</b> <b>Shs.1,637,290,544,945</b></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Serikali iepuke kuingia katika mihadi huku ikijua hakuna fedha zilizotengwa. Aidha wakati umefika kwa Serikali kuwachukulia hatua kali Maafisa Wahasibu watakaoenda kinyume na matakwa ya mfumo wa bajeti unaoendeshwa kwa fedha taslim</li> <li>• Madeni ya jumla ya Sh.21,630,000,000 yanatakiwa kutambuliwa na kuingizwa katika Hesabu Jumuifu za Taifa</li> </ul>
10.2(iii)	<p><b>Usimamizi mbaya wa mali za Serikali</b></p> <p>Serikali ilinunua mashine za kuchapisha Visa kwa ajili ya Balozi za Tanzania nchi za nje. Mashine</p>

	<p>hizo hazitumiki kikamilifu katika Balozi nyingi kwa sababu ya ukiritimba wa teknolojia na hivyo kusababisha ugumu wa matengenezo pale zinapoharibika. Hii ina maana kuwa Serikali haikupata thamani halisi ya fedha kutokana na ununzi wa mashine hizo.</p>
10.2(iv)	<p><b>Balozi kupewa fedha kidogo kuliko mahitaji halisi</b></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Fedha zinazotolewa kwa ajili ya Balozi za Tanzania nchi za nje hazitoshi kugharamia matumizi ya kawaida na Maendeleo</li> <li>• Maduhuli yote yanayokusanywa na Balozi zetu yanapaswa kulipwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali</li> <li>• Utoaji fedha za matumizi kwa ajili ya Balozi za Tanzania nchi za nje uzingatie Sheria ya Matumizi (Appropriation Act) iliyopitishwa na Bunge</li> </ul>
10.2(v)	<p><b>Kufanyiwa marekebisho Kanuni za Utumishi za 1979 Balozini</b></p> <p>Iko haja ya haraka ya kufanyia marekebisho Kanuni za Utumishi za 1979 katika Balozi za Tanzania nchi za nje ili ziendane na wakati uliopo.</p>
10.2(vi)	<p><b>Umiliki wa ardhi na majengo</b></p> <p>Ardhi na majengo yanayomilikiwa na Balozi za Tanzania</p> <p>London, Nairobi na Maputo hayana Hati Miliki. Iko haja kwa Serikali kupitia Wakala wa Majengo (TBA) kuhakikisha kuwa umiliki wa ardhi na majengo katika Balozi hizo unarasimishwa.</p>
10.2(vii)	<p><b>Kuzingatiwa kwa Sheria ya Fedha</b></p> <p>Usimamizi wa fedha za sekta ya elimu nchini katika shule za msingi na sekondari unapaswa kuimarishwa. Vitendo vinavyosababisha uvunjifu</p>

10.2(viii)	<p>wa kanuni za fedha za sekta ya elimu ikiwa ni pamoja na matumizi mabaya vichukuliwe hatua kali kwani kuachia viendeleo ni kudidimiza maendeleo ya elimu nchini.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Hatua za kuondoa michango yenye usumbufu</b> Serikali ichukue hatua kali na za haraka kuhakikisha kuwa michango yenye usumbufu kwa wazazi inaondolewa kwani kuiacha iendeleo ni kuwaongezea wazazi mzigo wa kuwasomesha watoto wao.</li> <li>• Serikali inashauriwa kuhakikisha kuwa matumizi ambayo hayapo katika bajeti yanadhibitiwa. Aidha, Serikali ihakikishe kuwa fedha za kutosha zinaelekezwa katika Sekta ya Elimu ili kuepuka athari za kushuka kwa kiwango cha elimu nchini</li> <li>• Jitihada za makusudi zifanyike kupunguza tatizo la uhaba wa walimu katika shule hapa nchini, ongezeko linalokusudiwa lilenge pia kuwapata walimu wenye sifa stahiki</li> <li>• Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi izingatie viwango vya idadi ya walimu na watu wengine katika sekta ya elimu kama inavyoagizwa na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma.</li> </ul>
------------	--

	<ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Wizara ya Nishati na Madini kupewa fedha kwa wakati</b></li> </ul> <p>Suala la kuhakikisha kuwa Wizara ya Nishati na Madini inapewa fedha kwa wakati lina paswa kupewa umuhimu. Hazina kutoa fedha mwishoni wa mwaka wa fedha kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini ni wa kuepukwa</p>															
	<table border="1"> <thead> <tr> <th>Mwaka</th> <th>Toleo la fedha Na.</th> <th>Kiasi</th> <th>Tarehe ya kutoa fedha</th> <th>Maoni</th> </tr> </thead> <tbody> <tr> <td>2007/2008</td> <td>58/EB/AG/159/071/516</td> <td>180,000,000</td> <td>20/6/2008</td> <td>Siku 10 kabla ya mwaka wa fedha kwisha</td> </tr> <tr> <td>2008/2009</td> <td>58/EB/AG/159/08/606</td> <td>7,500,000,000</td> <td>25/6/2009</td> <td>Siku 5 kabla ya mwaka wa fedha kwisha</td> </tr> </tbody> </table>	Mwaka	Toleo la fedha Na.	Kiasi	Tarehe ya kutoa fedha	Maoni	2007/2008	58/EB/AG/159/071/516	180,000,000	20/6/2008	Siku 10 kabla ya mwaka wa fedha kwisha	2008/2009	58/EB/AG/159/08/606	7,500,000,000	25/6/2009	Siku 5 kabla ya mwaka wa fedha kwisha
Mwaka	Toleo la fedha Na.	Kiasi	Tarehe ya kutoa fedha	Maoni												
2007/2008	58/EB/AG/159/071/516	180,000,000	20/6/2008	Siku 10 kabla ya mwaka wa fedha kwisha												
2008/2009	58/EB/AG/159/08/606	7,500,000,000	25/6/2009	Siku 5 kabla ya mwaka wa fedha kwisha												
10.2(ix)	<p><b>Kutayarisha na kufuatwa kikamilifu kwa mpango wa mwaka wa manunuzi</b></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Inapendekezwa kuwa mwaka wa fedha ujao rasilmali zaidi zielekezwe katika kuhakikisha kuwa usimamizi wa mikataba unaimarishwa. Aidha, mafunzo ya ujumla ya Sheria ya Manunuzi yalenge katika eneo hili la usimamizi bora wa mikataba</li> <li>• Inapendekezwa kuwa watumishi katika kitengo cha manunuzi wapewe mafunzo katika utunzaji wa kumbukumbu. Aidha, miongozo ya namna ya kutunza nyaraka na kumbukumbu mbalimbali (inatayarishwa na PPRA) inapaswa kusambazwa katika Taasisi zote zinazofanya manunuzi (PEs)</li> </ul>															
10.2(ix)	<p><b>Masuala ya Kodi</b></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Pamoja na kwamba walipa kodi wanayo haki kisheria kwenda katika Mahakama za kawaida ili kupata haki katika masuala ya kodi, uongozi wa TRA unashauriwa kushauriana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Jaji Mkuu ili kesi au rufaa</li> </ul>															

	<p>zote za kodi zishughulikiwe na Bodi ya Rufaa za Kodi kwa upande wa kesi za rufaa au Mahakama Kuu - Kitengo cha Mahakama ya Biashara kwani hivi ndio vyombo vyenye dhamana kubwa zaidi ya kushughulikia masuala ya kodi.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Mfumo wa uangalizi na udhibiti wa ndani katika Mamlaka ya Mapato unapaswa kuimarishwa ili kuhakikisha kuwa marejesho za mapato na malipo ya kodi vinapitiwa kwa makini ili kubaini udanganyifu na mianya ya ukwepaji kodi kwa lengo la kuongeza mapato yatokanayo na kodi na kuzuia matumizi mabaya ya fedha za Serikali.</li> <li>• Serikali inashauriwa kuchunguza sababu zilizofanya TRA ishindwe kukusanya kiasi kilichokadiriwa katika bajeti yake, na kwa kushauriana na TRA ije na hatua madhubuti zitakazoondoa tatizo hilo la kutofikia malengo katika ukusanyaji mapato.</li> <li>• Kwa kuwa Balozi zetu nchi za nje zinaruhusiwa kisheria kubakiza sehemu ya fedha zinazokusanya na kuzitumia kufidia pengo litokanalo na upungufu wa bajeti zake, ninaishauri Serikali kwamba salio la maduhuli katika Balozi zetu liwasilishwe kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali na kuingizwa katika hesabu jumuiifu za maduhuli.</li> <li>• Uhamisho wa fedha kutoka katika Ofisi ndogo za Ubalazi kwenda katika Balozi nyingine udhibitiwe na Wizara ya Fedha na Uchumi.</li> </ul>
--	---

10.2(x)	<p><b>Daraja la Umoja</b></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Kuna haja ya kuwekwa miundombinu muhimu katika eneo la daraja. Kinahitajika kituo kidogo cha polisi, forodha, na huduma za uhamiaji katika eneo la daraja. Kwa kuanzia, kuna jengo la ofisi na nyumba za watumishi pembezoni mwa barabara ambazo zilikuwa zinatumiwa na mkandarasi ambazo zinaweza kutumiwa kwa muda kwa ajili ya kuweka miundombinu na kutoa huduma za forodha, uhamiaji na kituo kidogo cha polisi.</li> <li>• Ili kunufaika zaidi na Daraja la Umoja, Serikali zote mbili hazina budi kugharamia ujenzi wa barabara ya lami kutoka eneo la daraja kwenda Masasi-Tunduma (umbali wa Kilometa 70) na kuelekea katika Makao Makuu ya Wilaya iliyoko karibu nchini Msumbiji (wastani wa umbali wa Kilometa 165). Hii itarahisisha usafiri kuelekea kwenye daraja na kuwawezesha watumiaji zaidi kulitumia daraja.</li> <li>• Kwa kuwa ujenzi wa daraja uliogharimu zaidi ya Dola za Kimarekeni 27.0 milioni umegharamiwa kwa asilimia 100 na Serikali za nchi hizi mbili, na kwa kuwa watumiaji wengi wa daraja hili hawatakuwa ni wananchi wa Tanzania na Msumbiji peke yake, kuna haja ya kuanzisha ushuru utakaotozwa magari yote yatakayovuka katika daraja na kwa hali hiyo, ni vyema ikafikiriwa kujengwa kituo cha kukusanya ushuru.</li> <li>• Kati ya pande mbili za daraja, upande wa Tanzania unaonekana kuwa na uhai zaidi kiuchumi. Uongozi wa halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu uhimizwe kuwatafuta wawekezaji ambao watawekeza katika eneo hilo ili kuinua hali ya uchumi katika halmashauri hiyo na taifa kwa ujumla.</li> </ul>
---------	--



## 2.2 Masuala ya kaguzi za miaka ya nyuma yasiyoshughulikiwa

Ofisi za Wizara, Idara, Sekretarieti za Mikoa na Balozi zimekuwa na maendeleo mazuri katika utekelezaji wa masuala ya kaguzi za nyuma. Hata hivyo, katika mwaka huu wa ukaguzi, Wizara, Idara, Sekretarieti za Mikoa 46 zilikuwa hazijashughulikia masuala ya miaka ya nyuma yenye jumla ya Sh 468,627,883,842. Kati ya kiasi hicho, Wizara ya Fedha inaongoza kwa kiasi kikubwa cha Sh 361,327,312,329.79 ikifuatiwa na Idara ya Magereza yenye Sh. 19,261,840,595 wakati Sekretarieti ya Mkoa wa Lindi ikiwa ya tatu yenye Sh. 10,146,855,167. (Kiambatisho I)

Balozi zilikuwa na masuala yasiyojibiwa yenye thamani ya Sh. 11,286,222,839, Dola za Kimarekani 335,586, Paundi za Kiingereza 79,567.82, Euro 1,550,208, Dinari 12,554,84, Riyal za Oman 69,844,847 na Faranga za Uswisi 1000.

Muhtasari wa ulinganisho wa masuala ya ukaguzi yasiyoshughulikiwa kwa 2008/2009 na 2009/2010 ni huu ufuatao:-

Mwaka wa fedha	2008/2009	2009/2010
TShs	1,055,460,602,544	11,286,222,839
JPY	17,089,499,858	699,000,000
USD	2,100,000	2,326,580
GBP	-	79,567.82
EURO	-	1,550,208
OMR	-	69,844,847
CHF	-	1,000
SAR	-	25,572,480

Lengo la kuwasilisha matokeo ya ukaguzi pamoja na mapendekezo kwa mkaguliwa ni kumsaidia mkaguliwa kurekebisha kasoro zilizojitokeza katika usimamizi wa fedha na udhibiti wa mali katika Wizara, Idara, Wakala, Sekretarieti za Mikoa na Balozi. Kutojibiwa

kwa hoja na mapendekezo ya ukaguzi kama inavyoonekana katika Wizara, Idara, Wakala, Sekretarieti za Mikoa na Balozini kosa kubwa kwa Maafisa Wahasibu wa taasisi hizo.

kutoshughulikiwa kwa hoja na mapendekezo ya ukaguzi kunasababisha kasoro zilizojitokeza wakati wa ukaguzi kujirudia katika miaka inayofuata. Pia, hii inaonyesha kutowajibika kikamilifu kwa Maafisa Wahasibu na uongozi wa taasisi husika. Orodha ya Masuala ya miaka ya nyuma yasiyojibiwa yako kwenye **Kiambatisho Na. I** katika ripoti hii.

Muhtasari uliotolewa hapo juu unaonyesha jumla ya masuala yasiyoshughulikiwa kwa mwaka 2008/09 yaliyohusu Wizara, Idara, Sekretarieti za Mikoa yalikuwa na thamani ya Sh 1,055,460,602,544, JPY 17,089,499,858 na USD2,100,000. Katika mwaka 2009/10 jumla ya Wizara, Idara, Idara, na Sekretarieti za Mikoa zenye masuala yasiyoshughulikiwa ilipanda kutoka 37 hadi 46 na kiasi kilichohusika pia kilipanda na kufikia Sh 468,627,883,842, JPY 699,000,000. Aidha, Dola za Kimarekani ziliongezeka hadi kufikia 2,326,580. Kwa hali hiyo, thamani ya masuala yasiyoshughulikiwa iliongezeka katika mwaka 2009/10 ikilinganishwa na mwaka 2008/09

Mchanganuo huu unaonyesha kwamba Menejimenti za Wizara, Idara, Sekretarieti za Mikoa na Ofisi za Balozini hazikufanya jitihada za kutosha kushughulikia mapendekezo ya ukaguzi. **Kiambatisho Na. I** katika ripoti hii ni orodha ya Wizara, Idara, Idara, na Sekretarieti za Mikoa na thamani ya masuala ya nyuma yasiyoshughulikiwa.



## SURA YA 3

### MAKUSANYO YA MADUHILI NA MCHANGANUO WA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO

#### 3.1 Utangulizi

Sehemu hii inatoa mchanganuo wa kina wa ugharimiaji wa Wizara, Idara, Sekretarieti za Mikoa kwa mwaka 2008/2009 na 2009/2010. Wizara, Idara, Sekretarieti za Mikoa na Balozzi kwa kiasi kikubwa zinapata fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kupitia Hazina.


#### 3.2.1 Ulinganisho wa fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na matumizi halisi ya Kawaida katika Wizara, Idara, Sekretarieti za Mikoa na Balozzi

Taarifa za fedha zinaonyesha kwamba, jumla ya fedha zilizotolewa na Hazina kwa ajili ya matumizi ya kawaida katika mwaka wa fedha 2008/2009 zilikuwa Sh. 3,590,968,044,750 wakati matumizi halisi yalikuwa Sh. 3,533,021,852,627. Kwa upande mwingine, fedha zilizotolewa na Hazina kwenda Wizara, Idara, Sekretarieti za Mikoa katika mwaka wa fedha 2009/10 zilikuwa Sh. 6,251,629,581,428 wakati matumizi halisi yalikuwa ni Sh. 6,237,494,869,945 (Kiambatanisho II)

Taarifa hii imeonyeshwa kwenye muhtassari kama ifuatavyo:

	2008/09	2009/10
Fedha zilizotolewa (Sh)	3,590,968,044,750	6,251,629,581,428
Matumizi halisi (Sh)	3,533,021,852,627	6,237,494,869,945
Tofauti (Sh)	57,946,192,123	14,134,711,483

Pia taarifa hiyo hapo juu imeonyeshwa katika chati mhimili hapa chini



kwenye histogramu hapa chini:-

### 3.2.2 Ulinganisho wa Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo zilizotolewa na Hazina kwa ajili ya Wizara, Idara, kwa miaka ya fedha 2008/2009 na 2009/2010

Kumbukumbu zinaonyesha kwamba jumla ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mwaka 2008/2009 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni Sh 4,952,445,794,870 na kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ni Sh. 1,635,263,360,853 kukiwa na tofauti ya Sh. 3,317,182,434,017 (67%).


Pia, fedha kutoka Mfuko Mkuu kwa matumizi kama hayo katika mwaka 2009/2010 yalikuwa ni Sh. 6,251,629,581,428 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. 2,299,010,652,135

kwa ajili ya matumizi ya maendeleo kukiwa na tofauti ya Sh. 3,952,618,929,293 (sawa na asilimia 63.2%)

Mchanganuo huo umewekwa katika jedwali lifuatalo:-

Mwaka wa fedha	Fedha kwa Shughuli za kawaida (Sh)	Fedha kwa shughuli za Maendeleo (Sh)
2008/09	4,952,445,794,870	1,635,263,360,853
2009/10	6,251,629,581,428	2,299,010,652,135

Pia taarifa hiyo hapo juu imeonyeshwa kwenye chati mhimili kama ifuatayo:



### 3.2.3 Ulinganisho wa bajeti dhidi ya fedha zilizotolewa na Hazina kwa ajili ya maendeleo katika Wizara na Idara


Bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya maendeleo katika Wizara na Idara kwa mwaka 2008/2009 ilikuwa Sh. 2,268,306,465,161 ambapo kiasi kilichotolewa na Hazina kilikuwa Sh. 1,635,263,360,853 ikiwa ni upungufu wa Sh. 633,043,104,308 sawa na asilimia 27.9

Aidha, bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo kwa Wizara na Idara katika mwaka 2009/2010 ilikuwa Sh. 3,004,100,724,639 ambapo fedha zilizotolewa na Hazina zilikuwa Sh. 2,299,010,652,135 hivyo kusababisha ugharamiaji pungufu kwa Sh. 705,090,072,504 (23.5 %).

**Muhtasari wa bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo katika Mafungu ya Wizara**

Mwaka	Bajeti iliyoidhinishwa (Sh.)	Fedha halisi zilizotolewa (Sh.)	Tofauti (Sh.)
2008/2009	2,268,306,465,161	1,635,263,360,853	633,043,104,308
2009/2010	3,004,100,724,639	2,299,010,652,135	705,090,072,504

Kutokana na jedwali hapo juu, inaweza kuhitimishwa kwamba, shughuli za maendeleo za jumla ya Sh. 705,090,072,504 au asilimia 23.5 hazikutekelezwa katika mwaka wa fedha 2009/10 ikilinganishwa na kiasi ambacho hakikutolewa na Hazina cha Sh. 633,043,104,308 au asilimia 27.9 katika mwaka 2008/2009. Hii inadhihirisha kwamba, shughuli za maendeleo za kiasi hicho cha fedha hazikutekelezwa Taarifa kwenye jedwali hilo hapo juu pia imeonyeshwa kwenye chati mhimili kama ifuatavyo:



Kutokana na uchambuzi na chati mhimili hapo juu, ni dhahiri kuwa kuna tatizo kubwa katika ugharimiaji wa shughuli za maendeleo ambapo fedha zinazotolewa na Hazina kugharamia miradi ya maendeleo zimeendelea kupungua ikilinganishwa na bajeti iliyopitishwa na bunge.

#### **3.2.4 Matokeo ya ukaguzi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania**

Mamlaka ya Mapato Tanzania imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria na.15 ya mwaka 1995 kama ilivyorekebishwa na Sheria Na.8 ya mwaka 1996 ikiwa na majukumu ya kusimamia ukusanyaji wa kodi za Serikali kuu pamoja na ukusanyaji wa mapato mbalimbali ya Serikali. Tangu kuanzishwa kwake, Mamlaka ya Mapato Tanzania imekuwa ikitayarisha hesabu zilizokuwa zikionesha Mapato na Matumizi. Aidha, kuanzia mwaka wa fedha 2008/2009, Mamlaka ya Mapato Tanzania imeanza kutayarisha aina mbili za Taarifa za Hesabu ambazo ni zile za Mapato na Taarifa ya Hesabu za Matumizi.

#### **3.2.5 Masuala ya miaka iliyopita yasiyojibiwa**

Hadi kufikia wakati wa kutoa taarifa yangu kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (Disemba 31, 2010) Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikuwa na masuala mbalimbali ya ukaguzi yaliyoripotiwa katika taarifa zilizopita yaliyofikia kiasi cha sh 220,292,054,615 na Dola za Kimarekani 47,255,243 kama yalivyoainishwa hapa chini hayakuwa yameshughulikiwa kikamilifu.



Idara	Kiasi (Sh.)	Kiasi (Dola za Kimarekani)
Ushuru wa Forodha	22,969,924,801	-
Idara ya Kodi za ndani	16,207,984,641	-
Idara ya walipa kodi wakubwa	181,114,145,173	47,255,243
<b>Jumla</b>	<b>220,292,054,615</b>	<b>47,255,243</b>

Baadhi ya masuala yaliyoainishwa kwenye jedwali yamesalia bila kujibiwa kikamilifu tangu mwaka 2001/2002 na baadhi yake yanasubiri maamuzi ya Mahakama.

#### **Ukusanyaji wa Mapato**

Hesabu za Mapato yaliyokusanywa Tanzania Bara yalifikia kiasi cha sh 4,637,513,963,999 ikilinganishwa na makisio ya sh 5,028,922,100,000 ikiwa ni makusanyo pungufu kwa kiasi cha Sh. 391,408,136,001 sawa na asilimia 8% ya Makisio ya Mapato ya Mwaka. Kwa upande wa Zanzibar, mapato yaliyokusanywa ni kiasi cha Sh. 59,998,034,392 ikilinganishwa na Makisio ya Mapato ya Sh. 63,234,200,000; hali inayo oneshwa makusanyo pungufu ya Sh. 3,236,165,608 sawa na asilimia 5 ya makisio ya Mapato ya mwaka.

Mchanganuo wa makusanyo ya mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania kupitia idara zake mbalimbali ni kama yalivyoainishwa katika jedwali hili hapa chini:-

## Tanzania Bara

Idara (a)	Lengo (a) Sh.	Makusanyo halisi (b) Sh.	Ziada/Pungufu ya Makusanyo (c) = (b-a) Sh.	% (c/a)
Idara ya Kodi za Ndani	801,335,700,000	817,503,772,367	16,168,072,367	2
Idara ya Walipa kodi Wakubwa	2,104,570,900,000	1,812,264,222,572	-292,306,677,428	-14
Ushuru wa Forodha	2,079,338,700,000	1,974,699,982,914	-104,638,717,086	-5
Jumla ndogo	4,985,245,300,000	4,604,467,977,853	-380,777,322,147	-8
Ongeza: Vocha za Hazina	43,676,800,000	33,045,986,146	-10,630,813,854	-24
Jumla Kuu	5,028,922,100,000	4,637,513,963,999	-391,408,136,001	-8

## Zanzibar


Idara	Lengo (a) Sh.	Makusanyo halisi (b) Sh.	Ziada/Pungufu ya Makusanyo (c) = (b-a) Sh.	% (c/a)
Idara ya Kodi za ndani	24,397,700,000	24,602,517,602	204,817,602	1
Ushuru wa Forodha	38,836,500,000	35,395,516,790	-3,440,983,210	-9
Jumla ndogo	63,234,200,000	59,998,034,392	-3,236,165,608	-5

Mwelekeo wa makusanyo ya mapato kwa pande mbili za Serikali - yaani Tanzania Bara na Zanzibar kwa miaka mitatu mfululizo ni kama ifuatavyo:-

## Tanzania Bara

Mwaka	Lengo (a) Sh.	Makusanyo halisi (b) Sh.	Tofauti (c) = (b-a) Sh.	% (c/a)
2006/2007	3,426,255,700,000	3,512,810,000,613	86,554,300,613	2.5
2007/2008	4,600,849,900,000	4,174,371,105,259	426,478,794,741	-9.3
2008/2009	5,028,922,100,000	4,637,686,999,618	391,235,100,382	-8


Mwelekeo huo wa makusanyo unaweza kuonyeshwa katika chati mhimili kama ifuatavyo:



### Zanzibar

Mwaka	Lengo (a) Sh.	Makusanyo Halisi (b) Sh.	Tofauti (c) = (b-a) Sh.	% (c/a)
2007/2008	36,179,800,000	39,858,524,813	3,678,724,813	10.16
2008/2009	49,220,900,000	53,877,284,997	4,656,384,997	9.5
2009/2010	63,234,200,000	59,998,034,392	-3,236,165,608	-5

Mwelekeo huo wa makusanyo kwa upande wa Zanzibar unaweza kuonyeshwa katika chati mhimili kama ifuatavyo:



Matokeo ya makusanyo ya Mapato kwa miaka mitatu iliyopita yanaonyesha kuwa Tanzania Bara imekuwa ikifanya vizuri mwaka hadi mwaka, kwani makisio yamekuwa yakiongezeka hali kadhalika makusanyo ya mapato nayo yamekuwa yakiongezeka. Aidha, katika mwaka wa fedha 2009/2010 makusanyo ya mapato yamekuwa chini ya makisio kwa asilimia 8. Menejimenti ya Mamlaka ya Mapato Tanzania imeonyesha sababu za kushuka kwa makusanyo ya mapato kumetokana na Serikali kuweka malengo ya juu zaidi ya makusanyo bila kuinisha vyanzo vipya vya kodi na sababu nyingine ni utekelezaji wa makubaliano ya kuwa na viwango sawa vya kutoza ushuru wa forodha kutoka nchi moja kwenda nyingine kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kwa upande mwingine, makusanyo ya mapato Zanzibar yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka. Hata hivyo, katika mwaka 2009/2010 kulikuwa na ongezeko kubwa la makadirio ya makusanyo ya maduhuli ikilinganishwa na miaka miwili iliyopita, jambo lililosababisha malengo ya ukusanyaji kutofikiwa kwa asilimia 5.

Sababu zilizochangia mafanikio katika ongezeko la mapato mwaka hadi mwaka ni hatua zilizochukuliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania kuimarisha udhibiti wa ndani hasa misamaha ya kodi ambayo imepunguzwa kwa kiasi kikubwa katika kipindi cha miaka mitatu. Aidha, kumekuwepo ongezeko kubwa la mapato yatokanayo na kodi za mapato kutokana na mageuzi katika kodi ya ajira yaliyofanywa tangu mwaka 2008/2009 na punguzo la nakisi ya kodi kwa sekta ya makampuni. Hali kadhalika, Mkakati wa kukuza Uchumi Zanzibar (MKUZA) umesababisha kuwepo vianzio vingi vya mapato hasa katika sekta zinazokua haraka za utalii na mawasiliano.

### 3.2.6 Misamaha ya Kodi Sh. 680,667,900,000

Mamlaka ya Mapato Tanzania imeonyesha kuwa kiasi cha Sh 680,667,900,000 kilikuwa ni misamaha ya kodi iliyotolewa kwa Taasisi mbali mbali na watu binafsi kama inavyoonekana hapa chini:

Taasisi	Idara ya Forodha (Sh )	Idara ya Kodi za ndani (Sh)	Jumla (Sh)
Taasisi za Serikali	52,743,800,000		52,743,800,000
Mashirika ya Umma	8,758,700,000		8,758,700,000
Taasisi za Kidini	281,200,000		281,200,000
Taasisi zisizo za KiSerikali	22,147,100,000		22,147,100,000
Miradi ya Wafadhili	72,458,100,000		72,458,100,000
Makampuni na watu binafsi	36,174,600,000		36,174,600,000
Sekta ya Madini	48,738,600,000		48,738,600,000
Kituo cha Uwekezaji Tanzania	268,002,300,000		268,002,300,000
Misamaha ya kodi za Ongezeko la Thamani	-	168,671,900,000	168,671,900,000
Misamaha ya Kodi katika Maduka yasitozwa kodi	-	2,691,600,000	2,691,600,000
<b>Jumla</b>	<b>509,304,400,000</b>	<b>171,363,500,000</b>	<b>680,667,900,000</b>

Endapo kiasi hiki cha Sh. 680,667,900,000 ambacho ni sawa na asilimia 14.7 ya makusanyo yote kingekusanywa, ni dhahiri kuwa kiasi cha Sh. 391,235,100,382 kilichokusanywa pungufu kwa Tanzania Bara kisingekuwepo na badala yake kungekuwepo ziada ya Sh.289,432,799,618.



## SURA YA 4

### MATOKEO YA UKAGUZI WA AWALI WA MALIPO YA UZEENI

#### 4.0 Utangulizi

Ukaguzi wa awali wa mafao ya wastaafu unafanywa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Kifungu cha 29 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008. Kifungu cha 5 (a) cha Sheria hiyo hiyo ya Ukaguzi kinamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhakikisha kwamba fedha zinazokusudiwa kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali, matumizi yake yawe yameidhinishwa na kwamba zitatolewa kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 136 ya Katiba, na iwapo ataridhika kwamba masharti hayo yatatekelezwa ipasavyo, basi ataidhinisha fedha hizo zitolewe. Kutokana na ukweli kuwa malipo ya pensheni hulipwa bila makadirio yake kuidhinishwa na Bunge, ni vyema Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu akafanya ukaguzi wa awali kwa malipo hayo ya mafao ya wastaafu ambayo si rahisi kukadiriwa kwa uhakika na kutengewa fedha.

#### 4.1 Madhumuni ya ukaguzi wa awali

Lengo la kufanya ukaguzi wa awali wa mafao ya wastaafu ni kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kuweza kuhakiki usahihi wa malipo hayo na kuzuia au kubaini makosa mapema kwa nia ya kulinda fedha za Serikali na wakati huo huo, kuhakikisha kuwa wastaafu wanalipwa kile wanachostahili. Ukaguzi wa awali ni muhimu kwa kuwa malipo yasiyo sahihi yakifanywa kwa wastaafu inakuwa vigumu kwa Serikali kuyarejesha kutoka kwa wastaafu hao.

Pia ni wajibu wangu kuona kuwa Sheria na kanuni za mafao na sera za kazi zilizopo kuhusiana na mawasiliano ya kiutendaji, muundo wa utumishi wa mfumo wa mishahara unazingatiwa.



## 4.2 Mawanda ya ukaguzi wa awali

Matokeo ya ukaguzi na mapendekezo yaliyomo katika ripoti hii hayawahusu watumishi ambao mafao yao ya uzeeni yanashughulikiwa na Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Serikali (PSPF) na Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Mashirika ya Umma (LAPF). Ukaguzi wa awali wa mafao ya uzeeni unahusisha makundi yafuatayo:

- Maafisa wa Jeshi na Maafisa Usalama.
- Malipo ya Mikataba kwa Viongozi wa Kisiasa, wasiokuwa raia na wastaafu walioko kwenye ajira ya mkataba.
- Watumishi wa Serikali wasio na stahili ya pensheni ambao hulipwa fidia ya kiinua mgogo
- Mafao ya askari Polisi wa ngazi za chini
- Pensheni kwa Watumishi wa Serikali, waliotakiwa kulipwa kabla ya tarehe 1 Julai, 2004 lakini bado hawajalipwa

## 4.3 Matokeo ya ukaguzi na mapendekezo

### 4.3.1 Matokeo

Katika mwaka 2008/2009 Ofisi yangu ilianza na majalada 37 ya pensheni ikiwa ni bakaa kutoka mwaka 2008/2009. Jumla ya majalada 4,955 ya wastaafu yaliwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi na kufanya idadi ya majalada yote katika kipindi husika kuwa 4,960. Kati ya majalada yote yaliyokuwepo, majalada 4,960 yalikaguliwa, 325 yalirudishwa kwa Maafisa Masuuli kwa marekebisho na hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2010 majalada 32 yalikuwa yakiendelea kukaguliwa kama inavyoonyeshwa kwa ufupi hapa chini:

Mchanganuo	Majalada
Salio la nyuma 1 Julai, 2009	37
Majalada yaliyopokelewa katika mwaka	4,955
Majalada yaliyokuwepo kwa ajili ya ukaguzi	4,992
Majalada yaliyokaguliwa	4,960
Salio la majalada tarehe 30 Juni, 2010	32

#### 4.3.2 Ukokotoaji zaidi au pungufu wa mafao ya wastaafu

Majalada yaliyowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi yameonyesha kuwepo kwa makosa katika ukokotoaji wa mafao ya baadhi ya wastaafu. Makosa hayo yangesababisha mafao kulipwa zaidi au pungufu ya stahili ya mstaafu. Kwa mfano, kati ya majalada 4,960 ya pensheni yaliyokaguliwa, 164 yangelipwa zaidi kwa kiasi cha Sh. 301,506,150.5 wakati majalada 137 yangelipwa pungufu kwa kiasi cha Sh. 167,430,608.06 kama yalivyoonyeshwa hapa chini:-

##### (i) Fedha zilizozidishwa

Na.	Maelezo	Idadi ya kadhia	Kiasi (Sh.)
1.	Muda uliozidishwa	65	125,412,559.90
2.	Makosa katika ukokotoaji	63	156,695,038.70
3.	Mishahara iliyozidishwa	36	19,398,551.90
	<b>Jumla</b>	<b>164</b>	<b>301,506,150.50</b>

##### (ii) Kiasi kilichopunjwa

Na.	Maelezo	Idadi ya watumishi	Kiasi (Sh.)
1.	Kipindi kilicho punjwa	63	47,866,985.77
2.	Makosa katika ukokotoaji	9	24,214,863.55
3.	Mishahara iliyopunjwa	65	95,348,758.74
	<b>Jumla Sh.</b>	<b>137</b>	<b>167,430,608.06</b>

Kutokana na mchanganuo huo hapo juu, endapo malipo ya uzeeni yasingekaguliwa kabla ya kulipwa, Serikali ingepata

hasara ya Sh. 301, 506,150.5 wakati wastaafu wangepata malipo pungufu ya jumla ya Sh. 167,430,608.06. Kasoro zote mbili katika ukokotoaji zikichukuliwa kwa pamoja zingeisababishia Serikali hasara halisi ya Sh. 134,075,542.44.

#### **4.3.3 Changamoto zilizojitokeza wakati wa ukaguzi**

Wakati wa ukaguzi zilijitokeza changamoto ambazo zinaweza kuainishwa katika makundi matatu yafuatayo:

- (i) Matatizo ya utendaji,
- (ii) Tafsiri zisizo sahihi za Sheria za Panseni na Kanuni zake,
- (iii) Kasoro za kiutawala

Matokeo muhimu ya ukaguzi wa mafao ya uzeeni ni haya yafuatayo:-

- (i) Kutumia mshahara usio sahihi katika kukokotoa mafao
- (ii) Kuchanganya sheria za pensheni na zile za ajira za mikataba
- (iii) Kutozingatia Sheria za pensheni
- (iv) Kuchelewa kuwasilisha majalada ya wastaafu kwa ajili ya ukaguzi
- (v) Majalada kutokukamilika na kukosa nyaraka muhimu za kuthibitisha mafao ya kulipwa
- (vi) Kutokuwa na stahili ya kulipwa mafao
- (vii) Mkanganyiko kuhusu sheria inayotakiwa kutumiwa kulipa mafao ya pensheni

#### **4.3.4 Utumiaji wa mishahara isiyosahihi wakati wa kuandaa mafao ya mwisho**

Sheria ya Pansheni inaelekeza mshahara wa mwisho wa mtumishi akiwa kwenye ajira ya Umma ndio utumike

wakati wa kuandaa mafao ya mstaafu. Hata hivyo, imeonekana kuwa baadhi ya watumishi waliokuwa Serikalini waliteuliwa katika nafasi mbalimbali katika Mashirika ya Umma au uongozi wa kisiasa na hivyo kupokea mishahara iliyoko katika vyeo hivyo. Sio sahihi kisheria mishahara hiyo ya uteuzi katika mashirika na siasa kutumika kukokotoa mafao ya pensheni kwa wastaafu badala ya ile ya mwisho katika utumishi wa Umma.

Wakati wa kustaafu, baadhi ya wastaafu wamekuwa wakidai kuwa ukokotoaji wa mafao yao ufanyike kwa kutumia mishahara yao ya wakati wa kustaafu kinyume na sheria za pensheni kwani ajira zao zinasimamiwa na sheria tofauti za pensheni.

#### 4.3.5 Madai mara mbili ya mafao ya kustaafu (pensheni na ajira ya mikataba)

Baadhi ya watumishi wa Umma, wakati wa kipindi cha ajira zao waliteuliwa katika nyadhifa mbalimbali za mikataba lakini wakaendelea kubaki na hadhi yao kama waajiriwa wa kudumu na masharti ya pensheni. Wakati wa kustaafu watumishi wa namna hii wanaweza kuishia kulipwa kiinua mgongo kwa ajira ya mkataba pamoja na mafao ya uzeeni. Hii ni kinyume na sheria za pensheni kwani watakuwa wamelipwa mara mbili.

- Baadhi ya watumishi waliokuwa katika ajira za mikataba walikuwa wameandikishwa kama wanachama wa Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma (PSPF) kama maafisa walio katika masharti ya pensheni na hivyo kuchangia katika mfuko huo. Hii ni kinyume na sheria za pensheni kwani maafisa hawa hawana sifa ya kuchangia katika mfuko na kulipwa pensheni na PSPF.
- Wakati wa ukaguzi, ilibainika kuwa maafisa wa jeshi waliokuwa wameteuliwa katika nyadhifa za uongozi wa kisiasa waliendelea kuwa na nyadhifa zao za kijeshi kinyume na maagizo yaliyotolewa na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa

Tanzania na Katibu Mkuu Kiongozi yaliyowataka kujiuzulu vyeo vyao vya kijeshi mara tu baada ya uteuzi katika nyadhifa za kisiasa. Suala muhimu hapa ni kuhakikisha kuwa muda wa utumishi katika jeshi unalipwa pensheni na muda ambao mstaafu ametumikia uongozi wa kisiasa unalipwa tuzo ya mkataba. Hata hivyo, uzoefu umeonyesha kuwa utaratibu huo haufuatwi na hivyo kusababisha malipo mara mbili kwa maafisa wahusika; kwa mfano:

- Maafisa wa jeshi wanaopata ajira za kisiasa hawaachi utumishi wao jeshini hadi wanapofikia umri wa kustaafu katika jeshi na hivyo kusababisha ukokotoaji wa mafao yao ya kustaafu kujumuisha muda ambao wametumikia vyeo katika siasa. Matokeo yake, maafisa hawa huishia kulipwa pensheni.
- Imeonekana pia kuwa baadhi ya maafisa wastaafu wamerejeshwa tena kazini na hivyo kulazimika kurudisha barua zao za kustaafu. Hali hii inampa mstaafu husika haki ya kunufaika na sheria za pensheni zilizopo na hivyo kufanya pawepo na ongezeko la mafao ya uzeeni na malipo ya malimbikizo ya mishahara. Hii ni kinyume na sheria za pensheni ambazo zinataka mstaafu alipwe kulingana na masharti ya ajira yake na sheria za pensheni zilizopo kwa wakati huo. Kwa mfano, kuidhinisha mstaafu kulipwa mafao ya uzeeni kwa msingi wa sheria za pensheni zilizopo badala ya zile zilizofutwa.

#### **4.3.6 Kutozingatia sheria za Pensheni**

Imeonekana kuwa baadhi ya watumishi walioazimwa kwenda katika taasisi mbalimbali hudai mafao yao ya uzeeni yatawaliwe na sheria za pensheni za taasisi zilizowaazima jambo ambalo si sahihi.

#### **4.3.7 Ucheleweshaji wa kuwasilisha majalada kwa ajili ya ukaguzi**

Sheria ya Pensheni inataka mchakato wa kulipa mafao ya wastaafu kuanza miezi 6 kabla ya mtumishi kustaafu.

Utaratibu huu unalenga kukamilisha maandalizi ya malipo mapema na kulipwa kwa wakati. Kinyume na hivyo, baadhi ya majalada yanaletwa ukaguzi baada ya miezi kadhaa na mara nyingine baada ya mwaka kupita kutokea mtumishi alipostaafu.

#### 4.3.8 Kutokamilika kwa nyaraka za wastaafu

Baadhi ya majalada ya wastaafu huletwa kwa ajili ya ukaguzi wa awali yakiwa na nyaraka pungufu. Katika hali hii, inanilazimu kurudisha majalada hayo kwa ajili ya marekebisho. Hivyo basi, lengo la kulipa mafao kwa wakati halifikiwi.

#### 4.3.9 Mkanganyiko kuhusu sheria ipi itumike kulipa mafao

Imeonekana kuwa uongozi wa baadhi ya taasisi umekuwa ukiomba idhini ya kulipa mafao ya uzeeni bila kuzingatia sheria za pensheni zifuatazo:

- Mafaili ya pensheni yamekuwa yanaandaliwa kwa kutumia mishahara waliyolipwa watumishi katika Mashirika ya kimataifa na ya Umma. Ilibainika wakati wa ukaguzi kuwa watumishi hawa walijiriwa Serikalini kwa mkataba katika nafasi yenye mishahara wa chini ikilinganishwa na waliokuwa wanalipwa katika mashirika hayo; idhini iliombwa ili wahusika walipwe mishahara waliyokuwa wanalipwa wakati wakiwa katika ajira za mashirika ya kimataifa na ya umma. Hii ni kinyume na Aya ya 47(a), (b) na (c) ya Kanuni za Kudumu na Kifungu cha 14 Sheria ya Pensheni kama ilivyorekebisha tarehe 20 Machi, 1978. Sheria tajwa zitatumika tu endapo ajira ya mtumishi ni ya masharti ya kudumu na pensheni.
- Pia, imeonekana kuwa baadhi ya maafisa walioacha kuwa viongozi wa kisiasa kwa namna ambayo sheria za pensheni zilizopo ziliruhusu wao kulipwa mafao lakini malipo yao hayakutayarishwa kwa wakati kwa madai

kuwa maafisa wahusika hawakuomba kulipwa mafao hayo.

Aidha, waajiri wao hawakushughulikia stahili zao za mafao kwa vile maafisa hawa waliendelea kuteuliwa katika nafasi ambazo mafao yake ya pensheni yanatawaliwa na sheria nyingine. Wakati maafisa hawa wanapostaafu katika ajira yao ya mwisho, huomba kibali cha kuunganisha muda wote wa ajira ili walipwe pensheni kwa sheria inayowapa manufaa zaidi kimapato. Kwa vyovyote vile, sheria haitoi mwanya kwa mstaafu kunufaika kwa kutumia sheria inayosimamia ajira yake ya mwisho katika mashirika ya kimataifa au taasisi nyingine.

#### **4.3.10 Kutokuwa na stahili ya kulipwa pensheni**

Watumishi wa ngazi ya chini Serikalini waliokuwa wameajiriwa chini ya masharti ya muda na baadae wakaingizwa katika masharti ya kudumu na pensheni, mafao yao ya uzeeni yalidikotolewa kama vile bado walikuwa chini ya masharti ya muda kinyume na sheria za pensheni ambazo zinataka kipindi alichotumikia mstaafu chini ya masharti ya muda kupata kibali cha Katibu Mkuu Hazina ili kihesabiwe katika masharti ya kudumu kwa madhumuni ya kulipa pensheni

#### **4.3.11 Kasoro katika kutayarisha malipo ya uzeeni**

Kwa ujumla, matatizo yaliyoelezwa hapo juu yamechangiwa zaidi na udhaifu wa watayarishaji majalada kwani baadhi yao walishindwa kufuata sheria za pensheni na miongozo. Ijapokuwa kasoro hizo zimeelezwa pia katika ripoti ya mwaka ulipoita, hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa.

## SURA YA 5

### MAMBO MUHIMU YALIYOJITOKEZA KATIKA UKAGUZI WA WIZARA, IDARA, WAKALA NA SEKRETARIETI ZA MIKOA

#### 5.1 Manunuzi yaliyofanywa bila kuwa kwenye mpango wa anunuzi wa mwaka

Kifungu cha 45 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 inazitaka Taasisi za ununuzi kuweka mpango wa mwaka wa manunuzi ili kuepuka manunuzi ya dharura na kupata thamani ya fedha, kupunguza gharama za matumizi na kupata manunuzi sahihi kwa njia ya kandarasi. Ukaguzi umebainisha kwamba katika mwaka wa fedha 2009/2010, Taasisi zilizoonyeshwa hapa chini zilifanya manunuzi yenye thamani ya Sh. 50,685,371,565.58 bia kufuata Kifungu cha sheria kilichotajwa hapo juu:

Na.	Fungu	Wizara/Idara/Wakala/Sekretarieti za Mikoa	Kiasi (Sh.)
1	23	Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali	49,433,343,399.58
2	99	Wizara ya Mifugo na uvuvi	320,871,938
3	81	Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza	54,424,314
4	50	Wizara ya Fedha	373,184,960
5	34	Wizara ya Mambo ya Nje na Uhusiano wa Kimataifa	212,897,447.23
6	91	Tume ya kudhibiti Madawa	40,748,400
7	29	Idara ya Magereza	358,394,154
8	82	Sekretarieti ya Mkoa wa Ruvuma	11,654,400
		<b>Jumla</b>	<b>50,685,371,565.58</b>

#### 5.2 Matengezezo ya magari katika karakana zisizoidhinishwa na TEMESA Shs.176,722,089

Wizara/Idara/Wakala/Sekretarieti za Mikoa zinatakiwa kutengeneza magari yake kupitia TEMESA au kupeleka katika karakana zilizoidhinishwa na TEMESA kuwa zinao utaalam unaotakiwa katika fani ya ufundi wa magari kwa



mujibu wa Kanuni ya 5 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma (Mali, kazi, huduma zisizo za ushauri na uuzaji wa mali ya umma kwa zabuni) ya mwaka 2005.

Katika ukaguzi wa mwaka huu, imebainika kuwa Wizara/Idara/Wakala/Sekretarieti za Mikoa zipatazo 5 zililipa jumla ya Sh. 176,722,089 katika karakana binafsi za magari ambazo hazijaidhinishwa na TEMESA kama gharama za matengenezo ya magari. Hakuna kibali kilichoombwa kutoka TEMESA kabla ya kupeleka magari katika karakana hizo.

Na.	Fungu	Wizara/Idara/Wakala/Sekretarieti za Mikoa	Kiasi (Sh.)
1	79	Sekretarieti ya Mkoa wa Morogoro	7, 887, 983
2	87	Sekretarieti ya Mkoa wa Kagera	3,464,678
3	98	Wizara ya Maendeleo ya Miundombinu	40,545,082.00
4	75	Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro	13,833,969
5	29	Idara ya Magereza	118,878,359.82
		<b>Jumla</b>	<b>176,722,089</b>

### 5.3 Malipo ya mishahara kwa wastaafu wasiokuwa kazini na maafisa wasio na stahili Sh.1,842,607,565.29

Ukaguzi wa orodha za malipo ya mishahara mwaka huu umeonyesha kuwa Wizara/Idara/Wakala/Sekretarieti za Mikoa zilizo rodheshwa hapa chini zililipa jumla ya Shs.1,842,607,565.29 kama mishahara kwa wastaafu, wasiokuwa kazini na wasiokuwa na stahili kwa vile hawakuwa tena kazini.

Na.	Fungu	Wizara/Idara/Wakala/Sekretarieti za Mikoa	Kiasi (Sh.)
1	31	Ofisi ya Makamu wa Rais	3,735,894.72
2	32	Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi nwa Umma	1,686,726,709.00
3	48	Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Mkakazi	26,020,151.77
4	52	Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii	83,768,896.00
5	69	Wizara ya Maliasili Na Utalii	10,052,511.80
6	85	Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora	6,315,000.00
7	87	Sekretarieti ya Mkoa wa Kagera	21,662,551.00
8	93	Idara ya Magereza	4,325,851.00
		<b>Total</b>	<b>1,842,607,565.29</b>

Jedwali hilo hapo juu linaonyesha kuwa bado kuna matatizo makubwa katika mifumo ya udhibiti wa ndani katika eneo hili la usimamizi wa mishahara.

#### 5.4 Ununuzi wa samani kwa maafisa wasiokuwa na stahili Sh.650,714,800.66

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma (UTUMISHI) ilitoa Waraka Na. C/CA/134/213/01/G/69 wa tarehe 30 Januari, 2006 unaohusu malipo ya posho ya nyumba na ununuzi wa samani kwa nyumba za Serikali kwa maafisa wenye stahili. Waraka huu ulirekebisha Nyaraka za nyuma na ulikusudia kuondoa mkanganyiko wa tafsiri uliokuwepo ambao ulisabababisha utekekezaji wake utofautiane katika Wizara na Taasisi mbalimbali za Umma na hivyo kusababisha malipo ya posho ya samani au samani kununuliwa kwa ajili ya nyumba binafsi badala ya zile za Serikali.

Waraka uliotajwa hapo juu unaeleza kuwa ni maafisa wanaoishi katika nyumba za Serikali tu ndio wenye stahili ya kununuliwa samani kwa ajili ya nyumba hizo. Aidha, samani hizo zitabakia kuwa mali ya Serikali hata pale maafisa hao watakapohama katika

nyumba hizo. Kwa wale maafisa wanaoishi katika nyumba zao na wana stahili kulipwa posho ya nyumba, Waraka unawapa stahili ya posho ya asilimia 30 ya mishahara yao kwa mwezi lakini hauelezi lolote kuhusu nyumba hizo binafsi kununuliwa samani.

Kinyume na matakwa ya Waraka huo wa UTUMISHI, Wzara, Mikoa na Taasisi zifuatazo zililipa jumla ya Sh. 650,714,800.66 kwa ajili ya ununuzi wa samani kwa maafisa wanaoishi katika nyumba binafsi na hivyo kusababisha matumizi yasiyokuwa na manufaa kwa Serikali.

Na.	Fungu	Wizara/Idara/Wakala/Sekretarieti za Mikoa	Kiasi (Sh.)
1	26	Ofisi ya Makamu wa Rais	90,207,007.00
2	32	Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi nwa Umma	111,163,427.00
3	43	Wzara ya Kilimo Chakula na Ushirika	29,685,000.00
4	46	Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi	86,563,593.00
5	53	Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto	55,895,840.00
6	58	Wizara ya Nishati na Madini	92,365,000.00
7	59	Tume ya Kurekebisha Sheria	13,695,000.00
8	68	Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia	18,830,539.00
9	69	Wizara ya Maliasili Na Utalii	119,373,094.66
10	96	Wizara ya Habari, Vijana na Michezo	32,936,299.00
		<b>Total</b>	<b>650,714,800.66</b>

**5.5 Malipo yenye nyaraka pungufu Sh.362,026,933,382.25**  
 Malipo ya jumla ya Sh.362,026,933,382.25 yalikuwa na nyaraka pungufu kinyume na Kanuni ya 95(4) ya Kanuni za Fedha za Umma ya 2001 (iliyorekebishwa 2004). Kwa hali hiyo, uhalali wa malipo hayo haukuweza kuthibitishwa.

Na.	Fungu	Wizara/Idara/Wakala/Sekretarieti za Mkoa	Matumizi ya Fungu kwa mwaka (Sh.)	a matumizi ya fungu	Nyaraka pungufu (Shs)
1	18	Mhakama Kuu ya Tanzania	15,014,131,026	5.5	825,240,000.00
2	19	Mahakama za Wilaya na Mwanzo	14,518,897,754	0.2	29,527,500.00
3	21	Hazina	279,993,233,165.09	0.05	150,611,256.00
4	22	Deni la Taifa na Matumizi mbalimbali	1,325,400,889,388	21.12	279,993,233,165.09
5	29	Idara ya Magereza	97,127,525,644	0.08	80,559,598.00
6	32	Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi nwa Umma	42,219,435,856	19.07	8,052,888,683.00
7	40	Mahakama	17,754,949,678	2.05	363,966,918.60
8	42	Ofisi ya Spika	69,044,710,084.36	0.07	48,539,438.00
9	46	Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi	501,586,424,372	0.07	342,039,444.00
10	50	Wizara ya Fedha	219,008,886,868.11	31.96	70,000,000,000
11	52	Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii	480,316,736,838.48	0.12	597,967,673
12	69	Wizara ya Maliasili Na Utalii	47,310,103,630	0.35	165,448,602.00
13	82	Sekretarieti ya Mkoa wa Ruvuma	81,389,666,900	0.04	34,627,787.00
14	85	Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora	5,607,717,181	2.13	119,742,418
16	92	Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania	14,466,757,157	7.22	1,044,265,701
17	94	Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma	9,437,247,483.26	1.00	94,712,958
18	95	Sekretarieti ya Mkoa wa Manyara	69,697,097,548	0.12	83,562,240.56
		<b>Total</b>			<b>362,026,933,382.25</b>

## 5.6 Mali na vifaa visivyopokelewa Sh.13,865,874,762

Mali na vifaa vyenye thamani ya jumla ya Sh. 13,865,874,762 vililipiwa lakini havikupokelewa au vilipokelewa pungufu kwenye Wizara/Idara na Wakala kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapa chini. Hali hii ni kinyume na Kanuni ya 122 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma (Mali, kazi, huduma zisizo za ushauri na uuzaji wa mali ya umma kwa zabuni) ya mwaka 2005.

Na.	Fungu	Wizara/Idara/Wakala/Sekre tarieti za Mikoa	Kiasi (Sh.)
1	29	Idara ya Magereza	295,463,511.00
2	40	Mahakama	204,833,667.00
3	48	Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Mkakazi	126,835,900.00
4	52	Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii	1,648,407,271.00
5	56	Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa	4,886,045,280.00
6	56	Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa	611,104,553.00
7	75	Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro	329,877,640.00
8	78	Sekretarieti ya Mkoa Mbeya	208,439,409.00
9	89	Sekretarieti ya Mkoa wa Rukwa	19,728,778.00
10	98	Wizara ya Maendeleo ya Miundombinu	5,830,602,264.00
		Total	13,865,874,762.00

## 5.7 Malipo yaliyofanyika kutoka katika vifungu visivyohusika Sh.5,296,243,598

Katika mwaka 2009/2010, ukaguzi wa majaribio ulibaini kuwa baadhi ya Wizara/Idara/Wakala/Sekretarieti za Mikoa na Balozzi hazikuzingatia bajeti ya Mpango wa Kati wa Matumizi ya Fedha za Umma (MTEF) na hivyo kufanya malipo ya kiasi cha Shs. 5,296,243,598 kutoka katika vifungu vingine ambavyo

havikukasimiwa matumizi hayo bila kibali cha Hazina kinyume na Kanuni ya 51(1-8) ya Kanuni za Fedha za Umma za 2001 (zilizorekebishwa 2004).

Na.	Fungu	Wizara/Idara/Wakala/Sekretarieti za Mikoa	Kiasi (Sh.)
1	39	Jeshi la Kujenga Taifa	309,972,400.00
2	44	Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko	263,963,996.00
3	46	Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi	362,445,738.00
4	52	Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii	3,894,809,822.00
5	56	Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa	30,313,727.00
6	61	Tume ya Uchaguzi ya Taifa	262,025,808.00
7	75	Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro	12,471,000.00
8	86	Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga	80,991,107.00
9	94	Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma	79,250,000.00
		<b>TOTAL</b>	<b>5,296,243,598.00</b>

#### 5.8 Malipo yenye shaka Sh.15,711,104,612

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara, Idara, Sekretarieti za Mikoa mitatu zilifanya malipo yenye shaka yanayofikia Sh. 15,711,104,612. Malipo hayo yalionekana kukosa viambatanisho ambavyo vingenyeshataarifa za kina pasipo kuacha mashaka yoyote kuhusiana na usahihi wa malipo hayo.

Mchanganuo wa malipo yenye shaka ni huu ufuatao:

Na.	Fungu	Wizara/Idara/ Wakala/Sekre tarieti za Mikoa	Kiasi (Sh.)
1.	Mahakama	40	267,658,188
2.	Wizara ya Fedha	50	15,415,146,424
3	Sekretarieti ya Mkoa wa Manyara	95	28,300,000
	<b>Jumla</b>		<b>15,711,104,612</b>

Muhtasari wa malipo yenye shaka kwa mwaka 2007/2008 na 2008/2009 upo kwenye jedwali lifuatalo kwa ajili ya ulinganisho:-

Mwaka	Kiasi (Sh)	Wizara, Idara, Sekretarieti za Mikoa
2008/2009	2,130,565,329	9
2009/2010	15,711,104,612	3

**5.9 Kukosekana kwa orodha ya waliolipwa kiasi cha Sh.48,000,270,000 kwa ajili ya kuchochea ukuaji wa uchumi**

Serikali ililipa kiasi cha Sh. 48,000,270,000 katika Benki Kuu ya Tanzania kama sehemu ya mchango wake wa kuchochea ukuaji wa uchumi ili kukabiliana na msukosuko wa uchumi ulioikumba dunia. Hata hivyo, hatukupatiwa orodha ya walionufaika na fedha hizo za kufidia hasara na kulipia mikopo wala utaratibu utakaotumika kwa wafanyabiashara husika kurejesha fedha hizo pindi hali ya uchumi itakapoimarika. Kwa hali hiyo, nimeshindwa kujiridhisha kuhusu uhalali wa malipo hayo na urejeshwaji wake utakavyokuwa.

## 5.10 Ukaguzi wa Usimamizi wa Manunuzi

### 5.10.1 Utangulizi

Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) iliwasilisha taarifa ya mwenendo wa manunuzi katika Taasisi mbalimbali ambayo imeonyesha kwa kiwango kikubwa mapungufu yaliyojitokeza katika taarifa ya mwaka uliopita. Kwa kutambua kazi nzuri iliyofanywa na Mamlaka hii, nimeamua kujumuisha masuala yaliyobainishwa na Mamlaka hii kwenye taarifa yangu.

Lengo la ukaguzi uliofanywa na PPRA ni kubaini kiwango cha uzingativu wa Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004; Kanuni zake za 2005 na Tangazo la Serikali Na. 177 la 2007 na kwamba manunuzi yaliyofanywa yanawakilisha thamani halisi ya fedha zilizotumiwa na taasisi husika. Muhtasari wa matokeo na mapungufu yaliyojitokeza ni kama ifuatavyo:

### 5.10.2 Utendaji wa Taasisi za Ununuzi (Procuring Entities - PEs)

Pamekuwepo na ongezeko kidogo la utoaji taarifa za zabuni/kandarasi zilizotolewa na Taasisi za Ununuzi kutoka asilimia 59% mwaka jana hadi 65% mwaka 2009/2010. Hata hivyo, kiwango kilichofikiwa hakitoshi kwani lengo lilikuwa ni kwa Taasisi zote za Ununuzi kuzingatia kikamilifu matakwa ya kutoa taarifa sahihi zihusuzo zabuni/kandarasi ilizotoa, kwani takwimu hizo zinaweza kuzisaidia taasisi hizo na Serikali kujua mwelekeo na hivyo kupanga mipango yake kwa msingi wa taarifa zilizopo.

Kutokana na uchambuzi uliofanywa kwa Taasisi 226 zilizowasilisha taarifa ya bajeti zake za manunuzi PPRA, pamoja kiasi cha manunuzi kichofanywa, ni dhahiri kuwa kwa sasa matumizi yatokanayo na manunuzi ni asilimia 52 ya matumizi yote ya Serikali. Japokuwa kiasi hiki kiko chini ya kile cha asilimia 70 kilichochoeleka, bado inaonyesha kuwa kiasi kikubwa cha fedha za Umma kinatumika katika manunuzi.



### 5.10.3 Matokeo ya Ukaguzi wa Manunuzi

Matokeo ya ukaguzi uliofanywa na PPRA umeonyesha wastani wa kiwango cha uzingatifu cha asilimia 55 kilichokokotolewa kutokana na viashiria 13 vya uzingatifu. Kiwango cha wastani cha uzingatifu wa viashiria hivyo kwa Wizara, Idara, Wakala, Mashirika ya Umma na Mamlaka ya Serikali za Mitaa ilikuwa 57%, 59% na 50%.

Kwa upande mmoja, hali ya utendaji wa Taasisi zote za Manunuzi ulikuwa chini ya wastani (chini ya 50%) katika viashiria vitano ambavyo ni: Kuundwa kwa Vitengo vya manunuzi na mchanganyiko wa watumishi wake kitaaluma; Kutayarishwa mpango wa mwaka wa manunuzi; Utunzaji kumbukumbu na uahakika wa udhibiti wa ubora. Kwa upande mwingine, utendaji wa Taasisi za manunuzi ulikuwa juu ya wastani (50% na zaidi) katika viashiria 8 vifuatavyo: Kuundwa kwa Bodi za manunuzi na mchanganyiko wa wajumbe wake; Utendaji wa Maafisa Wahasibu, Bodi za Manunuzi na Vitengo vya Manunuzi; Kuzingatia viwango vilivyoidhinishwa; Kutangaza zabuni; Kutumia njia sahihi za manunuzi; Kuzingatia matumizi ya nyaraka kubalifu za zabuni kama zilivyoielezwa katika kanuni na utekelezaji wa mkataba.

Mchanganuo kuhusu hali ya ujumla ya uzingatifu wa sheria na kanuni za manunuzi umeonyeshwa katika **Kiambatisho Na. III**

PPRA ina lengo la kuhakikisha kuwa wastani wa uzingatifu wa sheria na kanuni za manunuzi kwa Tasisi za Ununuzi unafikia asilimia 80 hadi kufikia mwisho wa mwaka 2010/2011. Kwa sababu ya uhaba wa fedha na nyenzo, kipaumbele kitapewa maeneo ambayo yataleta matokeo ya kuridhisha katika kujenga uwezo wa Taasisi za Manunuzi kuzingatia Sheia ya Manunuzi ya Umma ya 2004, Sura ya 410 na Kanuni zake za 2005. Kutokana na ripoti ya PPRA, umuhimu utaelekezwa katika maeneo yafuatayo:

**(a) Kuundwa kwa Vitengo vya Manunuzi na kuvipa watumishi**

Kuundwa kwa Vitengo vya manunuzi na kuvipa watumishi wenye sifa stahiki ni tatizo linalozikabili Taasisi za Manunuzi. Kaguzi zilizofanywa na PPRA zilibaini kuwa wastani wa kiwango cha uzingatifu katika kuunda Vitengo vya manunuzi na kuvipa watumishi wenye sifa stahiki kilikuwa 43%. Wastani wa uzingatifu katika eneo hili kwa upande wa Wizara, Idara, Wakala, Mashirika ya Umma na Mamlaka ya Serikali za Mitaa ilikuwa 44%, 49% na 38%. Kwa upande wa Serikali Kuu, tatizo linatokana na udhaifu katika Sheria ya Manunuzi ambayo haisemi lolote kuhusu anakotakiwa kuwajibika Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi katika Taasisi za Manunuzi na wakati mwingine, baadhi ya vitengo vya Manunuzi viliundwa kama Kamati za Bodi ya Zabuni

**(b) Utayarishaji wa mipango ya mwaka ya manunuzi**

Mapitio ya utayarishaji wa mipango ya manunuzi ya mwaka unaonyesha kwa wastani uzingatifu wa asilimia 46%, kwa Wizara, Idara na Wakala; asilimia 47 kwa Mashirika ya Umma na asilimia 30 kwa Halmashauri.

Mapungufu dhahiri yaliyobainika kuhusu mipango ya manunuzi ya mwaka na utekelezaji wa mipango hiyo yanajumuisha:

- Fomu zilizoidhinishwa kwa ajili ya kutumika hazikufuatwa. Muda wa kushughulikia hatua mbalimbali za manunuzi haukuonyeshwa.
- Mahitaji kwa kila idara hayakujumuishwa
- Manunuzi yaliyoonyeshwa kwenye makisio hayajajumuishwa kwenye mpango wa mwaka wa manunuzi.
- Vikao vingi vya Bodi za Zabuni
- Utumiaji mwingi wa utaratibu wa dodoso za bei katika manunuzi yenye thamani ndogo ndogo.
- Mipango ya manunuzi isiyo halisi

**(c) Usimamizi wa Mikataba**

Katika kutathimini usimamizi wa mikataba, mambo yaliyozingatiwa ni kama ifuatavyo:

- Baadhi ya mikataba haikuwa imesainiwa
- Baadhi ya mikataba ilikosa nyaraka muhimu kama vile masharti ya mkataba, michoro, maelezo ya kina ya jinsi ya kutekeleza mkataba; mikataba mingine ilikuwa na nyaraka zisizohusiana na mkataba kama vile tangazo la zabuni/dodoso la bei na maelezo kwa waomba zabuni
- Kutotumia kifungu cha fidia kwa kuchelewa kutekeleza mikataba
- Kutokuwa na vikao katika eneo la mradi kutathmini uekelezaji wa miradi.
- Kutokuwepo mipango ya kudhibiti na kutoa hakikisho la ubora katika utekelezaji wa mikataba; kazi zilizokamilika hazikufanyiwa tathmini kuona kama zimekidhi matakwā ya utekelezaji aliyopewa mkandarasi katika mkataba
- Taarifa za utekelezaji hazikuandaliwa
- Taarifa za wasimamizi wa mikataba hazikutayarishwa
- Muda wa utekelezaji mikataba kuongezwa bila kufuata taratibu
- Malipo kufanywa kwa kazi ambayo haijafanyika kwa kuzidisha kiwango cha kazi iliyokamilika
- Kutokuteuliwa kwa Kamati za mapokezi na ukaguzi wa mali zilizonunuliwa kuthibitisha usahihi, ubora na idadi.
- Kutokuwepo kwa udhibiti wa ubora na usimamizi mbaya wa mikataba kilikosababishwa na ufinyu wa rasilimali (watu, fedha, magari, zana za kudhibiti ubora n.k.)
- Kukosekana miongozo katika uendeshaji wa miradi ya kijamii

**(d) Utunzaji wa nyaraka**

Tathmini iliyofanywa ilibaini kuwepo mapungufu makubwa kwenye orodha ya wazabuni, dodoso za bei, mikataba, nyaraka za manunuzi kutowekwa sehemu moja, upungufu katika usimamizi wa nyaraka na mikataba, upungufu wa

sehemu za kutunzia nyaraka pamoja na ukosefu wa taratibu za kutunza mafaili. Matatizo haya yalisabisha wakaguzi kutopata uhakika kamili kuhusu zabuni zilizotangazwa na muda mwingi ulitumika kwa vile nyaraka hazikutunzwa sehemu moja.

**(e) Ufisadi katika Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe**

Ilithibitika wakati wa ukaguzi kuwa mkandarasi alilipwa kiasi kikubwa cha fedha kwa kazi ambazo hazikufanyika. Uchunguzi wa haraka uliofanywa na PPRA ulibaini kuwa mkandarasi alilipwa kiasi cha Sh. 40,120,000 isivyostahili kwa ajili ujenzi wa barabara. Aidha, mabadiliko ya gharama yalitolewa (bila maandishi) yakilenga kupunguza ukubwa wa kazi (kutoka makalvati yenye vipimo vya kipenyo cha 3.0m x 1.5m x 6m hadi 0.7m) kwenda kipenyo cha 0.7m katika eneo la barabara ya Nyakahanga - Nyabiyonza. Mkandarasi alilipwa malipo yote bila kuzingatia kiasi cha kazi kilichopungua.

**(f) Tathmini ya ufanisi wa Taasisi za Manunuzi katika kushughulikia zabuni**

Tathmini imeonyesha kuwa wastani wa siku zinazotumiwa na Taasisi za Manunuzi (PEs) kushughulikia zabuni (kuanzia ufunguzi wa zabuni hadi kutoa zabuni kwa mshindi) ni siku 42. Muda huu ni zaidi ya ule uliopendekezwa katika Jedwali la tatu la Gazeti la Serikali Na. 97 la 2005 ambapo ni siku 12. Kutokuwepo kwa ufanisi katika mchakato wa kushughulikia zabuni kunasababishwa na Taasisi za manunuzi kutokuwa na mpango wa mwaka wa manunuzi.

**(g) Miradi ya Kijamii**

Ukaguzi wa PPRA umeonyesha kuwa wafadhili wa maendeleo hupeleka fedha nyingi katika miradi ya kijamii. Miradi hii ni pamoja na MMEM (Mpango wa Maendeleo Elimu ya Msingi); MMES (Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari); PADEP (Participatory Agriculture Development

and Empowerment Programme); DASIP (District Agricultural Sector Investments Programme) na Mfuko mwa Maendeleo ya Jamii (TASAF). Hata hivyo, kasoro nyinngi zimeonekana katika utekelezaji wa miradi hii kutokana na kutokuwepo miongozo ya manunuzi iliyorahisishwa kwa ajili miradi ya kijamii. Kwa hali hiyo, inapendekezwa kuwa PPRA iharakishe kutayarisha na kusambaza miongozo ya manunuzi kwa ajili ya miradi ya kijamii.

**(h) Ununuzi wa zana za kufundishia**

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi iliwaidhinisha wazabuni watatu kusambaza zana za kufundishia katika Halmashauri zote nchini. Hii imesababisha manunuzi kuchelewa kufanyika na hivyo kuongezeka kwa gharama za zana hizo kwani hakuna ushindani. Zaidi ya hapo, utaratibu huu hautoi nafasi sawa kwa wauzaji wengine wenye uwezo wa kutoa huduma hiyo kwa maelezo kuwa hawajaidhinishwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Kwa hali hiyo, inapendekezwa kuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi iongeze orodha ya wazabuni walioidhinishwa ili pawepo ushindani, ufanisi na ubora wa mali.

**5.11 Taarifa ya Mhakikimali wa Serikali kuhusu usimamizi wa vifaa**

Sehemu ya XV ya kanuni za Fedha za Umma inashughulika na matakwa ya kuwepo uhakikimali huru wa vifaa vya Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mkoa. Kwa hali hiyo, nimepokea taarifa ya uhakiki mali kwa mujibu wa Kanuni ya 245 (3) ya Kanuni ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (ilivyorekebishwa 2004). Kutokana na Kanuni hiyo, Mhakiki Mali wa Serikali anatakiwa kubaki na nakala moja ya taarifa niyo kwa ajili ya kumbukumbu zake na kupeleka nakala moja kwa Afisa Masuuli mhusika, Katibu Mkuu Hazina, Mhasibu Mkuu wa Serikali na Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali.

Kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni iliyotajwa hapo juu, kitengo cha Uhakiki Mali chini ya Wizara ya Fedha na Uchumi, kilifanya uhakikimali wa kina katika wizara/Idara na Wakala 17 na Sekretariati za Mikoa 9 kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2009.

Nimeridhika na kazi iliyofanywa na kitengo hiki na nimeona kuwa taarifa walizotoa ni za manufaa na zenye mambo muhimu ya kuingiza katika taarifa yangu.

Katika mwaka husika, pamekuwepo na udhaifu mkubwa katika usimamizi wa vifaa kama ilivyoelezwa katika Kiambatanisho IV.



## SURA YA 6

### UCHAMBUZI WA HESABU JUMUIFU ZA TAIFA

#### 6.1 Utangulizi

Hesabu Jumuiifu za Taifa ni muhtasari wa utendaji na uchangiaji unaolenga kuonyesha uwazi na uwajibikaji katika Serikali. Kwa madhumuni ya ripoti hii, taarifa jumuiifu zinamaanisha taarifa zifuatazo:

- Taarifa ya Mapato na Malipo
- Taarifa ya ulinganisho wa makisio na kiasi halisi kilicholipwa
- Taarifa ya Mtiririko wa fedha
- Taarifa ya malipo kwa aina ya kazi
- Vielekezi katika taarifa ya fedha

Hesabu Jumuiifu za Taifa pamoja na viambatanisho huwezesha wasomaji kufanya uchambuzi na kutathmini utendaji wa Serikali wa mwaka na msimamo wa Serikali katika kipindi cha mwaka wa ukaguzi husika.

#### 6.2 Masuala ya miaka iliyopita yasiyojibiwa

Hadi kufikia wakati wa kutoa taarifa yangu kwa Hesabu Jumuiifu za Taifa, kulikuwa na masuala mbalimbali ya ukaguzi yaliyoripotiwa katika taarifa zilizopita kama yalivyoainishwa hapa chini ambayo hayakuwa yameshughulikiwa

- **Makusanyo ya kodi ambayo bado hayajapokelewa**  
Sh.52,422,025,182

Uongozi ulitakiwa kuthibitisha mapokezi ya uhamisho wa fedha kiasi cha sh.52,422,025,182 kwenda kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali. Hadi tarehe ya taarifa hii, hati na nyaraka za kuhamisha kiasi cha Sh. 45,644,726,077



zimepatikana na kuhakikiwa bado nyaraka za kiasi cha Sh.6,777,299,114 kuthibitisha mapokezi ya fedha hizo kwenye akaunti ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)

- **Matumizi yaliyofanyika zaidi ya makisio Sh.67,412,110,917**  
Uongozi ulitakiwa kutoa maelezo ya kina kuhusu matumizi zaidi ya makisio yaliyopitishwa. Kiasi cha Sh.65,826,781,829 kimehakikiwa na marekebisho kufanyika katika mafungu mabalimbali isipokuwa kiasi cha Sh.1,585,329,088 za mafungu 74,79, na 93 bado kutolewa maelezo.
- **Tofauti katika Hesabu Jumuifu za Taifa ya Sh.2,194,266,087**  
Uongozi ulitakiwa kufanya usuluhisho na kuondoa dosari/tofauti katika Hesabu Jumuifu za Taifa ili zionyeshe bakaa halisi kataka vitabu.

Marekebisho ya kiasi cha Sh.109,859,615.62 katika mafungu yafuatayo 32, 38,56, 99,43, 46,71 na 88 hayakuwasilishwa ukaguzi.

### 6.3 Matokeo ya ukaguzi ya mwaka kuhusu Hesabu Jumuifu za Taifa

Yafuatayo ni masuala muhimu yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi wa Utendaji kifedha wa Hesabu Jumuifu za Taifa

#### 6.3.1 Jumla ya matumizi ya Serikali Sh. 8,522,395,969,190

Jedwali hapa chini linaonyesa mtiririko wa fedha za matumizi ya kawaida na ya maendeleo katika Hesabu Jumuifu za Taifa kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali na Serikali za Mitaa kwa miaka 2008/09 na 2009/10.

Matumizi ya kawaida yameongezeka kutoka Sh.4,929,614,519,420 mwaka 2008-09 hadi kufikia

Sh.6,237,494,869,945 mwaka 2009-10 sawa na asilimia 27, wakati matumizi ya maendeleo yameongezeka kutoka Sh.1,606,484,993,991 mwaka 2008-09 hadi kufikia Sh.2,284,901,099,246 kwa mwaka 2009-10 ikiwa ni sawa na asilimia 42.

Akaunti ya matumizi	2008/09 (Sh)	%	2009/10 (Sh)	%
Kawaida	4,929,614,519,420	75	6,237,494,869,945	73
Maendeleo	1,606,484,993,991	25	2,284,901,099,246	27
Jumla	6,536,099,513,411	100	8,522,395,969,190	100

Kwa ujumla, fungu la kawaida lilitumia asilimia 73 ya fedha zote wakati fungu la maendeleo lilitumia asilimia 27 tu.

### 6.3.2 Makusanyo ya maduhuli

Taarifa Jumuifu ya mapato iliyoishia tarehe 30 Juni, 2010 inaonyesha makusanyo halisi ya Sh. 7,928,122,248,611 ikilinganisha na makadirio ya Sh. 10,063,686,670,897 hivyo kuonyesha upungufu wa makusanyo ya Sh. 2,135,564,422,286 sawa na asilimia 21.22 ya makisio yaliyoidhinishwa na bunge. Upungufu wa makusanyo ni dalili za awali zinazoashiria hali mbaya hivyo Serikali inatakiwa kutathimini mwenendo mzima wa maduhuli ili kuboresha makusanyo.

Mtiririko wa makusanyo ya maduhuli kwa muda wa miaka mitatu ya nyuma ni kama inavyoonekana hapa chini:

Miaka	2007/2008 (Sh)	2008/2009 (Sh)	2009/2010 (Sh)
Makisio	6,160,992,762,345	7,704,909,780,498	10,063,686,670,897
Makusanyo halisi	5,305,427,340,743	6,427,630,892,809	7,928,122,248,611
Upungufu	855,565,421,602	1,277,278,887,689	2,135,564,422,286

Makusanyo katika fungu la kawaida yanatokana na kodi mbalimabali, makusanyo yasiyo ya kodi na makusanyo kutokana na raslimali za serekali ambapo katika fungu la maendeleo maduhuli yanatokana na mikopo ya nje, misaada ya wafadhili, mikopo isiyokuwa na riba na mikopo ya ndani ya nchi.

### 6.3.3 Misaada kutoka nje ya nchi Sh. 2,393,256,357,651

Taarifa ya misaada kutoka nje ya nchi inaonyesha kiasi cha Sh.3,932,474,455,117 ikiwa ni makadirio ya misaada iliyotarajiwa kupokelewa kutoka vyanzo mbalimbali nje ya nchi kwa mwaka wa fedha 2009-10.

Hata hivyo, kiasi halisi kilichopokelewa ni Sh.2,393,256,357,651 ikiwa ni sawa na asilimia 61 ya makisio yote. Hii inaonyesha kwamba mashariti ya misaada hayakuzingatiwa au misaada hiyo haikuletwa na wahisani.

Misaada yote iliyoletwa na kupokelewa ni kama ifuatavyo:

	Madhumuni	Kiasi (Shs.)
1	Mfuko Mkuu wa kuchangia bajeti	1,212,101,028,546
2	Mfuko wa wachangiaji	600,564,470,177
3	Fedha za miradi ya maendeleo	580,590,858,927
	Jumla	2,393,256,357,650

Kwa mtazamo huo hapo juu, Serikali inatakiwa kufanya jitihada kuongeza makusanyo ya mapato ya ndani ya nchi ili kuondokana na utegemezi wa misaada toka nje.

### 6.3.4 Taarifa ya mapato yasiyokusanywa

Taarifa Jumuiifu ya Hesabu za Serikali imeonyesha maduhuli yasiyokusanywa yameongezeka kutoka Sh. 10,020,246,900 kwa mwaka 2008/2009 hadi kufikia Sh. 116,320,437,345 kwa mwaka 2009/2010 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 1,060. Hii inaonyesha kuwa kulikuwa na udhaifu

katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali katika mwaka wa fedha 2009/2010

### 6.3.5 Kuongezeka kwa Deni la Taifa Sh. 10,503,806,011,884.90

Taarifa ya Deni la Taifa kama lilivyoonyeshwa katika Hesabu Jumuifu za Taifa kwa kipindi kilichoishia 30 Juni, 2010 limeongezeka kwa asilimia 38 kutoka kiasi cha Sh. 7,621,286,730,033.80 katika mwaka wa fedha 2008/09 hadi Sh. 10,503,806,011,884.90 katika mwaka wa fedha 2009/10 kama inavyoonyeshwa katika jedwali hapa chini:

Maelezo	2007/08 Sh.	2008/09 Sh.	2009/10 Sh.
Deni la nje	4,601,657,485,229	5,386,646,362,543	7,747,903,803,161
Deni la ndani	1,875,794,357,188	2,234,640,367,491	2,755,902,208,703
<b>Jumla</b>	<b>6,477,451,842,417</b>	<b>7,621,286,730,034</b>	<b>10,503,806,011,885</b>

Jedwali hapo juu, linaonyesha ongezeko la deni la ndani kwa kiasi cha Sh. 43,373,690,323 na Shs.358,846,010,303 sawa na asilimia 2 na 19 kwa miaka 2007/2008 na 2008/09. Na baadae sh. 521,261,841,212 kwa mwaka 2009/10 ikiwa ni sawa na asilimia 23.

Kwa upande mwingine, deni la nje limeongezeka kwa Sh.2,361,257,440,618 sawa na ongezeko la asilimia 44 ikilinganishwa na kiasi kilichotolewa taarifa mwaka uliopita. Kwa ujumla, kuna ongezeko la deni la Taifa la kiasi cha Sh.2,882,519,281,851 ikiwa ni asilimia 39 katika mwaka 2009/2010 ikilinganishwa na mwaka 2008/2009. Kinyume na hivyo uchumi wa taifa umekuwa kwa asilimia 6.5 tu kutoka mwaka 2008/09 hadi 2009/10.

Kwa kutumia asilimia inaonyesha kuwa deni la ndani limeongezeka kidogo ukilinganisha na lile deni la nje, lakini

kwa ujumla wake utaona kuwa Serikali ilikopa kiasi kikubwa cha fedha kutoka katika taasisi mbalimbali za nje kuliko kiasi kilichokopwa katika taasisi za ndani ya nchi. Hii inamaanisha kuwa Serikali ina dhima kubwa katika kuwalipa wadai wa nje kuliko wadai wa ndani, na hii kiuchumi ina maana kuwa kiasi kikubwa cha mtaji katika fedha za kigeni kitalipwa nje ya nchi.

#### **6.3.6 Mihadi isiyoshughulikiwa Sh. 93,860,806,990**

Taarifa Jumuifu inaonyesha mihadi isiyoshughulikiwa kufikia Sh. 93,860,806,990 hadi ilipofika tarehe 30 Juni, 2010 ikiwa ni pungufu ya Sh. 275,883,320,206 au asilimia 75 ikilinganisha na ile ya mwaka 2008/09 ya kiasi cha Sh. 369,744,135,196.

Inabidi Serikali iwe na tahadhari kubwa katika kujiingiza katika mihadi ambapo hakuna fedha za kugharamia matumizi hayo. Hali kadhalika, pale Serikali inapokuwa na bakaa ya fedha ambazo hazina mihadi ni vyema zikarudishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Pia, ninapendekezo kuwa Mlipaji Mkuu wa Serikali atoe Waraka kwa Maafisa Masuuli wote akiwataka kutayarisha Mchanganuo wa Fedha zilizotumika katika kulipia mihadi iliyowekwa. Hii itasaidia kufuatilia kwa karibu endapo fedha zilizotengwa kwa ajili ya mihadi zimetumika kama ilivyokusudiwa.

Vilevile, kuhakikisha kuwa madai yote ambayo Serikali inadaiwa na yamekuwapo kwa muda wa miaka mitano au zaidi, basi ni lazima yawe yamehamishiwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali kulingana na Kanuni ya 133(1) ya Kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2001 (zilizorekebishwa 2004) inavyoelekeza.

**6.3.7 Taarifa ya Mikopo iliyotolewa na Serikali Sh. 424,087,766,124**

Taarifa Jumuiifu ya mikopo isiyorejeshwa inaonyesha kufikia Sh. 424,087,766,124 hadi ilipofikia tarehe 30 Juni, 2010 ikiwa ni sawa na ongezeko la Sh. 7,624,537,979 au asilimia 2 ikilinganishwa na salio la Sh 416,463,228,145 mwaka 2008/09.

Hata hivyo, mapitio ya taarifa ya madeni yasiyolipwa imebaini kwamba madeni yamekaa bila kulipwa kwa muda wa zaidi ya miaka mitatu. Zaidi ya hayo, taarifa ya Msajili wa Hazina inaonyesha kwamba Serikali imeshindwa kuokoa kiasi cha Sh. 281,864,968 kutoka kwa Ginaac Industries Ltd na kiasi cha Sh.44,062,788 kutoka kwa Mansoons Ltd kwani kampuni hizi hazipo na hakuna uhakika wa kuwepo rehani kama dhamana ya mikopo hiyo. Kwa mantiki hiyo, Serikali haiwezi kukusanya mikopo hiyo (Kiambatanisho V).

**6.3.8 Taarifa ya Madeni Yasiyotarajiwa Sh. 26,276,785,317**

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2010, Serikali ilikuwa na madeni yasiyotarajiwa yaliyohusisha Wizara tisa na Mikoa mitatu kama inavyoonekana hapa chini:-

S/n	Jina la wizara/mkoa	Kiasi (Sh.)
1	Wizara ya Afya na Usitawi wa Jamii	802,000,000
2	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo Na Uvuvi	970,309,970
3	Wizara ya Maliasili na Utalii	1,608,732,000
4	Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika	2,329,656,164
5	Wizara ya Elimu	282,543,545
6	Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana	1,026,246,335
7	Mkoa wa Lindi	169,700,000
8	Mkoa wa Dodoma	97,945,379
8	Ofisi ya Wairi Mkuu	259,554,088
10	Wizara ya Miundo Mbinu	16,209,047,878
11	Mkoa wa Rukwa	28,879,926
12	Wizara ya Maji na Umwagiliaji	2,492,170,032
	<b>Jumla</b>	<b>26,276,785,317</b>

Hata hivyo, chanzo cha madeni haya hakikuonyeshwa.

Madeni yasiyotarajiwa kama haya ni mzigo mkubwa kwa Serikali hasa pale yanapoiva na kutakiwa kulipwa, hivyo ningependa kuishauri Serikali kujiepusha katika kufanya maamuzi ambayo yatasababisha kushamiri kwa madeni yasiyotarajiwa.

**6.3.9 Taarifa ya Udhamini wa Serikali Sh. 711,804,989,096  
(i) Utoaji wa dhamana zaidi ya kiwango**

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2010 Serikali ilikuwa na madeni yaliyoingwiwa kwa njia ya Udhamini wa Serikali yanayofikia Sh. 711,804,989,096. Haikuweza kufahamika ni kwa jinsi gani Serikali ilikuwa ikidhamini zaidi ya kiwango kinachotakiwa kama inavyoelekezwa katika Kifungu Na. 13 (1)(b) cha Sheria ya Mikopo ya Serikali, Misaada na Udhamini ya Mwaka 1974 kama ilivyorekebishwa mwaka 2004 kinasema hivi:

“.....Kiwango cha juu kabisa ambacho Serikali inaweza kudhamini deni hakitazidi asilimia 70 ya fedha ziliyokopwa.....”

Ukaguzi ulibaini kwamba dhamana hizo hazikuwa na rehani halisi, hii inaweza kusababisha Serikali kujiweka hatarini kwa kuwa na dhamana ya kiasi kikubwa cha mikopo.

Kwa wastani, Serikali ilikuwa na dhamana ya asilimia 96.8 ya mikopo yote

**(ii) Tofauti ya dhamana katika Taarifa Jumuiifu Shs.3.94 bilioni**

Ulinganisho uliofanywa kati ya kiasi kilichoonyeshwa na Msajili wa Hazina cha Sh. 451,927,787,912 na kile kiasi kilichoonyeshwa na Hesabu za Taifa cha Sh. 447,987,521,547 imebainika kuwa na tofauti ya Sh. 3,940,266,366. Tofauti kati ya taarifa hizi mbili inahitaji kufanyiwa usuluhisho.

#### **6.3.10 Mfuko wa kubadilisha Madeni na Benki Kuu Sh. 2.099 bilioni**

Taarifa ya fedha Iliyochapishwa ya Benki Kuu ya Tanzania imeonyesha madeni yanayo fikia kiasi cha Sh.2.009 bilioni. Kwa mujibu wa benki kuu ni madeni yaliyozuiliwa katika akaunti yakisubiri kuwasilishwa kwa ripoti ya utekelezaji katika matumizi ya fedha ya miaka iliyopita, ili kuhlalisha utoaji wa fedha nyingine zaidi. Bakaa katika akaunti imebakia kwa muda mrefu. Hakuna juhudi za Serikali katika kuthibitisha kama bado kuna madai halali dhidi ya bakaa hii. Kuna uwezekano wa fedha hizi kupotea bila kujua.

#### **6.3.11 Amana na malipo ya Serikali ambayo hayakuonyeshwa katika taarifa ya fedha**

Taarifa ya fedha ya Benki Kuu ya Tanzania kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2010 haikuonyesha masuala kadhaa kuhusu amana za Serikali katika benki kama yanavyoelezwa hapa chini:

i) **Riba ya mkopo wa Serikali ya Sh. 266,800,000**  
Hesabu Jumuifu za Taifa zilionesha jumla ya Sh. 3,456.6 milioni kama mikopo ya muda mfupi ya Serikali kwa mwaka 2009/10 na kati ya mikopo hiyo, kiasi cha sh. 3,189.8 milioni kilikuwa kimelipwa na kubaki bakaa ya Sh. 266,800,000 hadi tarehe 30 Juni, 2010.

ii) **Malipo ya Uwezeshaji Uchumi Sh. 21,630,000,000**  
Jumla ya Sh. 21,630 milioni zimeonyeshwa kama fedha zilizotolewa na Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania kwa ajili ya kuendeleza mpango wa uwezeshaji ili kuwezesha utekelezaji wa mpango wa ukuaji kiuchumi.

Fedha hizi hazijaonyeshwa katika Hesabu Jumuifu za Taifa. Pia, bado taarifa ya utekelezaji wa mipango na miradi iliyofadhiliwa pamoja na makampuni ambayo yamefaidika kutokana na mpango haijawaasilishwa Ukaguzi.



**iii)Juhudi za kupata unafuu wa madeni kimataifa ya Sh.  
85,716,634,000**

Shirika la Fedha Duniani (IMF) lilifuta madeni yote ya Tanzania ya hadi kufikia tarehe Desemba 31, 2004. Kiasi cha madeni yaliyokuwepo hadi Desemba 2004 kilikuwa SDRs. 234,030,000 sawa na dola za Kimarekani milioni 336. Madhumuni ya kufuta madeni hayo ilikuwa kutoa rasilmali kubwa katika kupunguza umaskini na matatizo ya kiuchumi. Kufikia tarehe 30 Juni 2010, fedha za msamaha wa madeni zilizokuwa hazijatumika zilikuwa Sh. 85,716,634,000

Pamoja na ushauri wetu kuhimiza Serikali kuonyesha fedha Serikali haijaona umuhimu wa kufanya hivyo katika vitabu vyake vya hesabu.

**(iv) Gharama za kudhibiti ukwasi Sh. 26,850,000,000**  
Serikali inadaiwa na Benki Kuu ya Tanzania kiasi cha Sh. 26,850,000,000 ikiwa ni gharama za kudhibiti ukwasi.

**6.3.12 Taarifa ya Madeni Yasiyolipwa Sh. 160,756,067,191**

Hesabu Jumuifu za Taifa zinaonyesha madeni ambayo hayajalipwa kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2010 yanayofikia Sh.160,756,067,191. Hili ni ongezeko la asilimia 50.2 ikilinganishwa na kiasi cha madeni yasiyolipwa ya mwaka uliopita ya Sh. 107,063,198,140.

Ilibainika kwamba kati ya madeni yote ya kiasi cha sh.160,756,067,191, madeni ya kiasi cha Sh. 39,916,624,968 yalitokana na ununuzi wa mali na vifaa mbalimbali kupitia wazabuni (kama inavyoonekana hapa chini); hii inamaana kwamba hati za kuagiza vifaa na mali hazikulipwa kwa wakati hadi mwisho wa mwaka. Madeni haya hayakutakiwa kuwepo kwa kuzingatia mfumo mzima wa Serikali wa malipo kupitia mtandao wa IFMS unaozingatia malipo au mapato kwa fedha tasilimu.

Chanzo cha deni	Kiasi (Shs.)
Malipo ya mishahara ya nyuma	2,324,505,288
Mishahara ambayo haikuchukuliwa na wahusika	40,549,345,464
Matengenezo ya magari	2,040,379,524
Kodi ya pango ya ofisi	554,591,928
Kunyunyizia wadudu	4,872,883
Vifaa na huduma	39,916,624,968
Maji na Umeme	24,708,108,554
Mafunzo	18,456,400
Mali	35,399,700
Gharama za Kandarasi	50,543,057,975
Utekelezaji wa Mipango	60,724,507
<b>Jumla</b>	<b><u>160,756,067,191</u></b>

### 6.3.13 Vitega Uchumi vya Serikali Sh. 8,718,182,145,310

#### (i) Jumla ya vitega uchumi

Kwa mujibu wa Hesabu Jumuifu za Taifa, thamani ya vitega uchumi vya Serikali imeongezeka kwa kiasi kikubwa kutoka Shs.5,296,890,205,898 mwaka 2006/07 hadi kufikia Sh. 5,850,455,182,908 katika mwaka wa fedha 2007/08.

Katika mwaka 2008/09, thamani ya vitega uchumi vya Serikali iliongezeka na kufikia Sh. 7,074,822,870,933 na baadaye kuongezeka kwa kiasi kikubwa na kufikia Sh. 8,718,182,145,310 katika mwaka 2009/10. (Angalia jedwali hapa chini):

Maelezo	2006/07 (Shs)	2007/08 (Shs)	2008/09 (Shs)	2009/10 (Shs)
Mashirika na Taasisi za nje	833,792,464,960	709,955,580,650	931,255,007,966	957,398,792,596
Taasisi za ndani	4,463,097,740,898	5,140,499,602,258	6,143,567,862,967	7,760,783,352,714
<b>Jumla</b>	<b>5,296,890,205,858</b>	<b>5,850,455,182,908</b>	<b>7,074,822,870,933</b>	<b>8,718,182,145,310</b>

Zaidi ya hayo, ilibainika kuwa kiasi kilichotolewa taarifa hakikujumisha mashirika tisa ambayo taarifa zake hazikuwasilishwa pamoja na taarifa jumuifu kwa ajili ya ukaguzi

Vile vile, kiasi cha Sh. 100 bilioni zilizotolewa kwa Benki ya Rasilmali Tanzania kwa ajili ya kutunisha mtaji na kiasi cha shs 50 bilioni kwa ajili ya kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo; fedha hizi hazikujumuishwa kwenye Hesabu Jumuifu za Taifa kama sehemu ya rasilimali za Serikali.

(ii) Uwekezaji hasi Sh.2,740,753,908  
Hadi tarehe 30 Juni 2010, Uwekezaji mwingine wa mashirika ya kigeni ulikia kiasi cha Sh. 2,740,753,908. Hata hivyo, wakati hesabu zinafungwa tarehe 30 Juni, 2009 rasilmali hii ilikuwa na bakaa ya Sh.17, 597,200,948. na hivyo kutokuwepo sababu ya kutolewa kwa msaada wa aina hii ya uwekezaji.

Zaidi ya hayo, mitaji katika mashirika ya kigeni imeshuka kutoka Shs.122, 873,730,766 tarehe 30 Juni 2009 hadi Shs.116, 378,791,291 tarehe 30 Juni 2010. Sababu za upungufu au kushuka hazijatolewa.

Hata hivyo, katika kidokezo namba 13 hakitoi maelezo ya uwekezaji ikiwa ni pamoja na mali ambazo ziko chini ya udhibiti wa Serikali, matumizi ya Serikali, hisa za Serikali, mapato na gharama zilizotumika kwa kuzingatia kanuni na Mwongozo wa Kimataifa katika Sekta ya Umma ya kuandaa hesabu (IPSA 7 namba 8).

#### 6.3.14 Taarifa ya Mali Sh.7,981,954,338,324

Hesabu Jumuifu za Taifa zinaonyesha kwamba hadi tarehe 30 Juni 2010 kulikuwa na mali za thamani kiasi cha Sh. 7,981,954,338,324. Nyongeza ya mali katika kipindi cha mwaka ilikuwa Sh. 908,134,585,051 na mali zilizofutwa zilikuwa Sh. 1,696,150,527 hivyo kusababisha ongezeko halisi la asilimia 13 tangu taarifa ya mwisho ya tarehe 30 Juni 2009 ya Sh.7, 075,515,903,800 ilipotolewa. Jedwali hapa chini linaonyesha mwenendo wa mali katika kipindi cha mwaka:

S/N	Aina ya mali	Bakaa hadi 30 <sup>th</sup> Juni 2009	ongezeko	Mali zilizofutwa	Bakaa hadi 30 <sup>th</sup> Juni 2010
1	Ardhi na majengo	1,094,152,472,800	680,563,487,463	1,348,746	1,774,714,611,517
2	Mitambo na mashine	74,912,334,493	82,353,343,855	314,165,748	156,951,512,600
3	Thamani na vifaa	339,642,158,587	24,303,252,384	186,073,196	363,759,337,775
4	Magari	5,043,887,919,288	49,719,512,623	1,157,466,177	5,092,449,965,734
5	Komputa	132,886,132,703	20,550,336,101	37,096,660	153,399,372,144
6	Vifaa vya zimamoto	63,190,000	7,681,662,375	-	7,744,852,375
7	Intangible Assets	80,010,710,259	21,896,374,447	-	101,907,084,706
8	Biological assets	3,863,963,540	1,801,237,355	-	5,665,200,895
9	Ujenzi	306,097,022,130	19,265,378,448	-	325,362,400,578
	<b>Jumla</b>	<b>7,075,515,903,800</b>	<b>908,134,585,051</b>	<b>1,696,150,527</b>	<b>7,981,954,338,324</b>

Hata hivyo, katika kufanya mapitio ya taarifa ya mali imebainika kwamba:

(i) Hakuna daftari au kumbukumbu zinazoonyesha uandikishaji wa mali za Serikali

(ii) Jumla ya nyongeza ya mali iliyoripotiwa katika jedwali la mali ni Sh.908, 134,585,051 wakati Taarifa ya Mtiriko wa fedha inaonyesha jumla ya kiasi cha Sh.1, 026, 466,877,315 kilitumika kununua mali, hivyo kusababisha tofauti ya Sh.118,332,292,264

### 6.3.15 Taarifa ya Vifaa na mali nyingine Sh.16, 806,978,964

Hadi tarehe 30 Juni 2010 Hesabu Jumuiifu za Taifa zinaonyesha kiasi cha Sh 16,806,978,964 kikiwa ni vifaa na mali nyingine za Serikali. Kiasi hiki ni pungufu kwa asilimia 89 kutoka bakaa ya mwaka uliopita ya Sh.146,854,683,983.

### 6.3.16 Taarifa ya upotevu Sh.11,152,048,065

Hesabu Jumuiifu za Taifa zinaonyesha kuwa kulikuwa na ongezeko la upotevu wa mali na vifaa kutoka sh 3,128,398,112 mwaka 2008/2009 hadi Sh 11,152,048,065 mwaka 2009/2010, hii ikiwa ni ongezeko la Sh. 8,023,649,953 sawa na asilimia 256.

**6.3.17 Mifuko Maalum ya Fedha Sh. 78,014,807,604**  
Hesabu Jumuiifu za Taifa zilionyesha kiasi cha Sh. 78,014,807,604 katika Mifuko Maalum inayosimamiwa na Wizara na Idara mbalimbali kulingana na Kifungu cha 12 cha Sheria ya Fedha ya Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004). Ongezeko hili la Sh. 32,460,970,038 ni sawa na asilimia 140 ya bakaa iliyokuwepo mwaka wa fedha uliopita.

Hata hivyo, kiasi hiki kilikuwa ni bakaa katika mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2009 ikiwa ni fedha za uendeshaji katika Wizara na idara mbalimbali. Aidha, kiasi hakijumuishi fedha nyingine zilizotolewa mwaka wa fedha 2009/10 ikiwa ni pamoja na zile zilizotolewa kama mkopo. Taarifa ya Fedha za mifuko iliyoorodheshwa hapa chini haikuwa katika Hesabu Jumuiifu za Taifa. Mifuko hiyo ni:

- Mfuko wa Maendeleo Hazina
- Polisi Zawadi na Fedha za tozo/adhabu
- Mfuko wa Zawadi Magereza
- Mfuko wa Maafa
- Mfuko wa Maendeleo ya Elimu
- Mfuko wa Nyumba
- Mfuko wa dharura wa Mashirika
- Mfuko wa Huduma za Afya
- Mfuko wa Zana za Kilimo

**6.3.18 Usuluhisho wa Taarifa za benki na Daftari la fedha**

Mapitio ya Taarifa ya Usuluhisho wa tofauti kati ya akaunti za benki ulibaini kuwepo kwa tofauti ambazo bado kusuluhishwa katika vitabu vya fedha (Kiambatanisho VI) kama ifuatavyo:

- 1 Makusanyo katika Benki yasiyo katika Kitabu cha Fedha 56,230,975,146.63
- 2 Malipo Katika Kitabu cha Fedha (bila hundi) 83,500,942,913.53
- 3 Malipo katika benki yasiyokuwa katika Kitabu cha Fedha 524,588,992,794.08

4 Makusanyo katika Kitabu cha Fedha yasiyokuwa Benki  
182,857,092,164.47

Taarifa hiyo pia ilionyesha hundi za Shs.304, 876,466,064 ambazo baadhi yake hazikuwa zimelipwa kwa zaidi ya miezi 6. Hakuna marekebisho yaliyofanyika kufuta hundi hizo au kuingizwa kwa kiasi husika katika akaunti ya benki.

Zaidi ya hayo, makusanyo katika Benki ambayo hayakuwa katika kitabu cha fedha yanafikia jumla ya Shs.56, 230,975,147 na malipo katika benki ambayo hayakuwa yamefanyika katika kitabu cha fedha yalikuwa Sh. 524, 588,992,794. Hapakuwa na kumbukumbu yoyote ya makusanyo na malipo haya na kufanya iwe vigumu kufuatilia chanzo chake.

**Matumizi zaidi katika akaunti za benki  
Sh.1,331,073,630,470.30**

Mapitio ya taarifa za akaunti ya Mfuko Mkuu wa Serikali yamebaini kuwa, katika kipindi cha mwaka husika, Mfuko Mkuu wa Serikali ulipokea jumla ya Sh. 8,088,374,116,556.58 kama mapato ikilinganishwa na jumla ya matumizi ya Sh. 8,550,640,390,566.58 na hivyo kusababisha matumizi zaidi katika akaunti ya benki ya jumla ya Sh.462,266,274,010.32 kwa mwaka husika. Kiasi hiki kikijumlishwa na matumizi zaidi ya mwaka jana ya Sh. 868,807,356,459.98 kinafanya jumla ya malimbikizo ya matumizi ya ziada katika akaunti ya Benki Kuu ya Tanzania kufikia Sh. 1,331,073,630,470.30. Hata hivyo, matumizi haya ya ziada katika akaunti ya Benki Kuu ya Tanzania hayakuonyeshwa katika Taarifa ya Deni la Taifa.

#### **6.3.19 Fedha ambayo haikutumika kutorudishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali Sh. 31,821,562,811**

Hesabu Jumuifu za Taifa zimeonyesha kuwa kiasi cha Sh 31,948,316,299 kilibaki bila kutumika katika za benki. Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2009 ni kiasi cha Sh. 126,753,488 tu ndicho kilikuwa kimerejeshwa katika Mfuko

Mkuu wa Serikali. Tofauti ya kiasi cha Sh 31,821,562,811 kilikuwa bado kurejeshwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

**6.3.20 Usimamizi wa madeni yanayotarajiwa kutokana na ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi katika kutekeleza miradi (PPP)**

Kufuatia uanzishaji wa sera ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, Ofisi ya Waziri Mkuu imepewa dhamana ya kusimamia sheria ya ubia kati ya sekta binafsi na sekta ya umma ya mwaka 2010 inayotoa mwongoo wa utekelezaji wa sera na uendeshaji wake.

Sera ya hii imeanza kutumika Tanzania kupitia ubinafsishaji na hasa katika kutoa huduma kwa jamii katika vitega uchumi mbalimbali ikihusisha kwa kiasi kidogo sekta ya Nishati na Mawasiliano. Mikataba mingi ni ya makubaliano ambayo hayahusishi ukarabati na uwekezaji katika vitega uchumi vipya.

Baadhi ya sekta zimeonyesha ufanisi kwa kutumia sera hii. Kwa mfano Elimu, Afya na Maji.

**6.3.21.1 Udhaifu katika mfumo wa kusimamia ubia kati ya Sekta ya Umma na binafsi**

Mapitio ya makubaliano yaliyofanywa kati ya Serikali na sekta binafsi kwa baadhi ya wawekezaji binafsi imeonekana kuwepo mafanikio kidogo yenye mapungufu makubwa. Mazungumzo hayo ni kati ya Serikali na SONGAS LTD, IPTL, ARTUMAS, TRL, ATCL, Kiwira Coal Mine (TANPOWER LTD), City Water na TICTS. Mapungufu yafuatayo yamebainika:

- i. Pamoja na matatizo na mapungufu yaliyotokana na sera ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Fedha haijatengeneza mwongozo na viwango vinavyotumika katika sera ya ubia ambayo ingesaidia kuepuka madeni yasiyotarajiwa. Bado Serikali inatengeneza kanuni za sheria ya ubia na mikakati

na inategemea kukamilisha kazi hiyo ifikapo mwanzoni mwa mwezi Julai 2011

- ii. Hakuna uthibitisho wowote kama tathimini ya kina imefanywa na Serikali ili kuona endapo kuna faida au hasara kuingia ubia na sekta binafsi
- iii. Hakuna uthibitisho unaoonyesha kuwa Sheria ya Manunuzi inatumika katika kuwapata wawekezaji na kwamba wataalamu waliobobea katika fani mbalimbali wanatumiwa katika kufanya uchambuzi wa kuwapata wawekezaji wenye uwezo.
- iv. Mfumo wa ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa kwa ubia kati ya Serikali na sekta binafsi umeonekana kuwa dhaifu
- v. Hakuna uthibitisho wowote kama tathimini ya viashiria vya hatari vinavyoweza kutokea endapo Serikali itaingia ubia na sekta binafsi inafanywa kabla kabla ya makubaliano ya kuingia ubia.
- vi. Imetuwia vigumu kupata tathimini nzima ya uwezo wa rasilmali na fedha anaopaswa kuwa nao mwekezaji au mbia na Serikali. Imeonekana kwamba Serikali inachukua jukumu la kuwapa fedha wawekezaji binafsi kwa njia ya kutoa fedha moja kwa moja au kwa mikopo au kuwadhamini kwa mfano;

- Mkopo kwa SONGAS LTD
- Malipo kwa IPTL kuiwezesha kuendelea kutoa huduma
- Malipo ya mishahara kwa watumishi wa TRL na TANPOWER LTD
- Kutoa mkopo kwa ARTUMAS
- Na kutoa udhamini kwa Kagera Sugar Ltd

Matokeo ya udhaifu uliotajwa hapo juu ni kama ifuatavyo:

- i. Serikali kuingizwa katika gharama ambazo hazikutarajiwa kutokana na ubia na sekta binafsi na kusababisha matumizi ya fedha ambazo hazikuwa kwenye maksio ya Serikali
- ii. Bila kuwepo uchanganuzi wa kina wa vihatarishi katika uwekezaji Serikali imejikuta ikiingia ubia na wawekezaji



wasio na uwezo kifedha na baadaye mzigo wote hubebwa na Serikali

- iii. Bila kufanya uchambuzi wa kina wa gharama na manufaa pamoja na thamani ya fedha baadhi ya rasilmali au vitega uchumi vimeonekana kutokuwa endelevu kiuchumi

#### **6.3.21.2 Usimamizi wa Madeni Yamkini kutokana na ubia kati ya Serikali na sekta binafsi mali na amana zake**

Mara nyingi makubaliano ya ubia (PPP) yameonekana kutokuwa na mpangilio mzuri wa uwendeshaji kwani ni dhahiri kwamba mwisho wa ubia husababisha Serikali kuwa na madeni makubwa ambayo haikuyatarajia. Mapitio ya ukaguzi yamebaini yafuatayo:

- i. Kutoa mikopo na kudhamini sekta binafsi ni makosa kulingana na kifungu namba 13 & 14 cha Sheria Mikopo, Udhamini na Misaada ya mwaka 1974 (iliyorekibishwa mwaka 2004)
- ii. Hakuna vielelezo vinavyoonyesha rehani kwa mikopo na dhamana inayotolewa kwa wawekezaji binafsi. Zaidi ya hayo, Mashirka ya Umma hayatakiwi kutoa ahadi na rehani kama inavyoelekezwa katika kifungu namba 13(c) & 14(i) cha Sheria ya Mikopo, Udhamini na Misaada ya mwaka 1974 (iliyorekibishwa mwaka 2004)
- iii. Mali zote za Serikali pamoja na zile zinazotokana na ubia kati ya Serikali na sekta binafsi haziandikwi wala kuoneshwa katika Hesabu Jumuiifu za Taifa ingawaje ni chache.
- iv. Makisio ya Serikali hayazingatii gharama za madeni yanayotarajiwa yatokanayo na ubia na sekta binafsi

Kwa kutokuwepo rehani halisi, Serikali inajiweka katika mazingira hatarishi ya ukwasi endapo wawekezaji watahinda kulipa mikopo. Pia, mali za Serikali kutokuandikwa kwenye daftari la fedha kunaweza kusababisha upotefu wa mali hizo bila kujua na pia madeni yasiyokuwa na kumbukumbu hayawezi kulipwa

kwa wakati kwani inakuwa vigumu kujua muda yanapokuwa yameiva.

#### **6.3.21.3 Kutojihusisha kikamilifu kwa Serikali katika kutayarisha mikataba na kujenga makubaliano**

Serikali iliingia makubaliano ya mikataba ifuatayo:

- i. Ujenzi wa hosteli ya Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)
- ii. Ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma na NSSF, PPF, PSPF, LAPF and NHIF and
- iii. Ujenzi wa Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela-Africa na PPF.

- Ukaguzi umebaini kuwa hakuna vielelezo vinavyoonyesha ushiriki wa Serikali katika kubuni na kujenga miradi yote mitatu iliyotajwa hapo juu

- Ofisi ya ukaguzi haikupewa mikataba husika inavyoonyesha masharti katika ubunifu, ujenzi na makubaliano ya namna ya kufanya malipo

Ushiriki mbovu wa Serikali katika kufuatilia mwenendo wa ujenzi wa miradi hiyo mitatu, kunaweza kuisababishia kubeba gharama kubwa kwa wakandarasi kutumia bei za juu kwa gharama za ujenzi.katika

#### **6.3.22 Kutozingatia sheria za fedha na miongozo ya kimataifa ya sekta ya umma katika kuandaa taarifa za fedha**

Hesabu Jumuifu za Taifa hazikuandaliwa kulingana na kifungu cha 25(1) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebisha 2004) inayomtaka Mhasibu Mkuu wa Serikali kuandaa taarifa na kuzipeleka kwa Waziri wa Fedha na Mdhhibiti na Mkaguzi na Mkuu wa Hesabu za Serikali zikionyesha mali zote na madeni ya Mfuko Mkuu wa Serikali (yaani Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania).

Taarifa iliyowasilishwa Ukaguzi haikuonyesha mali na madeni yote ya Serikali kama vile; majengo, madaraja, barabara, shule, hospitali na kadhalika.

Zaidi ya hayo, Hesabu Jumuifu za Taifa hazikuandaliwa kwa kufuata Sehemu ya 6 ya Miongozo ya Kimataifa ya Uandaji Taarifa za Fedha katika Sekta ya Umma (IPSAS). Kwa kutoonyesha mali zote na madeni yote ya Serikali kwenye vitabu vya fedha kunaweza kusababisha upoteve wa mali hizi bila Serikali kujua.

Madeni ya Serikali yasiyo kuwa na kumbukumbu huchelewa kulipwa kwa muda unaotakiwa. Kutokujumisha taarifa zote za taasisi za Serikali, Serikali za Mitaa na Wakala wa Serikali kwenye Hesabu Jumuifu za Taifa kunasababisha Taifa kuwa na taarifa ambazo sio kamili na kupoteza maana kwa umma.

## SURA YA 7

### 7.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UKAGUZI

#### 7.1. Utangulizi

Sura hii, inachambua misingi ambayo imepelekea utoaji wa aina fulani ya maoni ya ukaguzi. Uchambuzi huu una lengo la kufafanua vigezo na msingi iliyotumika katika kutoa maoni ya ukaguzi kama ilivyojadiliwa katika sura iliyotangulia.

Hati ya ukaguzi ni maoni rasmi au kukataa kutoa maoni kunakotolewa na mkaguzi huru kutokana na ukaguzi au tathmini iliyofanywa kwa Taasisi au Idara yake (mkaguliwa). Hati hii hutolewa ili kumwezesha mtumiaji wa taarifa za fedha kama hakikisho ili aweze kufikia maamuzi kutokana na matokeo ya ukaguzi uliofanywa.

Hati ya ukaguzi huchukuliwa kama nyenzo muhimu wakati wa kutoa taarifa za fedha kwa watumiaji. Inakusudia kulishauri Bunge na watumiaji wengine wa taarifa za Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa kama taarifa za fedha zimetayarishwa kwa kuzingatia viwango kubalifu vya Kimataifa vya kutayarisha taarifa za fedha katika sekta ya Umma (IPSAS) na kwa namna inavyotakiwa chini ya Kifungu cha 25 (4) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (zilizorekebisha 2004) ikiwemo Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa kuzingatia Sheria na Kanuni nyingine zilizowekwa.

Kwa lugha ya kawaida, hati ya ukaguzi ni hakikisho kwamba taarifa ya fedha iliyowasilishwa na mkaguliwa kwa kiwango kikubwa ni sahihi na ya kuaminika kwa ajili ya kufanya maamuzi ya Serikali kama vile Serikali kutathmini kama fedha zilizotengwa kwa ajili ya Wizara/Idara/Wakala na Sekretarieti za Mikoa zimetumika kwa manufaa ya Umma.

Ni muhimu kutambua kwamba hati ya ukaguzi inayotolewa kwa taarifa za fedha siyo hakikisho la moja kwa moja kwamba hali ya kifedha ya Taasisi ni nzuri na sahihi kabisa kuweza kutegemewa katika kufanyia maamuzi. Hati ya ukaguzi ni maoni tu kwamba taarifa iliyowasilishwa ni sahihi na haina makosa makubwa ambapo maamuzi mengine huachiwa mtumiaji wa taarifa kuamua.

## 7.2 Aina ya hati za ukaguzi

Kuna aina tano (5) za hati za ukaguzi, kila moja ikieleza mazingira tofauti anayokutana nayo mkaguzi. Hati hizo ni kama ifuatavyo:

- **Hati inayoridhisha**

Wakati mwingine hati hii huchukuliwa na wengi kama “hati safi”. Aina hii ya hati hutolewa wakati taarifa za fedha zilizowasilishwa hazina makosa mengi na zimezingatia matakwa ya viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS) na kwa mujibu wa Kifungu cha 25 (4) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebisha 2004) ikihusisha uzingatiaji wa Sheria na Kanuni.

- **Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo**

Katika mazingira fulani, hati ya ukaguzi inayoridhisha huweza kurekebisha kwa kuongeza aya yenye masuala ya msisitizo yanayodokeza masuala muhimu ambayo yasiporekebisha na mkaguliwa yanaweza kusababisha kutolewa kwa hati yenye shaka katika ukaguzi unaofuata. Kuongezwa kwa aya ya masuala ya msisitizo hakuathiri hati ya ukaguzi iliyotolewa.

Madhumuni ya masuala ya msisitizo ni kutoa uelewa zaidi kwa hali iliyotokea wakati wa ukaguzi licha ya kutolewa kwa hati ya ukaguzi inayoridhisha.

- **Hati yenye shaka**

Hali na mazingira inayosababisha kutolewa kwa hati hii, huwa katika kundi moja au mawili ambayo ni:

- Kunapokuwa na mashaka ambayo husababisha mkaguzi ashindwe kutoa hati ya ukaguzi.

Mambo yanayoweza kusababisha kutolewa kwa hati hii ni haya yafuatayo:

- Matumizi yasiyokuwa na hati za malipo
- Bidhaa na huduma zimenunuliwa bila kuwa na hati za kupokelea hivyo kukosekana uhakikisho kama zimepokelewa na kuingizwa katika vitabu
- Malipo mbalimbali kukosa viambatanisho
- Stakabadhi za maduhuli kutowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi
- Mali zinazomilikiwa au kununuliwa kukosa majedwali. Hii inasababisha mashaka ya kuwepo kwa mali hizo
- Kutopatikana kwa ushahidi wa mapokezi ya fedha zilizolipwa. Kutokuwepo stakabadhi za kukiri mapokezi kutoka kwa walipwaji unaweza kusababisha upotevu wa fedha. Katika hali hii kunakuwa na ufinyu wa mawanda ya ukaguzi.

Pale ambapo mkaguzi anapotoa maoni yanayotofautiana na hali halisi ya taarifa ya fedha zilizotolewa (kutokubaliana na taratibu kubalifu za utunzaji na uzingatiaji wa sheria na kanuni).

Kutokubaliana na uongozi katika njia iliyo bora ya utunzaji wa kumbukumbu na uzingatiaji wa sheria hutokea katika mazingira yafuatayo:

- Mali zinazomilikiwa na Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa kutoingizwa katika rejista.
- Mali zilizoununuliwa kutoingizwa vitabuni na hivyo kutolewa na matumizi yake kutoweza kuthibitishwa.
- Kutobainishwa salio la benki katika vitabu vya fedha

- Wakati kumbukumbu za hesabu zinapokosekana, kutokamilika au kutokuwa sahihi.
- Kutobainishwa kikamilifu kwa sera ya uhasibu iliyotumika
- Pale ambapo Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa zinapotumia njia isiy sahihi kama vile viwango vya uchakavu visivyo sahihi

Kwa hali hiyo, hati yenye shaka inaonyesha kuwa taarifa za fedha zilizowasilishwa ni sahihi isipokuwa kwa madhara yatokanayo na masuala halisi ya kiukaguzi yaliyogunduliwa.

#### (iv) Hati isiyoridhisha

Hati isiyoridhisha hutolewa inapogundulika kuwa taarifa za fedha za Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa kwa kiasi kikubwa si sahihi zinapoangaliwa katika ujumla wake, hazikuandaliwa kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS) na kwa namna inayotakiwa katika Kifungu cha 25(4) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004) inayoelezea kuwa taarifa zilizopo siyo sahihi na haziaminiki katika kupima matokeo ya uendeshaji katika Wizara/Idara/Wakala na Sekretarieti za Mikoa.

Maelezo ya hati isiyoridhisha huwa wazi ambapo ninaeleza kwamba taarifa za fedha hazikuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS) na kwa namna inayotakiwa katika Kifungu cha 25(4) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (ilyorekebishwa 2004).

#### (V) Hati mbaya

Hati mbaya ambayo hujulikana kama kukataa kutoa hati, hutolewa wakati ninaposhindwa na hivyo kukataa kutoa hati kwa taarifa za fedha. Aina hii ya hati hutolewa ninapotaribu kufanya ukaguzi kwa Taasisi na kushindwa kutokana na sababu mbalimbali na hivyo kusababisha kutotoa hati ya ukaguzi. Hali inayosababisha kutolewa kwa hati mbaya inaweza kusababishwa na kukosekana kwa uhuru au ufinyu mkubwa wa mawanda ya ukaguzi ama kwa

makusudi au la, mkaguliwa kukataa kutoa ushahidi na taarifa kwangu katika maeneo muhimu kwenye taarifa za fedha na panapokuwa na mashaka makubwa katika uendeshaji wa shughuli za mkaguliwa.

**Jedwali: Misingi ya kutoa hati ya ukaguzi**

Hali na sababu zinazosababisha kutolewa kwa hati ya ukaguzi	Masuala yenye athari lakini si mazito	Masuala yenye athari na mazito
Kutokukubaliana	Hati yenye shaka	Hati isiyoridhisha
Kuwepo mashaka		Hati mbaya

Jedwali hilo hapo juu hutoa mwongozo wa namna hati za ukaguzi zinavyotolewa, tafsiri yake ni kama ifuatavyo:

- (a) Pale ninapogundua masuala yanayosababisha kutokubaliana na masuala hayo ni yenye athari lakini si mazito, ninatoa hati yenye shaka (isipokuwa pale ambapo masuala yana athari na ni mazito hati isiyoridhisha hutolewa)
- (b) Pale ambapo matokeo ya ukaguzi yanasababisha kuwepo mashaka na:
  - (i) Mashaka hayo ni makubwa yana athari lakini si mazito, hati yenye shaka hutolewa
  - (ii) Mashaka yana athari na ni mazito, hati mbaya hutolewa

Madhumuni ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni kutoa ripoti ya ukaguzi ambayo inaonyesha uwiano ulio wazi, kuweka msisitizo kwa mambo muhimu yanayohitaji kushughulikiwa na uongozi wa wakaguliwa na kubainishwa fursa za kuboresha utendaji.



Maelezo ya kina ya hati za ukaguzi wa hesabu zilizotolewa katika mwaka wa ukaguzi na mwaka uliopita yako katika kiambatanisho VIII.

Jumla ya Wizara, 56, Sekretarieti za mikoa 21 na Balози 31 na hivyo kufanya jumla ya Wizara / Mikoa / Balози zilizokaguliwa katika mwaka wa fedha 2009/2010 kuwa 108 na matokeo yake ni kama ifuatavyo:

### **7.3 Hati inayoridhisha isiyo na mambo ya msisitizo**

Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa na Balози 22 (20.4%) kati ya 108 zilizokaguliwa mwaka huu zilipewa hati inayoridhisha isiyo na masuala ya msisitizo kama inavyoonekana katika

### **7.4 Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo**

Matokeo ya ukaguzi ya mwaka huu yalionyesha kwamba kati ya Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa 108 zilikaguliwa. Kati ya hizo 61 au asilimia 56.5% zilipewa hati zinazoridhisha zenye masuala ya msisitizo.

### **7.5 Hati yenye shaka**

Kati ya Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa 108 zilizokaguliwa 22 au asilimia 20.4 zilipewa hati zenye shaka.

### **7.6 Hati isiyoridhisha**

Mafungu mawili (2) au asilimia 2 yalifanya vibaya na hivyo kupewa hati isiyoridhisha. Mafungu hayo ni Hesabu Jumuiifu za Taifa na Sekretarieti ya Mkoa wa Lindi

### **7.7 Hati mbaya**

Katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2009/2010. Ukaguzi ulikutana na hali iliyosababisha ufinyu wa wigo wa ukaguzi kutokana na janga la moto lililoikumba Ofisi ya Sekretariati

ya Mkoa wa Dodoma na hivyo kunifanya kushindwa kutoa hati ya ukaguzi.

Jedwali lifuatalo pamoja na **Kiambatisho VII** vinaonyesha aina ya hati zilizotolewa kwa Wizara/Idara na Sekretarieti za Mkoa na Balozi katika taarifa za fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2010.

Maelezo	Hati inayoridhisha isiyo na masuala ya msisitizo	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo	Hati yenye shaka	Hati isiyoridhisha	Hati mbaya	Jumla
Wizara/Idara	11	31	13	1	-	56
Sekretarieti za Mkoa	3	9	7	1	1	21
Jumla ndogo	14	40	20	2	1	77
Balozi	8	21	2	-	-	31
Jumla Kuu	22	61	22	2	1	108
Asilimia	20.4%	56.5%	20.4%	1.9%	0.9%	100%

#### 7.8 Wizara/Idara na Sekretarieti za Mkoa zilizopewa hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo.

Ufuatao ni mchanganuo wa sababu za kutoa hati inayoridhisha yenye mambo ya msisitizo kwa kila fungu

1	Fungu 14 - Jeshi la Zima Moto na Uokoaji
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• masuala ya ukaguzi wa mwaka uliopita ambayo yalikusiana na malipo kwa ajili ya ununuzi wa magari yenye thamani ya Sh.705,197,958 hayakujibiwa na utawala hii ikiwa ni dalili kwamba hakuna ushahidi wa magari husika kupokelewa na hivyo kuleta hasara kwa Serikali ya kiasi hicho cha fedha.</li> <li>• Utawala hakueleza hatua zilizochukuliwa kulipa madeni ya jumla ya Sh. 396,615,262. Aidha, taarifa ya utekelezaji wa miradi yenye thamani ya jumla ya Sh.1,372,322,224 haikutolewa.</li> <li>• Kiwango cha kazi iliyofanywa na mkaguzi wa ndani kilikuwa duni. Kwa mfano maeneo ya mapato na manunuzi hayakukaguliwa katika mwaka wa ukaguzi. Hakukuwa na ushahidi wa kimaandishi kuthibitisha kwamba kazi inayofanywa na mkaguzi wa ndani ni iliwekwa katika kumbukumbu kwa ajili ya mapitio.</li> <li>• kanuni zinazotumika katika Sekta ya Umma inahitaji kila taasisi kuandaa sera ya usimamizi wa vihatarishi ambayo inafafanua jinsi ambavyo vihatarishi vinaweza kudhibitiwa. Katika ukaguzi wetu tulibabini kuwa Jeshi la Zima moto na Uokoaji halikuandaa sera ya usimamizi wa vihatarishi.</li> <li>• Jumla ya Shs.298, 600,000 zililipwa kwa M / S Noble Motors Ltd kwa ajili ya kusambaza magari kwa bei ya Shs.298, 600,000. Uthibitisho wa kuletwa kwa magari hayo toka kwa mwuzaji/wakala haukuthibitika..</li> <li>• Jumla ya Shs.41, 276,400 zililipwa kwa Open Sanit Enterprise kwa ajili ya ununuzi wa sare za Zima Moto na na uokoaji kwa bei ya Shs.41, 276,400. Mapokezi ya vifaa hivi hayakuthibitika.</li> </ul>

2	<p><b>Fungu 16: Mwanasheria Mkuu wa Serikali</b></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Kiasi cha Shs.559, 587,088.70 kilitolewa kwa viongozi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama masurufu kwa ajili ya gharama ya kazi mbalimbali kiasi ambacho hakikurejeshwa kinyume na Kanuni Na. 103 (1) ya Ununuzi wa Umma 2001 (iliyorekebishwa 2004).</li> <li>• Katika mwaka husika, jumla ya Shs.15, 979,058 zililipwa kwa New Habari (2006) Co. (T) Ltd na M / s White Sand Hotel kwa ajili ya huduma zilizotolewa katika miaka iliyopita (2006/07 na 2008/09) kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kinyume na Kanuni Na.85 (2) &amp; (3) ya Fedha za Umma ya 2001 (iliyorekebishwa 2004).</li> </ul> <p><b>Maswala mengine</b></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Malipo ya jumla ya Shs.70,708,701.3 hayakuambatanishwa na nyaraka sahihi, kinyume na Kanuni ya 95 na 139 ya Fedha za Umma 2001 (revised 2004).</li> <li>• Kiasi cha Sh. 93,000,000 zililipwa kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Makazi kwa ajili ya ununuzi wa nyumba zilizotengwa katika Kiwanja Na. 8 / 1 KB1, Independence Avenue Tanga. Hata hivyo, hapakuwa na makubaliano rasmi ya kimkataba kuhalalisha malipo hayo.</li> </ul>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kifungu cha 45 cha Sheria ya Ununuzi ya umma ya 2004 na Kanuni ya 25 ya Ununuzi wa Umma viinahitaji Kitengo cha manunuzi (PMU) kuandaa mpango wa mwaka wa manunuzi. Hata hivyo, ilibainika kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali hakuandaa mpango wa mwaka wa manunuzi kwa mwaka wa fedha 2009/2010 kama inavyotakiwa na sheria.</li> </ul>

3	<p><b>Fungu 19 - Mahakama za Mwanzo na Wilaya</b></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Kulikuwa na matumizi yenye nyaraka pungufu ya kiasi cha Sh. 29,527,500 kinyume na Kanuni. 95 (4) ya Kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebisha 2004). Hatukuweza kujiridhisha kama matumizi haya yalikuwa halali.</li> <li>• Hapakuwa na kumbukumbu nzuri za utunzaji wa vifaa kiasi kwamba vifaa vyenye thamani ya Sh. 68,842,603.70 (32,842,603.70 + 36.000,000.00) havikuweza kuthibitika kama vilipokelewa na kutumika kama ilivyokusudiwa. Udhaifu huu unaweza kusababisha mali ya umma kupotea pasipo kujulikana.</li> <li>• Afisa Masuuli hakuwa na anatumza daftari la mikataba kiasi kwamba hapakuwa na kumbukumbu kuhusu zuio (retention) la Sh.65,375,900.50 lilivo lilivyo lipwa kwa wakamdarasi. Hali hii inaweza kusababisha upotevu wa mali ya Umma kutokana na wakandarasi kudai malipo ya ziada bila utawala kujua usahihi wa malipo husika.</li> <li>• Utaratibu kwa ajili ya utunzaji wa vifaa vya stoo unajumuisha mafungu matatu bila kuwa na mipaka kati ya mafungu haya. Vilevile hapakuwa na utaratibu wa kuhesabu vifaa mwisho kiasi kwamba vifaa vyenye thamani ya Sh. 7,051,675 havikuweza kuthibitishwa kama vilikuwa ni vya fungu 14.</li> </ul>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Udhibiti wa masurufu haukuwa madhubuti kwa vile kumbukumbu za masurufu haziko kwa wakati pamoja na kutokuwa na akaunti binafsi ya kwa kila mfanyakazi mwenye masurufu ili kudhibiti utoaji na marejesho ya masurufu. Udhaifu huu umesababisha bakaa za masurufu za jumla ya Sh 26,107,990 hazikujulikana na kutolewaa taarifa katika taarifa za fedha.</li> </ul>

	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Udhhibiti wa mfumo wa ndani wa Mahakama za wilaya na za Mwanzo ni dhaifu kutokana na utendaji duni wa Kitengo cha ukaguzi wa ndani, Kamati ya Ukaguzi na Kamati ya Manunuzi.</li> </ul>
<b>4</b>	<b>Fungu 22: Deni la Taifa na Huduma za ujumla</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kulikuwa na ongezeko kubwa cha deni la taifa mwisho wa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2010 ambapo kiasi cha deni la taifa kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2009 kilikuwa Sh.7,621,286,730,034, ambapo taehe 30 Juni 2010 deni la taifa lilifikia kiasi cha Sh.10,503,806,011,885 ongezeko la Sh.2,882,519,281,851 (38% zaidi ya deni la mwaka uliopita) . Hali hii ni ya kutisha kama haitaendana na ukuaji wa hali ya uchumi wa nchi.</li> <li>• Kulikuwa na kiasi cha Sh.1,813,094,721,953 kilicholipwa kwa wadai mbalimbali nje ya nchi bila ambapo wadai hawa hawakukiri kupokea malipo haya.</li> <li>• Kulikuwa na masuala ya ukaguzi wa miaka iliyopita yenye ya Sh.9,479,812,094 na US\$.2,100,000 ambayo yalikuwa hayakujibiwa.</li> <li>• Hapakuwa na nyaraka za kuthibitisha malipo ya jumla ya Shs.251,325,000 kwa ajili ya kulipia huduma ya utekelezaji, maandalizi na kukuza maendeleo ya kiuchumi kwa njia ya uwekezaji wa kigeni.</li> </ul>
<b>5</b>	<b>Fungu 23: Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Thamani ya mali tarehe 1 Julai 2009 iliripotiwa katika taarifa ya fedha kama Sh. 11,258,831,928.94 wakati kiasi hicho wakati wa kufunga mwaka uliomalizika Juni 30, 2009 kilikuwa Sh.7,725,971,814.93 na hivyo kusababisha tofauti ya Sh.3532860114. Mali ya Idara iliyo ripotiwa katika taarifa ya Mali na Dhima haikuwa sahih.</li> </ul>

	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Idara iliendesha mafunzo ya ndani ya muda muda mrefu na mfupi ambapo jumla ya Sh. 2428558080 zilitumika bila kwa na mpango wa mafunzo kinyume na Ibara ya 5 ya Agizo la Serikali Na.1 ya 2009 ambayo inahitaji kwamba kila mafunzo ambayo yame fadhiliwa na Serikali kuwa na mpango wa mafunzo.</li> <li>• Manunuzi yenye thamani ya Sh. 49,433,343,399.58 yalifanywa katika mwaka husika nje ya mpango wa mwaka wa manunuzi.</li> <li>• Mihadi ya jumla ya Sh. 2,457,034,306.30 ilifanywa bila kuwa na mikataba au hati za malipo kuonyesha kwamba fedha zilihamishwa toka Akaunti ya Amana kwa lengo la kuepuka kusalimisha fedha katika mfuko mkuu wa Selikari ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha kama inavyotakiwa na Sehemu ya 23 ya Sheria ya Fedha Na. 6 ya 2001 (iliyorekebisha 2004).</li> <li>• Kulikuwa na mali yenye thamani ya Shs.15,639,981,948.43. ambayo haikuwa imeingizwa katika daftari la mtandao wa IFMS</li> </ul>
6	<b>Fungu 26: Ofisi ya Makamu wa Rais</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Taarifa za Fedha mwisho wa mwaka zilionyesha kuwa kompyuta na samani zilikuwa na thamani ya Sh. 408,925,994.06 wakati daftari la mali lilionyesha vifaa hivyo kuwa na thamani ya Shs.336,030,693.52 na hivyo kuwa na tofauti ya Shs.108,416,460.54.</li> <li>• Kutumia tofauti kanuni za matumizi. Malipo ya posho ya Sh.35,036,656.06 yalilipwa kupitia vifungu tofauti vya malipo bila kuwa na kibali cha cha kuhamisha fedha hizo kinyume na Kanuni. 51 (3) ya Kanuni za Fedha za Umma.</li> </ul>

7	Fungu 27: Msajili wa Vyama vya Siasa
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Jumla ya Shs.56, 180,087.44 zilitumika na Msajili wa Vyama vya Siasa wakati hazikuhusiana na shughuli za Vyama vya Siasa.</li> <li>• Kiasi cha Shs.272 ,759,940.50 zilitumika kulipia madeni ya miaka ya nyuma kwa Bodi ya Wadhamini chama cha UDP bila kuonyeshwa katika taarifa za fedha kama malipo yaliyo ahirishwa. Maliopo haya yana athiri utendaji wa Ofisi kwa mwaka wa sasa wa fedha.</li> <li>• Taarifa za fedha kwa malipo ya ruzuku ya Sh.17,146,819,904 kwa vyama vya Siasa mbalimbali hazikuwasilishwa na vyama husika katika Ofisi ya Msajili kinyume na Kifungu Na..14 (1) na (3) cha Sheria ya 1992 ya Vyama vya Siasa.</li> </ul>
8	Fungu 28: Idara ya Jeshi la Polisi
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Tulibaini kuwa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani hakikufanya kazi kama inavyotakiwa. Kwa mfano maeneo ya mapato na manunuzi hayakukaguliwa katika mwaka huo wa ukaguzi. Hapakuwa na ushahidi wa maandishi kuthibitisha kwamba kazi ya Mkaguzi wa ndani iliratibiwa vema ili kurahisisha mapitio ya taarifa hizo.</li> </ul>



	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Uhakiki wa bakaa mbalimbali ulionyesha kuwa taarifa ya Mapato na Matumizi haikuwa na bakaa wakati taarifa ya mtiririko wa fedhailionyesha Sh.2,443,438,541. Kulingana na maelezo ya utawala. Hii ni kinyume na Sehemu. 25 (2) ya Sheria ya Fedha ya umma ya mwaka 2001 (Revised 2004) ambayo inampa Afisa Masuuli wajibu wa kuandaa taarifa za fedha.</li> </ul>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Matokeo ya maamuzi ya mahakama kuhusu hasara ya fedha ya jumla ya Shs.56,701,500 haijawasilishwa.</li> <li>• Kibali kutoka PPRA kuhusu malipo ya jumla ya Tshs.801,431,485 si inavyohibitishwa kuwa kupatikana.</li> <li>• Idara ya Jeshi la Polisi ilikuwa na mihadi ya Shs.268,736,371 kwa ajili ya bidhaa na huduma ambayo ilikuwa haijalipwa wakati hapakuwa na pesa iliyotengwa kwa ajili ya madeni hayo. Hii ni kinyume na kanuni za fedha na bajeti kwa vile Serikali kuu ina tumia sheria za kimataifa za Taasisi za Umma kwa kutumia mfumo taslimu wa malipo.</li> <li>• Uongozi wa Idara ya Jeshi la Polisi haujaandaa sera ya usalama wa mfumo ya TEKNOHAMA.</li> <li>• Idara ya Jeshi la Polisi haijaandaa sera usimamizi wa vihatarishi malimbali vinavyoweza kuhathiri utendaji kazi wake.</li> <li>• Kuwepo kwa madeni makubwa kiasi cha Sh.17,122,418,239 kunakinzana na mfumo taslimu wa kanununi za kimataifa za taasisi za umma (IPSAS). Hali hii ina leta uwezekano kwa Idara kukabiliwa na mashtaka toka kwa wauzaji wa bidhaa na huduma.</li> </ul>

9	<b>Fungu 29: Idara ya Jeshi la Magereza</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Malipo yenye nyaraka pungufu Tshs.80,559,598</b> Wakati wa ukaguzi, tulibainisha malipo ya jumla ya Shs.80,559,598 zilizofanywa kwa walipwaji mbalimbali bila ya nyaraka za kutosha. Kutokana na kukosekana kwa nyaraka sahihi, ukaguzi haukuweza kujiridhisha juu ya usahii wa matumizi haya.</li> </ul>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>kutowasilisha nyaraka za kuhesabu mali Sh.4,590,356,463</b> Kiasi cha shilingi 4,590,356,463 kiliripotiwa katika taarifa za fedha kama vifaa na mali nyingine kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2010. Hata hivyo, nyaraka za kuhesabu mali hizo hazikuwasilishwa ukaguzi.</li> </ul>
10	<b>Fungu 30: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri haina daftari la mali ambalo linaonyesha maelezo ya mali, utambulisho wake, mahali na hali ya mali yenyewe. Mali inaweza kupotea pasipo utawala kuwa na taarifa.</li> </ul> <p>Kiasi cha Shs.40,140,000 kililipwa kama gharama za matengenezo ya vifaa vya elektroniki kwa ajili ya miezi ya Januari-Juni 2010. Hata hivyo, hapakuwa na ushahidi kuonyesha kwamba huduma hiyo kweli ilitolewai.</p>
11	<b>Fungu 32: Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Ununuzi wa vifaa na magari yenye thamani ya Shs.232, 794,959 na Shs.172, 597,534 havikuonyeshwa katika taarifa za fedha.</li> <li>•</li> </ul>

	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Bakaa ya mwanzo wa mwaka ya magari ya Sh. 1768910616 iliyo onyeshwa katika taarifa ya fedha inaonekana kutokuwa sahihi ikilinganishwa na ukweli kwamba magari sabini (70) ambayo hayakuthaminihwa.</li> <li>• Gari lenye usajili Na. STK 501 lenye thamani ya Sh.5, 337,812 liliuzwa katika mwaka husika wa ukaguzi lakini halikufutwa kutoka katika vitabu.</li> <li>•</li> </ul>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Ununuzi wa huduma ya ushauri na kazi za ujenzi yenye thamani ya Shs.220, 000,000 na Sh.7, 703,541,800 hazikuwa na maelezo muhimu. Pia mikataba ya makubaliano, majalada ya miradi na hati za kukamilika kwa miradi husika havikuletwa ukaguzi kwa uhakiki.</li> <li>• Ilibainika kuwa jumla ya Shs.63, 540,000 zililipwa kwa maafisa wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kama posho ya 30% ya nyumba kwa mwezi lakini, pamoja na kiasi hicho kulipwa, jumla ya Shs.111,163,427 zililipwa kwa maafisa hao kwa ajili ya kugharimia samani kinyume na maelekezo No.C/AC.134/213/01/G/69 yanayo taka watumishi wanaolipiliwa samani wawe ni wale wanaoishi katika nyumba za Serikali tu. Kiasi hicho ni kwa ajili ya miaka 4 (kutoka 2006/07 na 2009/10). Kiasi hicho hakijarejeshwa na maafisa husika.</li> <li>• Kinyume na Kanuni ya 54 (4). Na 85. (3) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001 Malipo ya Shs.311,193,971 yilifanywa katika mwaka wa fedha 2009/2010 pamoja na ukweli kwamba malipo hayo yalikuwa nahusu mwaka wa fedha uliopita. Kiasi hicho hakikuorodheshwa kama miadi ya mwaka uliopita.</li> <li>• Kiasi cha jumla ya Shs.45, 059,142 kililipwa kwa walipwaji mbalimbali kwa kutoa huduma kadhaa kwa</li> </ul>

	<p>ofisi, hata hivyo nyaraka husika hazikuwasilishwa kwa ukaguzi.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Kiasi cha Shs.129,346,883 kililipwa kwa M / s Paradise Holiday Resort kwa ajili ya kutoa huduma za hoteli na malazi kwa ajili ya watumishi mbalimbali kutoka Wizara 25. Maelezo kuthibitisha usahihi wa malipo hakuweza kupatikana.</li> </ul>
12	<p><b>Fungu 34: Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa</b></p>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Wizara aliingia katika mkataba na Kampuni ya Fujian Engineering (Group) ya kujenga Julius Nyerere Convention Centre kwa jumla ya Yuan za Kichina 183,500,000. Mkataba husika haukupitiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, kinyume na kifungu cha 55 (b) ya PPA na wala haukusainiwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.</li> <li>• Wizara iliingia gharama ya Shs.120,147,447, kwa ajili ya kutoa mizigo bandarini na uwekaji wa umeme katika Julius Nyerere International Convention Centre pasipokuwa katika bajeti.</li> <li>• Masurufu ya jumla ya Shs.294, 337,785 hayakurejeshwa hadi wakati wa ukaguzi kinyume na matakwa ya kifungu cha 103 (1) cha kanuni za Fedha ya Umma za mwaka 2001 zinazo hitaji masurufu kurejeshwa ndani ya siku kumi na nne baada ya ukamilishaji wa kazi husika.</li> <li>• Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa iliwasilisha taarifa ya dhima kwa kipindi kilicho ishia 30 Juni, 2010 ya Sh.4,518,491,712. Hii inaweza kuathiri utekelezaji wa shughuli za mwaka husika vile vile utaratibu huu unapingana na taslimu wa Viwango vya Kimataifa kwa Taasisi za Umma(IPSAS)</li> </ul>

13	<b>Fungu 38: Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Mfumo wa utunzaji kumbukumbu ni dhaifu kwa vile hati za malipo yenye thamani ya Sh. 9,748,422 hazikuonekana. Uongozi wa jeshi unakabiriwa na vihatarishi vya ubadhilifu.</li> </ul>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Malipo ya jumla ya Shs.89,724,043 kwa ajili ya kulipia waambata wa jeshi nje ya nchi hayakuwa na ushahidi wa mapokezi na jinsi fedha hizo zilivyotumika. Hivyo, kutokana na ukosefu wa ushahidi matumizi hayo, ni vigumu kuthibitisha kama fedha hizo zilitumika kwa matumizi halali.</li> <li>• Fedha za maendeleo kiasi cha Sh. 204,519,726 zilitumika kinyume na malengo ya bajeti husika ya mwaka wa fedha 2009/10.</li> </ul>
14	<b>Fungu 39: Jeshi la Kujenga Taifa</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Jeshi la kujenga Taifa ya halikufuata bajeti ya MTEF kwa vile malipo ya Shs.309, 972,400 yalitumika katika vifungu tofauti vya matumizi bila idhini sahihi wa kufanya uhamisho katika vifungu kinyume na Kanuni. 51 (1-8) ya 2,001 2,004 ya Fedha za Umma.</li> <li>• Taarifa za Fedha za Jeshi la Kujenga Taifa ya mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2010 ilionyesha kuwa JKT ilikuwa na madeni ya jumla ya Sh. 13,740,301,923.39 kati ya hizo Sh. 621,959,913.53 hazikuwa na nyaraka za kuthibitisha usahihi wake. Madeni haya yanaweza kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2010/2011.</li> <li>• Tulilibainisha kuwa matumizi katika baadhi ya vifungu ya Sh. 11,752,617 yalizidi makadirio yaliyopitishwa na hivyo kukiuka misingi ya uthibiti wa malipo ndani ya mfumo wa malipo wa IFMS.</li> </ul>

	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kutokana na kulimbikiza bakaa zisizo sahihi, Jeshi la Kujenga taifa liliripoti mali ya thamani ya Sh. 1113210081 katika mwaka wa fedha 2008/2009 ambayo haikuwa sawa na ile iliyoonyeshwa katika mwaka wa fedha wa 2009/2010.</li> </ul>
15	<b>Fungu 41: Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Gari Toyota Rav 4 4WD lenye thamani ya Shs.70,005,000 na pikipiki-175cc yenye thamani ya Sh.5,598,000 ambavyo vilikuwa havijapokelewa lakini vikaingizwa katika daftari la rasilimali za kudumu kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2010.</li> <li>• Mali zisizohamishika zenye thamani ya Shs.282,152,775 zilizonunuliwa katika kipindi cha mwaka wa fedha tuliokagua hazikuingizwa katika daftari la mali za kudumu.</li> <li>• Hapakuwa na ushahidi wa maandishi kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa na huduma zenye thamani ya Shs.135,770,294 unaoonyesha kwamba taratibu za zabuni zilifuatwa kulingana na Sheria ya Ununuzi ya Umma, ya mwaka 2005 na Kanuni zake.</li> <li>• lita 14,030 za diesel na petrol zenye thamani ya Sh.23 851,000 zilitolewa kwa magari mbalimbali bila kuwa na nyaraka za jinsi matumizi yake yalivyokuwa kama inavyotakiwa na Kanuni. 198 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma 2001 (revised 2004).</li> </ul>

16	16 Fungu 42: Ofisi ya Spika
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Idhini ya ununuzi wa bidhaa na huduma vya thamani ya Shs.536,478,821.60 toka Bodi ya Zabuni ilitolewa baada ya tarehe ya manunuzi.</li> <li>• Manunuzi ya thamani ya Shs.699,598,840 kwa ajili ya mkutano wa CPA hayakuwa katika mpango wa manunuzi. Manunuzi yasiyo na mpango huathiri shughuli zilizopangwa katika mwaka husika.</li> </ul>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Shs.160,085,789.90 zililipwa kwa mkandarasi mkataba kupitia mkataba IE/006/2009-10/HQ/GWND/03 zinazohusiana na utoaji wa huduma za upishi kwa ajili ya kamati za bunge bila ya kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni.</li> <li>• Malipo ya jumla ya Sh.17,971,500 hayakuwa na nyaraka husika kinyume na Kanuni ya. 95 (4) ya Kanuni za Fedha za Umma ya 2001 (iliyorekebishwa 2004).</li> <li>• Ankara kwa ajili ya matengenezo magari ya jumla ya Shs.22,747,227 zililipwa kwa ajili ya mwaka wa fedha 2008/2009 wakati hapakuwa nakumbukumbu na nyaraka za kuonyesha kuwepo kwa madeni katika mwaka husika.</li> <li>• Hati za malipo kwa ajili ya posho zenye jumla ya Shs.30,567,938 hazikuambatana na nyaraka husika.</li> <li>• Masurufu kwa mwaka wa fedha 2009/10 jumla ya Shs.32,393,900 hayakurejeshwa hadi wakati wa ukaguzi kinyume na kanuni ya 103 (1) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001.</li> </ul>

17	<b>Fungu 43: Wizara ya Kilimo na Chakula</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Mishahara isiyolipwa Hazina Shs.86,786,511</b> Kiasi cha jumla ya Shs.86, 786,511 ikiwa ni mishahara isiyolipwa kutokana na sababu mbalimbali hakikurudishwa hazina.</li> </ul>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Kutoa taarifa pungufu ya Mapato halisi Sh.3,652,666</b> Taarifa za fedha zilionyesha mapato kuwa Sh.1,914,200,246.86 wakati mapitio ya vitabu kuhusu fedha zilizopokelewa zilionyesha kuwa kuwa jumla ya mapato ilikuwa Sh.1,917,852,913.68. Hivyo kuna upungufu wa mapato kiasi cha Sh.3,652,666.</li> <li>• <b>Daftari la mali za kudumu halikuandaliwa vema</b> Daftari la mali za kudumu la halionyeshi taarifa muhimu kwa watumiaji wa daftari hilo mfano namba za vifaa na mali nyingine ili kurahisisha shughuli ya uhakiki wa mali.</li> </ul>
18	<b>Fungu 46: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Malipo yaliyofanywa bila nyaraka muhimu Shs.46, 341,491</b> Mapitio ya nyaraka za malipo kwa Idara ya Sera na Mipango, umebaini kuwa malipo ya Shs.46, 341,491 yalifanywa bila nyaraka kamilifu.</li> <li>• <b>Kukosekana kwa taarifa za masurufu ya Sh 518,649,690</b> Taarifa za kifedha kwa kipindi kinachoishia tarehe 30Juni, 2010 ilionyesha kuwa hapakuwa na masurufu mwisho wa mwaka. Hata hivyo, Wizara ilikuwa na masurufu yasiyorejeshwa ya Sh.518,649,690</li> </ul>



	<ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Madai ya Walimu yasiyolipwa Shs.282,543,545.34</b> Taarifa ya madeni sanjari na mali kwa mwaka ulioishia 30Juni, 2010 ilionyesha kuwa kulikuwa na madai ya walimu waliosalia kulipwa kwa kiasi cha Sh. 282,543,545.34 hadi mwisho wa mwaka wa fedha.</li> </ul>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Utoaji wa vifaa maalum kwa ajili ya walemavu Sh.422,999,976.18</b> hatukuweza kuthibitisha kama vifaa vya walemavu vyenye thamani ya Sh.422,999,976.18 vilivyosambazwa viliwafikia walengwana kwa vile taarifa na nyaraka za kupokelea mali(GRNs) hazikuletwa kwa ukaguzi.</li> <li>• <b>Kuchelewa kukamilika kwa ujenzi wa Shule ya Sekondari Miono Bagamoyo</b> Ujenzi wa shule ya Sekondari ya Miono Bagamoyo kwa gharama ya Sh. 4,185,825,273.00 kwa muda wa majuma thelathini na mbili (32) yaani (Machi 4, 2010 - 14 Oktoba 2010) ulikuwa bado kukamilika hadi wakati wa ziara ya ukaguzi ilipofanyika Desemba, 2010.</li> </ul>
<b>19</b>	<b>Fungu 49: Wizara ya Maji</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Wizara ya Maji na Umwagiliaji iliingia mkataba na M / S Nyakirang'ani Construction Limited kwa ajili ya ujenzi wa Bwawa katika kijiji cha Kawa katika Wilaya ya Nkasi kwa jumla ya Sh.1,092,868,644. Kazi ilitarajiwa kukamilika tarehe 2009/05/09 lakini hadi wakati wa ukaguzi Novemba, 2010, mkandarasi alikuwa amelipwa jumla ya Shs.721, 971,009 ingawa kazi ilikuwa haijakamilika.</li> <li>• Mkataba kati ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji na M / S Befra Construction Limited Company ulisainiwa kwa ajili ya ujenzi wa Bwawa katika Kijiji cha Mti Mmoja katika Wilaya ya Monduli wenye jumla ya Shs.695,765,256. Hata hivyo, Nyongeza ya kazi(adendum) No.1 ya Shs.206,592,730.30 haikuwa imeidhinishwa na Bodi ya Zabuni.</li> </ul>

20	<b>Fungu 55: Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora</b>
	<p>Masurufu ya kiasi cha Sh.17,644,786 yalitolewa kwa viongozi wa CHRAGG katika uwezo wa zao rasmi kwa ajili ya gharama za kazi mbalimbali, masurufu haya hayakurejeshwa kinyume na kanuni.103 (1) ya Kanuni za Fedha 2001 (iliyorekebishwa 2004).</p>
21	<b>Fungu 56: Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Ununuzi wa magari ya wagonjwa 43 ambayo hayajathibitika kupokelewa Sh.4,886,045,280 Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI aliingia katika mkataba (ME/022/2009/10/G/13 wa Februari 2010) na Toyota Tanzania Ltd kwa ajili ya kununua magari 43 ya ya wagonjwa kwa ajili ya Halmashauri kwa bei ya Sh. 4886045280. Wakati wa kuandika taarifa hii Januari 2011 magari haya yalikuwa hayajapokelewa.</li> <li>• Malipo yenye nyaraka pungufu Sh.6, 468,499 Jumla ya Sh.6, 468,499 zililipwa bila kuwa nyaraka sahihi kinyume na Kanuni. 95 (4) ya Kanuni za Fedha za Umma 2001 (iliyorekebishwa 2004) ambayo inatamka kwamba vocha ya malipo ambayo ni pungufu kwa sababu ya kukosekana kwa nyaraka itahesabika kama vocha iliyopotea.</li> <li>• Malipo yaliyofanywa katika vifungu vya matumizi (GFS codes) visivyo sahihi Shs.30,313,727</li> </ul>

	<p><b>Ukaguzi wa Miradi chini ya Wizara</b></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Kukosekana kwa taarifa ya utekelezaji juu ya Ujenzi wa Ofisi za Wabunge -Shs.975,660,000</b></li> </ul> <p>Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri iliipa maelekezo TAMISEMI kwa kuangalia majimbo ambayo hayana ofisi za wabunge ili Halmashauri husika ziweze kujenga nyumba hizo. Taarifa ya utekelezaji wa ujenzi huo haikutolewa.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Ununuzi wa magari 10 ambayo hayajapokelewa Shs.611,104,553</b></li> </ul> <p>Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Mradi wa MMES ulipia ununuzi wa magari 10 kwa Sh jumla. 611,104,553 kwa M / s Toyota (T) LTD hadi Januari 2011 magari haya yalikuwa hayaja pokelewa.</p>
22	<p><b>Fungu 57: Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa</b></p>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Ukosefu wa nyaraka za mkataba kwa ajili ya mradi wa Ultimate Building Machine (UBM), Sh.1,353,973,404.</b></li> </ul> <p>Wizara aliingia katika mkataba na Suma - JKT kwa ajili ya ujenzi wa majengo mbalimbali kwa mkataba wa jumla ya Sh.1, 353,973,404 mkataba husika haukupatikana kwa ukaguzi.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Kutoonyesha dhima za fidia Sh.9,000,000,000</b> Kuna amri kutoka Mahakama ya Rufaa ya Tanzania inayoihitaji Wizara kulipa Wanakijiji wa Tondoroni Sh.9, 000,000,000 kama fidia kwa ajili ya ardhi ambayo imechukuliwa na Jeshi.</li> </ul>

23	<b>Fungu 58: Wizara ya Nishati na Madini</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Magari manne yenye usajili STK 2812, STJ 9,710, STK 4,087, STK 745 na STK 740 hayatumiki kwa muda mrefu kwa vile ni mabovu. Hakuna juhudi za kuyatengeneza au kuyauza.</li> <li>• .Wizara ilikuwa na madeni ambayo hayajalipwa ya Shs.100,798,276.33 kutokana na huduma zinazotolewa na wauzaji mbalimbali.</li> <li>• Wizara haikuingiza kumbukumbu za wafanyakazi katika mfumo wa malipo. Jumla ya wafanyakazi 87 hawakuwa na kumbukumbu sahihi ya tarehe ya kustaafu kisi kwamba wafanyakazi wote walionyeshwa kuwa wanastaafu tarehe 01/01/ 1760.</li> <li>• .Mambo ya miaka ya nyuma ambayo hayakushughulikiwa yalifikia Shs.464,148,122.</li> </ul>
24	<b>Fungu 59: Tume ya Kurekebisha Sheria</b>
	<p>Tume ilinunua samani zenye thamani ya Sh13, 695,000 na kutolewa kwa maafisa ambao hawaishi katika nyumba za Serikali kinyume na maelekezo ya utumishi No.C/AC.134/213/01/G/69 ambayo yanahitaji taasisi za Serikali kununua samani kwa maafisa ambao wanaishi katika nyumba za Serikali tu.</p>
25	<b>Fungu 61: Tume ya Taifa ya Uchaguzi</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kuchelewa kufanya malipo yaliyosababisha hasara ya Sh.8,168,359.94 Malipo ya Shs.175,884,243.39 (dola 139,733.37 Exch rate. 1,258.71) yalitakiwa kulipwa katika mwaka wa fedha 2008/2009 badala yake yalilipwa katika mwaka 2009/2010 kwa exch. rate 1,317.17 sawa na Shs.184,052,603.23 kwa M/s WAYWARK InfoTech kwa kusambaza 2x Scamax 412CD Colour Duplex Scanners, na kusababisha hasara ya Sh. 8,168,359.94 kutokana na kiwango cha ubadilishaji kupanda.</li> </ul>

	<ul style="list-style-type: none"> <li>• ufanisi Kamati ya Ukaguzi Kamati ya Ukaguzi hakuwahi kufanya mkutano wowote katika mwaka wa fedha 2009/2010 kinyume na kanuni.32 ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001</li> </ul>
<b>26</b>	<b>Fungu 65: Wizara ya Kazi na Uwezeshaji</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Mkataba wa Kukodisha nyumba uliisha tarehe 24 Aprili 2008 kwa kipindi cha kuanzia 1 Julai 2008 hadi Juni 30, 2010 kukiwa na bakaa ya Shs.179, 263,699.99 kama kodi ya pango, kinyume cha Sheria ya Fedha, 2001, (iliyorekebisha, 2004) na Kanuni ya 53 (1) - (4), ambayo inataka hesabu ziandaliwe kwa mfumo wa pesa taslimu hivyo kuwa na madeni ni kinyume na matakwa ya sheria hiyo.</li> <li>• Hakuna kamati ya uendeshaji ya mifumo ya kompyuta na hivyo kushindwa kuandaa mkakati na sera ya masuala ya mifumo ya kompyuta.</li> </ul>
<b>27</b>	<b>Fungu 66: Tume ya Mipango</b>
	<p>Wakati wa ukaguzi wa mwaka husika, kulikuwa na malipo ya jumla ya Shs.148, 874,469.59 yalilipwa kupitia vifungu visivyo sahihi kinyume na Kanuni No.87 (1) (e) ya Kanuni za Fedha 2001 (zilizorekebisha 2004).</p>
<b>28</b>	<b>Fungu 68: Wizara ya Elimu ya Juu Sayansi na Teknolojia</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Wizara ilifanya uhamisho wa fedha za Maendeleo jumla ya Sh. 1806130000 bila ya idhini ya mlipaji Mkuu wa Serikali na kugharimia mradi ambao haukupitishwa na Bunge.</li> <li>• matumizi ya mwaka huu yalijumuisha malipo yenye nyaraka pungufu ya Sh. 18,615,943 kinyume na Kanuni. 95 (4) ya Kanuni za Fedha za Umma ya 2001 (iliyorekebisha 2004).</li> <li>•</li> </ul>

	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Wizara ililipa posho za samani ya Sh. 18,830,539 kwa maafisa wanaoishi katika nyumba binafsi kinyume na maelekezo ya utumishi C/AC/134/213/01/G/69 ya tarehe 30 Januari, 2006.</li> </ul>
<b>29</b>	<b>Fungu 70: RAS Arusha</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Ukosefu wa sera na mwongozo wa utekelezaji wa masuala ya mazingira. Sekretarieti ya Mkoa haikuandaa taarifa za utendaji</li> <li>• wa maswala ya mazingira kinyume na Kifungu. 36 (1) (e) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, 2004</li> <li>• Sekretarieti ilifungua akaunti ya benki bila ya idhini ya Mlipaji mkuu wa Serikali hivyo kukiuka kanuni. No.15 ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001 (iliyorekebisha 2004).</li> </ul>
<b>30</b>	<b>Fungu 91: Tume ya Kudhibiti Madawa ya kulevya</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Tume haikuwasilisha taarifa ya kina juu ya utendaji wake hivyo hatukuweza kuthibitisha utendaji wa Tume.</li> <li>• Tume ilisaini makubaliano ya msaada na Kituo cha Udhibiti wa Magonjwa cha Marekani, bila bila idhini ya Waziri wa Fedha kama sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya mwaka 1974 (iliyo rekebiswa 2004)</li> <li>• Ununuzi wa samani bila mpango - Sh. 40,748,400</li> </ul>
<b>31</b>	<b>Fungu 98: Wizara ya Maendeleo ya Miundombinu</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Mali za kudumu ambazo hazijaingizwa kwenye daftari Shs.390,410,101,912.77 Taarifa ya Mapato na Matumizi ilibaini kuwa kiasi cha Shs.390,410,101,912.77 kilichohamishwa kwenda taasisi malimbali chini ya Wizara ziliingizwa katika taarifa hiyo kama mali za kudumu za Wizara. Aidha, taarifa ya mali zisizo hamishika hazikuingizwa katika vitabu vya kudumu.</li> </ul>

	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Ununuzi wa tiketi za ndege Shs.15 656,342 Wizara ililipa kiasi cha Sh. 15,636,342 kwa M / S Sykes Travel Agent Ltd kwa ajili ya gharama ya tiketi za ndege kwa ajili ya miaka iliyopita i.e 2005/2006, 2006/2007 na 2007/2008 kinyume na Kanuni. 85 (3) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001.</li> </ul>
32	<b>Fungu 73: RAS Iringa</b> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Pamoja na kwamba katika kipindi cha mwaka wa ukaguzi Sekretarieti ya Mkoa wa Iringa ilikuwa na bajeti ya Shs.87,742,206,575 lakini Sekretarieti ya Iringa ilipokea kiasi cha Shs.89,157,513,885.51 na kusababisha fedha zaidi ya bajeti kupokelewa kiasi cha Sh.1,415,307,310.40</li> <li>• Taarifa ya fedha ilionyesha madeni ya jumla ya Shs.90,455,330. Hata hivyo, orodha ya madeni hayo haikuwasilishwa pamoja na taarifa ya fedha kuthibitisha takwimu iliyotolewa.</li> </ul>
33	<b>Fungu 74: RAS Kigoma</b> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Kulikuwa na matumizi yenye nyaraka pungufu kiasi cha Sh.17,433,100 ikiwa ni pamoja na malipo yaliyofanyika lakini hati zake za malipo hazikuletwa kwa ukaguzi.</li> <li>• Sekretarieti ya Mkoa wa Kigoma haijafuata matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 ndani ya Mkoa.</li> <li>• Sekretarieti ya Mkoa haijaandaa se IT na taratibu, usimamizi wa sera ya a ya mifumo ya kompyuta ikiwa ni pamoja na kuwa na mpango wa kukabiliana na maafa pale yanapotokea.</li> </ul>

	<ul style="list-style-type: none"> <li>Tulibaini kuwa baadhi baadhi ya wafanyakazi katika Sekretarieti ya Mkoa - Kigoma walikuwa wakipokea mishahara chini ya kiwango cha 1 / 3 kutokana na wingi wa makato kinyume na mwongozo no.C/CE.45/271/01/87 wa Utumishi.</li> </ul>
<b>34</b>	<b>Fungu 78: RAS Mbeya</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>Sekretarieti ya Mkoa ililipia gari la wagonjwa kwa ajili ya hospitali ya Mkoa toka Toyota Tanzania Limited jumla ya Sh. 77,047,000 Hata hivyo hadi wakati ripoti hii inaandikwa Februari 2010, gari hili lilikuwa halijaletwa</li> <li>Ujenzi wa nyumba ya makazi ya Mkuu wa Wilaya Chunya iliyogharimu kiasi cha Sh. 82,226,100.00 ulikuwa haujakamilika wakati tunafanya uhakiki.</li> <li>Sekretarieti ya Mkoa ilijenga na kukarabati nyumba zenye thamani ya Shs.180,586,859. Pamoja na nyumba hizi kukamilika, hazijaweza kutumika.</li> <li>Majokofu ambayo yalikuwa yaletwe na kuwekwa katika chumba cha kuhifadha maiti yenye thamani Sh. 98,521,670.05 yalikuwa hayajaletwa na kuwekwa kama ilivyo pangwa.</li> </ul>
<b>35</b>	<b>Fungu 79: RAS Morogoro</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>Sekretarieti ya Mkoa ilikuwa na madeni ya Sh. 430,887,625 kwa ajili ya wauzaji wa bidhaa, huduma na madai ya wafanyakazi. Sekretarieti haina uthibiti katika matumizi kwa vile hata matumizi ya mwaka wa tuliokagua yalizidi bajeti iliyopitishwa na vile izingatie kwamba Serikali kuu inatumia mfumo wa pesa taslim, hivyo kuwa na madeni ni ukiukaji wa kanuni na miongozo inayotumika.</li> </ul>



	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kulikuwa na mapato yazi yokusanywa ya Sh. 47,230,228 kutokana na udhaifu katika kushughulikia mikataba ya huduma ya afya.</li> <li>• Kutokana na mfumo dhaifu wa ndani, jumla ya Sh. 1,975,681.09 zililipwa kwa wastaafu, marehemu na watu walioacha kazi na hivyo kusababisha matumizi batili ya fedha za umma.</li> <li>• Mkoahaukutekeleza mipango ya utunzaji wa mazingira kinyume na matakwa ya kifungu cha 34 cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Namba 20 ya 2004.</li> <li>• Kiasi kilicho salia mwaka wa fedha 2008/09 cha Sh.4,608,052,562 1009/2010. Hata hivyo hatukuweza kujua kwa nini kiasi hiki hakikurejeshwa katika mfuko mkuu wa Serikali.</li> </ul>
36	<b>Fungu 80: RAS Mtwara</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kiasi cha Shs.28, 547,865 kililipwa kwa makandarasi zaidi ya bei ya mkataba. Hii ilikuwa na kukosa udhibiti wa kutosha katika mikataba ya ujenzi.</li> <li>• Sekretarieti ya Mkoa iliingia katika mikataba na makandarasi mbalimbali ya thamani ya Shs.910, 530,765. Tarehe 30 Juni 2010 jumla ya Shs.779,973,097 zilikuwa zimelipwa kwa wakandarasi hao ikiwa ni siku moja baada ya kusaini mikataba. Aidha, hadi 30/11/2010 miradi hii ilikuwa haijakamilika japo fedha zote zilikwisha lipwa.</li> </ul>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• .Kiasi cha Shs.59, 575,000 kiliingizwa katika gharama za mkataba kama fedha za tahadhari na kulipwa bila uthibitisho wa kazi gani ya tahadhari ilifanyika kinyume na kanuni ya 123 (6) ya kanuni za Manunuzi za Umma.</li> </ul>

	<ul style="list-style-type: none"> <li>• .Kulikuwa na udhaifu katika kuidhinisha malipo kiasi kwamba malipo yenye thamani ya Shs.107,326,870. Yalifanyika bila kuwa na nyaraka muhimu.</li> </ul>
<b>37</b>	<b>Fungu 81: RAS Mwanza</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Gharama za kuchelewesha kukamilisha ujenzi wa ofisi kiasi cha Shs.44,772,547 hazikutozwa kwa mkandarasi.</li> <li>• Matumizi ya mishahara ya Sh.3, 025,789,655 kwa mwaka uliomalizika Juni 30, 2010 hayakujumuisha matumizi ya kiasi cha Shs.68,146,508 hali ambayo inaweza kupotosha watumiaji wa taarifa za fedha.</li> <li>• Sekretarieti haikujumuisha katika taarifa za fedha mali zisizohamishika kinyume na Ibara 2.1.33 (a) ya kanuni za viwango vya Kimataifa kwa Sekta ya Umma Accounting (IPSAS).</li> </ul>
<b>38</b>	<b>Fungu 82: RAS Ruvuma</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Bidhaa na huduma za thamani ya Sh. 4,787,900 zililipiwa kutoka akaunti ya matumizi ya kawaida bila kutumia utaratibu wa ushindani wa bei kinyume na Kanuni za Ununuzi wa Umma Namba 68 (4) ya 2004.</li> <li>• malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na huduma mbali mbali ya jumla ya Sh. 11,654,400 yalifanywa bila ya kuwa katika na mpango wa manunuzi kinyume na kifungu 45 cha Sheria ya Ununuzi, 2004.</li> <li>• Malipo ya jumla ya Sh. 23,834,640 yalifanyika bila kuwa na nyaraka muhimu kinyume na Kanuni 95 (4) ya Kanuni za Fedha za Umma.</li> </ul>

	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Malipo ya jumla ya Sh. 10,793,147 yaliyotolewa na Sekretarieti kwa taasisi mbalimbali lakini taasisi hizo hazikukiri mapokezi kinyume kanuni Na. 95 (4) ya Kanuni za Fedha za Umma 2001 (iliyorekebishwa 2004).</li> <li>• Sekretarieti ililipa kiasi cha Sh. 5,820,500 kwa maafisa mbalimbali kama posho za kujikimu nje ya vituo vyao vya kazi. Hata hivyo hapakuwa na ushaidi kama maafisa hawa walipokea fedha hizo kutokana na kukosekana kwa nyaraka za kukiri kupokea.</li> <li>• Sekretarieti ilifanya malipo ya jumla ya Sh.8, 985,000 kwa watumishi mbalimbali bila kuwa katika bajeti kinyume na Kanuni na. 46 ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001.</li> </ul>
39	<b>Fungu 88: RAS Dar es Salaam</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kiasi cha Shs.814,642,900 kulihamishiwa kwenda katika Akaunti ya Amana, lakini kikaonyeshwa kama vifaa vilivyonunuliwa wakati hata orodha ya wazabuni husika hawa kuwekwa katika orodha ya miadi iliyoingiwa na Sekretarieti.</li> <li>• Tarakimu za miaka ya nyuma (yaani 2008/2009) zilizoonyeshwa katika hesabu za Amana na Matumizi ya Kawaida katika mwaka wa fedha 2009/2010 zilitofautiana na taarifa zilizoonyeshwa katika mwaka wa fedha 2008/2009.</li> <li>• Malipo ya fidia kwa waathirika wa mabomu Mbagala kiasi cha Sh.8,050,000,000 hayakuwa na nyaraka muhimu za kuthibitisha kama kweli malipo hayo yalifanyika kwa walemgwa.</li> </ul>

40	<p><b>Ubalozi wa Tanzania New Delhi</b></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Kutowasililisha sifa za uwakilishi kaitika balozi ndogo</b></li> </ul> <p>Ubalozi wa Tanzania New Delhi pia unalo jukumu la kiwakilisha Tanzania katika nchi 4, ambazo ni Bangladeshi, Sri Lanka, Nepal na Singapore.</p> <p>wakati wa ukaguzi huu (Februari, 2011), ubalozi ulikuwa haujawasilisha sifa za uwakilishi katika nchi hizi kwa maelezo kwamba Wizara alikuwa haijaleta taarifa hizo pamoja na kuwa ubalozi umekuwa ukiiumbusha Wizara lakini hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Matatizo kuhusu matengenezo ya mashine ya Visa stickerker</b></li> </ul> <p>Kutokana na ukweli kwamba mzabuni wa mashine za viza sticker ni mmoja tu, imekuwa vigumu kufanya matengenezo ya hii mashine hadi pale mzabuni huyu anayeishi Uholanzi anapopata muda kuja kutendeneza na kwa vile vifaa vya mashine hizi kama vile katriji havina utangamano na mashine nyingine. Kwa hiyo ni gharama kubwa kutumia mashine hizi.</p>
41	<p><b>Ubalozi wa Tanzania -Harare</b></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Hapakuwa na maelekezo wazi juu ya fedha zinazowasilishwa mwisho wa mwaka katika Taarifa za Fedha hivyo kusababisha kiasi cha Sh.7,396,827.10. kutotolewa taarifa. Wizara inatakiwa kutoa maelekezo ya wazi juu ya suala hilo.</li> <li>• Ubalozi ulipokea Sh.9, 942,289.23 chini ya kiwango kilichopelekwa na kutokana na gharama za benki. Hali hii inaweza kuzorosha utendaji kazi wa kazi za ubalozi. Hata hivyo, taarifa hizi hazikuingizwa katika taarifa ya kila mwezi ya benki</li> </ul>

	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kiasi cha \$ 540 (sawa na Shs.744,859.80) kililipwa kwa ajili ya matumizi ya mwaka wa fedha ujao pasipo kuwa katika bajeti</li> </ul>
<b>42</b>	<b>Ubalozi wa Tanzania -Lusaka</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Jumla ya Sh.2, 100,000 zililipwa bila kuwa na nyaraka za kutosha kinyume na Kanuni ya 95 (4) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001 (iliyorekebisha mwaka 2004).</li> <li>• Mkataba wa kupanga nyumba ya makazi kati ya ubalozi na Kampuni ya Intercontinental Relocation ulikatizwa na hivyo kusababisha deni la jumla ya ZK 11,411,071.60 (sawa na Sh.3,080,989.34). Kiasi hiki hakikuingizwa katika taarifa za fedha za mwaka.</li> <li>• Hapakuwa na maelekezo wazi juu ya fedha zinazowasilishwa mwisho wa mwaka katika Taarifa za Fedha hivyo kusababisha kiasi cha Sh. 15,476,733.58. kutotolewa taarifa. Wizara inatakiwa kutoa maelekezo ya wazi juu ya suala hilo.</li> <li>• Ubalozi ulipokea Sh.2,484,938.43 chini ya kiwango kilichopelekwa na kutokana na gharama za benki. Hali hii inaweza kuzorosha utendaji kazi wa kazi za ubalozi. Hata hivyo, taarifa hizi hazikuingizwa katika taarifa ya kila mwezi ya benki</li> </ul>
<b>43</b>	<b>Ubalozi wa Tanzania Abu Dhabi</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Ubalozi haukuwa na udhibiti wa kutosha ili kuhakikisha kuwa mambo ya miaka ya nyuma ya jumla ya TShs.72,150,854 yanafanyiwa kazi.</li> <li>• Ubalozi haukutoa ushahidi wa idhini kutoka Wizara ya mambo ya nje na Ushirikiano wa Kimataifa juu ya matumizi ya ziada ya Sh.865,057,652</li> </ul>

	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Ubalozi haukuandaa taarifa tayari ya ulinganifu wa bajeti na kiasi halisi kwa kuzingatia aya ya 1.9.12 ya Viwango vya kijasibu vya Kimataifa IPSAS.</li> <li>• Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa haijatatua tatizo la kushuka kwa viwango vya fedha za kigeni kwa kupeleka fedha kulingana na sarafu za kigeni ya nchi ambayo Ubalozi wa Tanzania ulipo.</li> <li>• Jumla ya Dh.165, 372 zilihamishwa kutoka katika akaunti ya makusanyo ya mapato ya visa kwenda akaunti ya matumizi ya kawaida bila ya kupata kibali cha Katibu Mkuu kama ilivyoagizwa katika waraka wa Wizara Na. 2 wa 2003/2004 Sehemu A(3)</li> <li>• Ubalozi haukuzingatia matakwa ya sehemu 35 ya Sheria ya ununuzi kwa kuandaa taarifa za manunuzi ya kila mwezi na kuwasilisha kwa MTB kwa ajili ya tathmini ya utendaji kitengo cha manunuzi</li> </ul>
45	<b>Ubalozi wa Tanzania Washington</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Ubalozi wa Tanzania Washington DC ulipokea fedha kwa ajili ya programu ya Mfumo wa kompyuta wa IFMS kiasi cha USD. 19,640.02 tangu mwaka wa fedha 2005/06 na kuziweka katika Akaunti ya Amana. Wakati wa mwaka wa fedha 2006/07 shughuli kadhaa yenye thamani ya dola 11,980 walikuwa kufanyika kwa ajili ya ufungaji wa mfuko huu ndani ya jengo na ofisi ya zamani 2,139 R Street, Hata hivyo, baada ya kuhama katika jengo la zamani Machi 2010 mfumo huu haukuweza kufanya kazi tena kwa vile unahitaji wataalamu wa kuufanyia marekebisho.</li> </ul> <p>Ubalozi kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Hazina wanatakiwa kupata njia bora ya kuhakikisha mfumo huu wa malipo unafanya kazi.</p>

45	<b>Ubalozi wa Tanzania-Addis Ababa</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Wakati wa mwaka wa ukaguzi Ubalozi wa Tanzania-Addis Ababa ulitumia dola 53,533.58 na ETB 38,640 kwa matumizi ambayo hayakuwa katika bajeti ya mwaka husika.</li> <li>• Fedha kiasi cha Sh.17, 223,845.60 (USD 12,892.10) zilizotumwa kwa lengo la kukuza utalii zilitumika kwa ajili ya shughuli za kawaida za Ubalozi.</li> <li>• Ukaguzi ulibainisha tofauti ya dola za Marekani 1,150.41 sawa na sh. 1,602,877.76 kati ya kiasi kilichopelekwa na kile kilichopokelewa na Ubalozi kwa ajili ya mishahara ya watumishi, FSA na matumizi mengine. Ilidaiwa kuwa matumizi haya yalikusiana na gharama za kuhamisha fedha katika benki, hata hivyo matumizi haya hayakuonyeshwa katika vitabu vya hesabu.</li> </ul>
46	<b>Ubalozi wa Tanzania Kuala Lumpur</b>
	<p>Mashine ya Visa Sticker kwa mara ya mwisho ilitumika tarehe 25 Agosti 2010 kutokana na ukosefu wa Cartridges tonner kwa ajili ya printer EPSON. Ilibainika kuwa Cartridges za aina hii ya mashine hazipatikani katika eneo hili la Kusini Mashariki mwa Asia. Ni mtengenezaji wa mashine hizi tu ambaye makao yake yako nchini Uholanzi anaweza kutoa huduma za matengenezo ya pale haja ya inapotokea.</p>
47	<b>Ubalozi wa Tanzania -Saudi Arabia</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Ulitoa taarifa ambazo zinapingana katika Angalizo na. 5 yaa taarifa za fedha kwamba "ubalozi ulifadhiliwa na fedha kutoka hazina ya" wakati Malipo yaliyotolewa na watu wengine yalikuwa ni Sh. 57,820,584.93</li> </ul>

	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Ubalozi haukuandaa taarifa ya kulinganisha bajeti na kiasi halisi ili kuzingatia aya ya 1.9.12 ya Viwango vya uhasibu vya kimataifa- IPSAS.</li> <li>• Taarifa ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2010 ilionyesha fedha zilizohamishwa kuwa Sh.257,453,697 (Angalizo16). Wakati Angalizo na. 18 lilionyesha kuwa fedha zilizohamishwa ilikuwa ni Sh.57,820,585 hivyo habari hizi kutokuwa za kweli.</li> <li>• Ubalozi ulionyesha kuwa mtiririko wa fedha kutoka shughuli za kila siku kuwa Sh.691,168,316 badala ya kiasi sahihi cha Sh. 251,889,552</li> <li>• Ubalozi ulitumia fedha za makusanyo ya maduuli kiasi cha SAR 90,400 kwa shughuli za kawaida bila kuwa na idhini ya Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.</li> </ul>
48	<b>Ubalozi wa Tanzania-Muscat</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Ubalozi ulitumia fedha za makusanyo ya maduuli kiasi cha OMR 68,852,847.80 kwa shughuli za kawaida na OMR 84,947.64 kulipia madeni bila kuwa na idhini ya Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.</li> <li>• Ubalozi haukuandaa taarifa ya kulinganisha bajeti na kiasi halisi ili kuzingatia aya ya 1.9.12 ya Viwango vya uhasibu vya kimataifa- IPSAS.</li> <li>• Ubalozi haukutoa taarifa za mahesabu nyingine zinazoonyesha kuwa makosa ya Tshs.214,993,825 yalirekebisha.</li> <li>•</li> </ul>



	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Hapakuwa na maelezo kuhusu baadhi ya bakaa zilizoonyeshwa katika taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2010 (ukurasa 23) kuonyesha usahihi wa bakaa hizo.</li> <li>• Matumizi ya ziada kama ilivyoonyeshwa katika taarifa ya utendaji ya jumla ya OMR 75,447.64 hayakupata kibali cha Afisa masuuli.</li> </ul>
<b>49</b>	<b>Ubalozi wa Tanzania Lilongwe</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Ubalozi ulinunua vitu vyenye thamani ya Sh.3,557,994 bila kuwa na idhini ya kamati ya manunuzi kama inavyothibitishwa katika mhtasari wa kamati ya manunuzi.</li> <li>• Kulikuwa na manunuzi ya bidhaa yenye thamani ya Sh.6, 071,975, ambayo hayakuidhinishwa na hivyo kuathiri matumizi yaliyopangwa.</li> <li>• Hapakuwa na maelekezo wazi juu ya fedha zinazowasilishwa mwisho wa mwaka katika Taarifa za Fedha hivyo kusababisha kiasi cha Sh. 14,071,746.98. kutotolewa taarifa. Wizara inatakiwa kutoa maelekezo ya wazi juu ya suala hilo.</li> <li>• Ubalozi ulipokea Sh.10,599,712.99 chini ya kiwango kilichopelekwa na kutokana na gharama za benki. Hali hii inaweza kuzorosha utendaji kazi wa kazi za ubalozi. Hata hivyo, taarifa hizi hazikuingizwa katika taarifa ya kila mwezi ya benki</li> </ul>
<b>50</b>	<b>Ubalozi wa Tanzania -Abuja</b>
	Ubalozi ulihamisha fedha za makusanyo ya maduuli kiasi cha TShs.179,500,844 kwenda katika akaunti ya matumizi ya kawaida bila kuwa na idhini ya Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

51	<b>Ubalozi wa Tanzania -Kinshansa</b>
	<p>Ubalozi ulihamisha fedha za makusanyo ya maduuli kiasi cha Shs.34,667,555 kwenda katika akaunti ya matumizi ya kawaida bila kuwa na idhini ya Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.</p> <p>Ubalozi ulifanya matumizi zaidi ya kiasi kilichopitishwa na bunge kwa kiasi cha Shs.188,370,697 na kutumia Shs. 177,079,048 zaidi ya kiasi kilichopelekwa bila kuwa na idhini ya Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.</p>
52	<b>Ubalozi wa Tanzania -London</b>
	<p>Ubalozi ulifanya matumizi zaidi ya kiasi kilichopitishwa na bunge kwa kiasi cha Shs. Shs.832,815,497 bila kuwa na idhini ya Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.</p>
53	<b>Ubalozi wa Tanzania-Moscow</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Ubalozi haukuwa na udhibiti wa kutosha ili kuhakikisha kuwa mambo ya miaka ya nyuma ya jumla ya Sh. 451,378,015.00 yanafanyiwa kazi.</li> <li>• Ubalozi ulifanya matumizi zaidi ya kiasi kilichopitishwa na bunge kwa kiasi cha Sh.533,129,381.00 bila kuwa na idhini ya Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.</li> </ul>
54	<b>Ubalozi wa Tanzania-Stockholm</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Ubalozi ulifanya matumizi zaidi ya kiasi kilichopitishwa na bunge kwa kiasi cha Shs. Sh.117,891,747.90. bila kuwa na idhini ya Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.</li> <li>• Ubalozi ulilipa jumla ya SEK 655,885 sawa na TShs.151,845,727.10 kwa ajili ya kuvunja mkataba wa nyumba. Haya ni malipo batili ya fedha za umma.</li> </ul>

	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Tarehe 30 Juni, 2009, Ubalozi ulikuwa na Madeni ya jumla ya SEK 1,772,728.96 ambayo ni sawa na shilingi 369,701,397.12. Hata hivyo wakati wa kuandika taarifa hii malimbikizo ya jumla ya TShs.129, 137,082.72 yalilipwa hivyo kuacha madeni ya Shilingi 240,564,314.40 madeni haya ya muda mrefu yanaweza kuathiri sifa nzuri ya Ubalozi na hata kusababisha Ubalozi kushtakiwa.</li> </ul>
55	<b>Ubalozi wa Tanzania-Kigali</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Ukaguzi ulibainisha kuwa Ubalozi ulipelekewa Shs.78,258,616.56 zaidi ya makadirio ya mwaka yaliyopitishwa na Bunge.</li> <li>• Ubalozi ulirejesha kiasi cha USD 24,266.00 HOM kwa ajili ya fedha alizotumia kutoka mfukoni mwake kama posho ya kujikimu wakati wa kusafiri katika nchi za Afrika Mashariki na kuhudhuria mikutano mbalimbali. Ukaguzi alibainisha Malipo ya dola za Kimarekani 10,324.00 yaliyolipwa yalitofautiana na idadi ya siku za mikutano iliyofanyika kwa kuzingatia barua za mwaliko kutoka Wizarani.</li> <li>• Wakati wa ukaguzi, tuligundua kuwa nyumba Na. 772 iliyoko mtaa wa Kacyiru ilichukua zaidi ya miezi 7 bila kukaliwa na Ubalozi uliendelea kulipia kodi ya nyumba na mishahara ya walinzi wakati nyumba haitumiki.</li> <li>• Tathmini ya masuala ya utawala na wafanyakazi iligundua kuwa nafasi ya HOC na katibu mhutasi ziko wazi kwa muda mrefu na hivyo kufanya masuala ya utawala katika ubalozi yasifanyike ipasavyo.</li> </ul>

56	<b>Ubalozi wa Tanzania -Nairobi</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Ubalozi ulifanya matumizi zaidi ya kiasi kilichopitishwa na bunge kwa kiasi cha Sh.17, 702,332 bila kuwa na idhini ya Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.</li> <li>• ukaguzi wa nyumba no.81 iliyoko eneo la Muthaiga ulionyesha kwamba nyumba iko katika hali mbaya kwa vile haijafanyiwa matengenezo ya kutosha na ina samani za zamani. Ubalozi uliomba fedha kwa ajili ya ukarabati kwa barua MFAIC na Kumb no. TZN/A.10/1 "D" / 12 hata hivyo hakuna majibu yaliyopokelewa toka Wizarani.</li> <li>• Serikali ya Kenya iliupatia ubalozi kiwanja na. LR 209/13678 eneo la Upper Hill, Nairobi zaidi ya kumi iliyopita kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ubalozi na makazi ya balozi na watumishi wengine.</li> </ul> <p>Kulingana na barua kumb. Na. AB 2/320/01/19 kutoka Wizara ya Mambo ya Nje kwenda Hazina, NSSF iko tayari kuendeleza ujenzi huo baada ya kupata dhamana ya Serikali. Hadi sasa Serikali bado haijatao dhamana kwa NSSF, bila ya mpango wa haraka, Serikali ya Kenya inaweza kubatilisha utoaji huo wa kiwanja.</p>
57	<b>Ubalozi wa Tanzania Paris</b>
	<p>Ubalozi haukuwa na udhibiti wa kutosha ili kuhakikisha kuwa mambo ya ukaguzi ya miaka ya nyuma yanafanyiwa kazi inavyotakiwa.</p>

58	Ubalozi wa Tanzania-Roma
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Ubalozi wa ulipokea mashine ya visa sticker kutoka Wizara ya Fedha na Uchumi, kwa madhumuni ya kuipeleka katika ubalozi mdogo wa Milan. Hadi wakati wa ukaguzi Machine hiyo ilikuwa bado katika Ubalozi.</li> <li>• Wakati wa ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Ubalozi, tuligundua kwamba kiasi cha TShs.270, 000,000 kilipokelewa na ubalozi kama mchango wa Wizara ya Kilimo na Ushirika. Vile vile tulibauini kwamba Ubalozi umekuwa ukipokea michango na kuiweka katika Akaunti ya Kilimo ambayo inasimamiwa na Mwakilishi wa Kudumu wa FAO. Hata hivyo hatukupewa miongozo ya jinsi ya mfuko huu unavyoendeshwa na majukumu ya Ubalozi juu ya usimamizi wa akaunti hii.</li> <li>• Ukaguzi wa hati za malipo na nyaraka nyingine ulibaini kuwa Ubalozi hakulipa kiasi cha Euro 257,811,809, sawa na TShs.434,441,257.46 ikiwa ni 8.89% na 30% makato ya kila mwezi kwa michango ya pensheni kwa ajili ya wafanyakazi wa ubalozi wenyeji wa nchi hiyo.kama michango ya mwajiri kwenda katika mfuko husika wa hifadhi ya jamii (INSP) pamoja na INPS kuuandikia ubalozi barua ya kuwakumbushia kulwasilisha makato hayo.</li> <li>• Kwa miaka mingi Ubalozi umekuwa ukiwalipa wafanyakazi wakazi wa nchi hiyo mishahara chini yakiwango kilichopitishwa na Serikali ya Italia kulingana na sheria za kazi, ambayo inamtaka mwajiri kulipa nyongeza kila baada ya miaka kinyume chake mwajiri anaweza kutozwa faini.</li> </ul>

59	<b>Ubalozi wa Tanzania-Beijing</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2010, Ubalozi ilitumia kiasi cha shilingi 1,284,034,623 dhidi ya bajeti iliyoidhinishwa ya TZS 1,074,423,600 na hivyo kusababisha matumizi ya ziada ya shilingi 209,611,023.</li> <li>• Ukosefu wa mawasiliano ya kutosha kati ya Ubalozi, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Wizara na sekta mbali mbali kumesababisha kuchelewa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya inayofadhiliwa na Serikali ya China.</li> </ul>
60	<b>Ubalozi wa Tanzania-Tokyo</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Ubalozi ilitumia kiasi cha shilingi 282, 738,520. zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa ba bunge bila kuwa na kibali.</li> <li>• Kuna umuhimu wa kupeleka mashine za visa sticker katika balozi ndogo za Melbourne, Seoul, Osaka na Perth kwa ajili ya udhibiti mzuri wa makusanyo ya visa.</li> </ul>

**7.8 Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa zilizopewa hati yenye shaka pamoja na sababu za maoni hayo.**

1	<b>Fungu 18: Mahakama Kuu ya Tanzania</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Mahakama ilifanya malipoya Sh. 825,240,000 ambayo hayakuwa na nyaraka timilifu kinyume na Kanuni. 95 (4) ya Kanuni za Fedha za Umma ya 2001.</li> </ul>

	<ul style="list-style-type: none"> <li>Taratibu za manunuzi hazikufuatwa kwa vile bidhaa zilinunuliwa bila idhini ya Bodi ya Zabuni. Aidha, kumbukumbu za stoo hazikuwekwa vizuri kiasi kwamba bidhaa zenye thamani ya Sh.270,248,424 hazikujulikana jinsi zilivyo tumika.</li> </ul>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>Malipo ya Sh. 14,181,854.60 yanayohusiana na miaka ya 2001 hadi 2006/07 ililipwa katika bajeti ya 2009/10 bila kibali cha nyongeza ya bajeti.</li> <li>Kuna udhaifu katika usimamizi wa mikataba hadi kusababisha malipo batili ya Sh. 34,439,536.10. Kiasi hiki hakikupangwa kulipwa katika bajeti ya 2009/10</li> <li>Udhibiti mifumo ni dhaifu kutokana na utendaji duni wa Kitengo cha ukaguzi wa ndani, Kamati ya Ukaguzi na Kitengo cha Manunuzi.</li> </ul>
<b>2</b>	<b>Fungu 21: Hazina</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li><b>Malipo ya madeni ya polisi ambayo hayakuhakikiwa Shs.600,000,000</b> Malipo ya Shs.600,000,000 ikiwa sehemu ya deni la Sh.1,284,359,467 linalodaiwa na Mkemia Mkuu wa Serikali kwa ajili ya huduma za maabara kwa ajili ya kuhakiki vielelezo toka Jeshi la Polisi kwa ajili ya uchunguzi. Hata hivyo, madai haya hayakupitishwa na wizara ya mambo ya Ndani wa kuhakikiwa kabla ya kulipwa.</li> <li><b>Mali, Mitambo na Vifaa kuonyeshwa pungufu Shs.117,676,890</b> Mapitio ya orodha ya Mali, Mitambo na Vifaa yalionyesha kwamba tarehe 1 Julai, 2009 haikujumuisha Mali, Mitambo na Vifaa vyenye thamani ya Shs.117,676,890 vilivyohamishwa kutoka fungu 50</li> </ul>

	<ul style="list-style-type: none"> <li> <p>• <b>Mali, mitambo na vifaa vyenye nyaraka pungufu Sh.3,329,757,580</b>  Taarifa ya Mali, mitambo na vifaa yenye thamani ya Sh.3,329,757,579.67 (Ardhi &amp; Sh.2,216,027,580, magari Shs.902, 730,000 na mali turathi Shs.211,000,000) hazikuwa na taarifa au nyaraka kama vile hati miliki ya ardhi, hati za umiliki wa magari, eneo mali ilipo na thamani ya mali.</p> </li> <li> <p>• <b>Fidia na kichocheo kwa makampuni ya liyopata hasara Shs.48,000,270,000</b>  Jumla ya Shs.48,000,270,000 zililipwa kwa Benki Kuu ya Tanzania kama sehemu ya mpango wa Serikali kuanzisha mfuko wa kichocheo ili kusaidia wafanyabiashara walioathirika na mtikisiko wa hali ya kiuchumi duniani. Hatukupewa orodha ya watu ambao walifaidika kutokana na fedha hizo katika kufidiwa hasara ikiwa ni pamoja na taratibu zinazohusiana na jinsi fedha hizo zilivyotumika.</p> </li> <li> <p>• <b>Malipo kwa kampuni ya Makaa ya Mawe Kiwira Kutohakikiwa Sh.2,000,000,000</b>  Kiasi cha Sh. 2,000,000,000 zililipwa kwa Kiwira Coal Mines Ltd kwa ajili ya mishahara ya wafanyakazi bila madeni hayo kuhakikiwa. Sikupata ushahidi kwamba malipo haya yalikuwa halali kutoka katika mfuko mkuu wa Serikali.</p> </li> <li> <p>• <b>Kukosekana kwa nyaraka kuhalalisha matumizi ya mafunzo Shs.150,611,256</b>  Malipo ya Sh.322,706,278 yalifanywa kwa wafanyakazi mbalimbali kwa ajili ya posho za kujikimu na gharama nyingine ili kuhudhuria mafunzo mbali mbali. Hata hivyo, hati ya mahudhurio hazikuletwa kwa uhakiki kinyume na mwongozo wa Serikali No.1 ya 2009.</p> </li> </ul>
--	---



	<ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Kukosekana kwa nyaraka za kuhamisha fedha Sh.626,254,082</b> Wizara alifanya uhamisho wa Shs. 626,254,082 kwenda A / C Na. 01103031108 ya Usimamizi wa Maendeleo NBC Ltd kwa ajili ya Mradi wa Mpango Mkuu wa Kupambana na Umaskini. Hatukupata taarifa muhimu zinazohusu uendeshaji wa akaunti hii ya benki ikiwa ni pamoja na majina ya waweka saini, statement ya benki ili kuhalalisha uendeshaji wake.</li> <li>• <b>Masurufu ambayo bado kurejeshwa Shs.179,743,537</b> Masurufu ya Sh.359,490,363 yalitolewa katika kipindi cha mwaka wa ukaguzi, hata hivyo hayakurejeshwa baada ya kukamilika kwa shughuli iliyokusudiwa, pia, baadhi ya maafisa walipewa masurufu kabla ya kurejesha yale ya awali kinyume na Kanuni. 103 (1) na 103 (7) za Kanuni za Fedha za Umma, 2001(iliyorekebishwa 2004).</li> <li>• <b>Ununuzi toka kwa mzabuni mmoja Shs.61, 625,000</b> Malipo ya TShs.61,625,000 yalifanywa kwa M/s Mkuki na Nyota Publishers kwa ajili ya madai ya kuchapisha nakala 3,000 za Kiswahili kwa ajili ya vitabu vya MKUKUTA II na nakala 2,000 za Kiingereza toka kwa mzabuni mmoja. Hapakuwa na ushahidi kuwa bidhaa hizi zilikuwa za dharura.</li> <li>• <b>Ukosefu wa udhibiti wa dhamana za mikopo ya kusafirisha bidhaa nje ya nchi.</b> Taarifa ya Dhamana ya Mikopo ya kusafirisha bidhaa nje ya nchi (ECG) ilionyesha kwamba katika 2009/2010 dhamana hizi zimeongezeka kwa Sh.16,112,318,198.75 kutoka TShs.181,725,850,003.72 ile ya mwaka 2008/2009 ya TShs.197,838,168,202.47 sawa na 8.9%. Hazina haijaonyesha ufuatiliaji ili kuhakikisha wkopaji wote wanarejesha mikopo yao, pia dhamana za TShs.59,308,729,997 ambazo</li> </ul>
--	---

	wakopaji wameshindwa kulipa bado wanaonekana kama dhamana hazijaisha muda wake katika vitabu vya Msajili wa Hazina.
<b>3</b>	<b>Fungu 33: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Katika ukaguzi wetu tulibaini kuwa Sh.64,283,000 zilizokusanywa hazikupelekwa benki. Hivyo, makusanyo hayo hayakuweza kuhakikiwa.</li> <li>• Jumla ya Sh.11,870,000 zililipwa kwa watu mbalimbali bila kuwa na nyaraka timilifu.</li> </ul>
<b>4</b>	<b>Fungu 40: Mahakama (Mahakama ya Ruffaa)</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Malipo yenye nyaraka pungufu Shs.213,170,352.60</b> Nyaraka kama vile mikataba, hati za kukamilika kwa kazi, mchanganuo wa matumizi kwa ajili ya malipo kwa wauzaji mbalimbali wa bidhaa na huduma hazikuletwa kwa uhakiki.</li> <li>• <b>Matumizi yanayoonekana kuwa hewa Shs.87,749,856.80</b> Mahakama ililipa gharama za hoteli kutoa nakala kwa ajili ya mafunzo. Hapakuwa na nyaraka za kutosha kuthibitisha uhalali wa malipo haya na kama kweli huduma hii ilitolewa.</li> <li>• <b>Uhamisho wa fedha kwenda Akaunti ya Amana Shs.71,926,400</b> Kiasi cha Sh.71,926,400 kiliamishiwa Akaunti ya Amana kwa ajili ya kufanya uchambuzi wa ADR Tanzania na kuendesha mafunzo ya wakufunzi. Hapakuwa na ushahidi kuonyesha kuwa shughuli hiyo ilikamilika kutokana na kukosekana kwa maelezo ya matumizi na taarifa ya kazi hiyo.</li> </ul>

	<ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Bidhaa zilizolipiwa lakini hazikuletwa Shs.204,833,667</b> vifaa vya kompyuta kwa ajili ya utoaji wa taarifa ya Sheria za Tanzania kutoka 1999 - 2006 na ununuzi wa Sheria za Tanzania 1998 kwa Shs.204,833,667 havikuthibitika kupokelewa.</li> <li>• <b>Matumizi yasiyo sahihi Shs.179,908,331</b> Matumizi ya jumla ya Shs.179, 908,331 zinazohusiana na ununuzi wa bidhaa na huduma zililipwa toka Akaunti ya Amana. Hata hivyo, tulibaini kuwa kulikuwa na mapungufu kadhaa katika malipo hayo kama inavyoonekana hapa chini: <ul style="list-style-type: none"> <li>i. Hapakuwa na ushahidi kuwa fedha hizo zilihamishiwa kwenye akaunti ya amana kwa ajili ya matumizi hayo kwa vile hapakuwa na kibali cha kufanya malipo hayo.</li> <li>ii. Hapakuwa na orodha ya madeni ambayo yalikuwa hayajalipwa au ahadi ili kuhalalisha kuwepo kwake mwisho wa mwaka.</li> <li>iii. Hapakuwa na kibali cha Afisa Masuuli kuidhinisha matumizi hayo.</li> <li>iv. Hapakuwa na idhini ya Bodi ya Zabuni kwa ajili ya matumizi ya fedha hizo.</li> </ul> </li> <li>• <b>Kukosekana kwa hati za malipo ya Sh. 150,796,566.00</b> Malipo kiasi cha Sh. 150,796,566.00 yalifanywa kwa watu na wazabuni mbalimbali, lakini hati husika za malipo hazikuletwa kwa ukaguzi.</li> </ul>
<b>5</b>	<b>Fungu 44: Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Bakaa ya mwanzo wa mwaka 1 Julai, 2009/10</b> ilikuwa Shs.240, 252,390 wakati hapakuwa na bakaa ya kufunga mwaka uliomalizika Juni 30, 2009. Tofauti hii bado haijasuluhishwa.</li> </ul>

	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kulikuwa na makosa katika uingizaji wa takwimu katika mfumo wa kompyuta na kuonyesha vifungu vya matumizi visivyo sahihi, ambapo mfano, posho ya mafunzo jumla ya Shs.164, 463,996 na posho za huduma jumla ya Shs.99, 500,000 ziliandikwa kama wazabuni na vifaa vinavyotumika.</li> <li>• Kulikuwa na kuzuiwa kwa wigo wa ukaguzi ambapo madeni ya thamani ya Shs.201, 013,253.80 hayakuwa na hati zinazo tosheleza. Wizara. Aidha bakaa ya mwanzo wa mwaka 1 Julai, 2009/10 ya madeni ilikuwa Sh. 788,788,822.80 wakati bakaa ya kufunga mwaka uliomalizika Juni 30, 2009 ilikuwa Shs.699, 289,208.00. Kimsingi takwimu hizi zilipaswa kuwa sawa. Tofauti hii bado haijasuluhishwa</li> <li>• Shughuli tatu zinazohusiana na uandaaji na utekelezaji wa Mkakati wa Maendeleo ya Viwanda na mpango wa Mkuu wa Mahakama ya Ushindani na kuhakikisha utendaji bora wa FTC zilikuwa na mafanikio ya kati ya 14% na 32%. Mwenendo huu usipoangaliwa unaweza kuzuia mafanikio ya malengo ya Wizara.</li> <li>• Tulibaini udhaifu wa udhibiti wa ndani juu ya usimamizi wa masurufu yasiyorejeshwa ambapo jumla ya Shs.25, 149,420 zilikuwa bado kurejeshwa wakati wa ukaguzi wetu.</li> </ul>
6	<b>Fungu 48: Wizara ya Ardhi na Makazi</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Taarifa za kifedha kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni, 2010 zilionyesha kuwa kulikuwa na mali na vifaa vyenye thamani ya Shs.907,872,442, hata hivyo, Vifaa vyenye thamani ya Shs.534,380,697 havikujumuishwa katika taarifa na mali na vifaa.</li> <li>• Jumla ya lita 72,836.8 za mafuta yenye thamani ya</li> </ul>

	<p>Shs.96,508,780 zilinunuliwa kutoka wakala wa Huduma za Ununuzi hazikuingizwa katika vitabu vya mafuta kinyume na Kanuni Na. 203 (1) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001 iliyorekebisha 2004.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Mapato yaliyokusanywa katika kituo cha Mwanza kati 12/10 /2009 na 31/12/2009 na kupelekwa benki tawi la NMB-Mwanza kupitia Retention Scheme Akaunti ya Mapato Akaunti na. CA 3111000007 ziliwekwa katika akaunti husika bila ya kuwa na nyaraka muhimu.</li> <li>• Malipo ya mishahara ya Sh 26,020,151.77 zililipwa kwa wastaafu mfanyakazi, marehemu na wafanyakazi waliofukuzwa kazi au kuscishwa ambao majina yao hayakufutwa kutoka katika orodha ya mishahara</li> <li>• mali yenye thamani ya Sh. 371,824,437 haikuingizwa katika daftari la mali za kudumu.</li> <li>• mali zilizonunuliwa katika kipindi cha mwaka husika zenye thamani ya Sh.1,146,390,436 zilijumuisha malipo ya Shs.360,000,000 ikiwa ni fidia ya ardhi No.17 Rushungi - Kilwa.</li> <li>• Mshauri kwa ajili ya ukarabati wa majengo chini ya Sekta Binafsi Competitive Project (PSCP) aliomba ada ya ushauri ya ziada ya Shs.47,979,406 kwa muda ulioongezeka toka Mei 2010 hadi Julai 2010 kutokana na kuchelewa kumaliza kazi.</li> <li>• Kiasi cha Sh.2,650,388,463 kilikopwa kutoka mfuko wa mradi wa viwanja 20,000 na Halmashauri saba. wakati wa ukaguzi kiasi hiki kilikuwa bado kulipwa. Baadhi ya Halmashauri hizo zimeshindwa kulipa hata nusu ya kiasi walichokopeshwa.</li> <li>• Manispaa za Ilala na Kinondoni zilikuwa na maeneo 157 ya wazi ambayo yalivamiwa na baadhi ya watu na</li> </ul>
--	---

	<p>kujenga nyumba katika maeneo hayo bila kibali kutoka Wizara ya Ardhi na maendeleo ya makazi, kinyume na kifungu 28 (f), 29, 30, 31, 32 na 33 ya Mipango Miji Sheria ya 2007 8. Pia ilibainika kuwa nafasi 69 za wazi zilichukuliwa na wavamizi bila hati yoyote ya kisheria na vingine 20 vimepewa hati ya kumiliki (CT).</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Bodi ya Mfuko wa Mikopo ya Makazi ipitisha mikopo ya jumla ya Sh.2, 148,502,144 ili kutolewa kwa watumishi 273 wa umma ambao waliomba mkopo, lakini hadi wakati wa ukaguzi, hakuna mikopo iliyokuwa imetolewa kwa wakopaji.</li> <li>• Wizara ni msimamizi mkuu wa sera za nchi na sheria kama vile Sheria ya Ardhi ya vijiji ya 1999 no.5 na sheria ya Ardhi No.4. Wizara ilitakiwa kutekeleza ya 5 ya kilimo Kwanza lakini shughuli zilizopangwa kutekelezwa hazikutekelezwa.</li> </ul>
7	<p><b>Fungu 50: Wizara ya Fedha</b></p>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Fidia kufanywa kwa wadai wasiostahili Shs.964, 188,492</b> Jumla ya Shs.964,188,492 ikiwa ni riba ya Shs.334,188,492 na gharama za usumbufu za Shs.500,000,000 zililipwa kwa Saddiq Super Service Station (SSSS) ya SLP 1762 Morogoro kama fidia kwa ajili ya kufutwa kwa zabuni ya kununua kampuni kutoka PSRC mali iliyokuwa ikimilikiwa na Tanzania Motor Services Company.</li> </ul> <p>Pia kiasi cha Sh.3,000,000,000 ikiwa sehemu ya madai ya Sh.7,500,000,000 yalifanywa kwa M / s Twiga Chemical Industry Ltd (TCI) kama fidia ya hasara ya biashara, na kwa ajili ya kufuta umiliki wa shamba Na. 17/18 katika eneo la Kimara Baruti. Hata hivyo, TCI hawakustahili kupata malipo ya fidia kwa sababu hati yao ya kufanya biashara ilikuwa tayari imefutwa na</p>

Kamishna wa Madini, na kwa mujibu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi barua kumb Na. CBD.70/264/01 ya tarehe 2 Machi 2005 TCI alikuwa anamiliki ardhi kama mpangaji baada ya kumalizika kwa hati yake ya kufanya biashara. Aidha, Kamati ya Usimamizi wa Deni la Taifa (NDMC) ilikataa madai juu ya ardhi katika mkutano wake uliofanyika tarehe 13 Januari 2006.

- **Malipo ya fidia isiyostahili kwa kampuni ya TANGO Limited Sh.554,464,133**

Kiasi cha Shs.554,464,133.60 kililipwa kwa M/S Tango Transport Limited (Verani Tango) kama fidia kwa mujibu wa hati za Magari yake zilizodaiwa kuchukuliwa na maafisa wa TRA mwaka 1997 kwa muda wa siku tisini (90). Hata hivyo, mapungufu yafuatayo yalibainishwa:

i. Mrejesho ya Shs.53,650,151 yaliambatanishwa na hati ya kukiri mapokezi ambayo uhalisi wake haukuthibitishwa. Aidha, kiasi hiki kililipwa mara mbili, wakati awamu ya kwanza malipo yalifanywa kwa amri ya mahakama.

ii. Malipo ya Sh.6,788,840 hayakuhusiana na madai ya msingi

iii. Malipo ya riba ya Shs.554,464,133.60 yalifanyika kwa 'compound interest' badala "simple interest".

#### **Taarifa ya Uwekezaji ya Msajili wa Hazina**

Mapitio ya taarifa ya uwekezaji ya **Msajili wa Hazina** yalibaini kuwa msajili wa hazina hakuwa na kumbukumbu sahihi juu ya hisa za Serikali katika mashirika ya umma yafuatayo:

- Benki ya Rasilimali(TIB)
- Tanzania Breweries
- Soko la Kariakoo
- Aluminium Afrika

• **Malipo ya kifuta jasho Sh.10,239,516,520**  
Jumla ya Sh.10,239,516,520 zililipwa kwa NMB Ltd kwa ajli ya kuwalipa kifuta jasho watumishi wake ambao walifanya kazi katika NBC wakati ikiwa chini ya Serikali. Tulibaini kuwa malipo haya hayakuwa halali na yalilipwa zaidi ya kiwango ambacho watumishi hao walistahili kupata kisheria. Malipo haya yalifanyika kutokana na msukumo wa vyama vya wafanyakazi bila kuzingatia taratibu za ajira na haki ya watumishi hao. Utaratibu huu unaweza kuigharimu Serikali kama Serikali haitakuwa makini kushughulikia maswala kama haya.

• **Malipo ya Shs.70, 000,000,000 kwa Benki ya Rasilimali (TIB)**

Wizara iliamisha kiasi ya Shs.70, 000,000,000 kwa kipindi kilichoishia Juni 30, 2010 kwenda TIB kwa ajili ya kubadilisha TIB kuwa taasisi ya Maendeleo ya Fedha na pia kufungua benki kwa ajili ya shughuli za kilimo. Tuliomba taarifa zifuatazo ambazo hadi tunaandika taarifa hii tulikura hatujapewa nyaraka hizo:

(I) taarifa ya akaunti ya benki kwa kipindi kilichoishia Juni 2010.

(ii) dondoo za ripoti ya fedha kuonyesha mapokezi yote, malipo na urari wa mfuko huo.

(iii) hatua zilizochukuliwa ili kuzuia uwezekano wa mfuko huo kuanguka kutokana na ukweli kuwa mkataba hauwabani TIB kuwajibika waliochukua mikopo wanaposhindwa kulipa.

(iv) Kibali cha baraza la mawaziri kuanziasha taasisi hizi mbili



	<p>backlog ya masuala bora Wizara haina uthibiti wa kama inavyoonyesha hapa chini:</p> <table border="1" data-bbox="501 302 1334 457"> <thead> <tr> <th>Mwaka</th> <th>Kiasi (Sh)</th> </tr> </thead> <tbody> <tr> <td>2004/2005</td> <td>8,000,000,000</td> </tr> <tr> <td>2006/2007</td> <td>257,217,954,621</td> </tr> <tr> <td>2008/2009</td> <td>114,634,665,123</td> </tr> </tbody> </table> <p>Kulikuwa na madeni yanayo tokana na dhamana za Serikali ambayo hayakingizwa vitabuni Shs.445, 791,155,000</p>	Mwaka	Kiasi (Sh)	2004/2005	8,000,000,000	2006/2007	257,217,954,621	2008/2009	114,634,665,123
Mwaka	Kiasi (Sh)								
2004/2005	8,000,000,000								
2006/2007	257,217,954,621								
2008/2009	114,634,665,123								
8	<p><b>Fungu 51: Wizara ya Mambo ya Ndani</b></p> <p>Bakaa za akaunti ya Amana Sh.2,704,050,959 hazikuwa na maelezo  Malipo ya Shs.423,183,545 yalifanywa kwa watu wengine, lakini hayakuonyeshwa katika vitabu vya fedha kinyume na viwango vya kimataifa vya uhasibu (IPSAS).  Madeni ya thamani ya Shs.230,605,439 hayakingizwa katika taarifa za fedha.</p> <p>Kulikuwa na udhaifu katika usimamizi wa mikataba vilevile nyaraka muhimu za mikataba hazikuletwa kwa uhakiki.</p> <p>Wizara haikuandaa taarifa ya Utendaji kulingana na waraka Na. 1 na Kanuni.8 (5) ya Kanuni za Fedha za Umma.</p>								
9	<p><b>Fungu 52 Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii</b></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Matumizi katika vifungu/kasima visivyo sahihi Sh.3,894,809,822</b>  Jumla ya malipo ya kiasi cha sh. 3,894,809,822 yalilipwa kwenye kasima isiyo sahihi na kusababisha kutopangwa katika kasima ya matumizi iliyopitishwa na Bunge</li> <li>• <b>Matumizi yenye nyaraka pungufu Sh.597,967,673</b>  Kulikuwa na malipo ya kiasi cha Sh.597,967,673 yaliyofanyika bila kuwa na nyaraka kinyume na kanuni na 95(4) ya sheria ya fedha ya Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebisha mwaka 2004) na kufanya malipo hayo yasiwe na uhalali.</li> </ul>								

- **Uhamisho wa fedha kiasi cha sh.5,051,875,931 usiokuwa na kibali cha Hazina**

Wizara iliamisha kiasi cha sh 1,968,475,931 kwenda Chuo cha Taifa cha Utafiti wa Madawa na kiasi cha sh 3,083,400,000 kwenda Mradi wa Sekta ya Maendeleo ya Afya bila kibali cha Hazina

- **Mishahara iliyolipwa kwa watumishi wastaafu, wafu na watoro kazini Sh.83,768,896**

Jumla ya mishahara inayofikia kiasi cha sh.83,768,896 ililipwa kwa watumishi ambao hawako kwenye utumishi wa umma. Hii imekuwa na athiri ya ongezeko la mishahara serekalini na ni matumizi mabaya ya fedha za umma.

- **Madai ya Matibabu yasiyokuwa na nyaraka Sh.32,579,904**

- **Kiasi cha Shs.32,579,904 kililipwa kwenda balozi za Tanzania ikiwa ni fedha kwa ajili ya matibabu. Hata hivyo, hapakuwa na hati za madai ya matibabu, stakabadhi za kukiri malipo, barua za rufaa na ripoti za matumizi kutoka ofisi za balozi zilizohusika na hivyo malipo yalifanywa kinyume na kanuni namba 95(4) ya sheria ya fedha za umma ya mwaka 2001 (iliyorekebisha mwaka 2004).**

- **Adhabu ya kuchelewesha michango ya mafao ya wastaafu Sh. 31,900,906**

Wizara ililipa kiasi cha Sh 31,900,906 ikiwa ni adhabu ya kuchelewesha michango ya wastaafu kinyume na Kanuni Namba 9(6) ya sheria utumishi wa umma mafao ya kustaafu ya mwaka 2003. Fedha hii isingelipwa endapo michango ya watumishi ingelipelekwa katika muda unaostaili.

- **Vifaa ambavyo havijapokelewa Sh.1,648,407,271**

Kiasi cha sh 1,895,253,371 kililipwa kwa wazabuni kabla ya kupokea vifaa. Hata hivyo, ukaguzi uliofanyika katika idara za Wizara umebaini kwamba vifaa vya thamani ya sh 1,648,407,271 vilikuwa havijaletwa. Hii ni kinyume na

	<p>kanuni 122 ya sheria ya manunuzi ya umma ya mwaka 2005</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Vifaa havijaingizwa kwenye daftari Sh.148,293,950</b> Kanuni 198 ya sheria ya fedha za umma ya mwaka 2001 inasema kwamba vifaa vyote vilivyonunuliwa lazima viandikwe kwenye daftari la vifaa. Kinyume na kanuni hii Wizara haikuandika kwenye daftari vifaa vya thamani ya Sh 148,293,950</li> </ul> <p><b>Masuala mengine</b></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Dosari kukaa muda mrefu bila ya kusafishwa katika benki na daftari la fedha.Masuala ya miaka ya nyuma ambayo hayakushughulikiwa yalikuwa sh 328,205,308.</li> <li>• Kulikuwa na madai ya kiasi cha Sh.210,240,827 na mihadi ya kiasi cha Shs.4,686,129,524</li> <li>• Taarifa ya upotevu ilionyesha upotevu wa kiasi cha sh 4,709,461,863.63 ikihusisha upotevu wa vifaa kiasi cha sh. 2,383,792.63 na madawa yaliyopitwa na wakati kiasi cha Sh.4,707,078,078,071 kwenye Idara ya Bohari Kuu ya Madawa katika mikoa mbalimbali.Upotevu huu ni wa tangu mwaka 2003/2004</li> </ul>
10	<b>FunGU 69: Wizara ya Maliasili na Utalii</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Wizara ina madai ambayo hayajashughulikiwa ya kiasi cha sh 663,541,372.75 ikijumuisha madai ya wazabuni na watumishi wa Wizara.Inaonekana kwamba Wizara inaudhaifu katika kudhibiti makisio yaliyopitishwa na Bunge kwani jumla ya matumizi yalizidi bajeti iliyopitishwa ukizingatia kwamba salio la fedha katika matumizi ya kawaida na maendeleo hadi tarehe 30 juni 2010 ilikuwa sh 65,601,951.09 tu. Mwelekeo huu una shindana na dhana ya bajeti ya fedha tasilimu inayotumiwa na Serikali. Zaidi ya hayo, viambatanisho vya madai ya kiasi cha sh 207,246,498 havikuweza kupatikana kwa ajili ya ukaguzi na kusababisha kutothibitishwa kwa uhalali wa madai hayo</li> </ul>

- Matumizi ya mwaka yanahusisha malipo yenye nyaraka pungufu ya kiasi cha sh 165,448,602 kinyume na kanuni 95(4) ya sheria ya fedha za umma ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004). Hivyo ni vigumu kujua kama ni matumizi halali ya fedha za umma.
- Mfumo wa uhasibu sio mzuri, kwani katika mwaka wa fedha 2009-10 nyaraka za mapokezi ya maduhuli ya kiasi cha Sh.1,667,139,734.64 kutoka kwenye vituo vya kukusanyia maduhuli hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. Zaidi ya hayo, kulikuwa na tofauti ya kiasi cha Sh.755,874,245.67 kati ya kiasi kilichoko kwenye taarifa ya maduhuli ya Sh 3,316,898,398.78 na kiasi kilichoko kwenye daftari la kukusanyia maduhuli.

Pia vyanzo vya makusanyo ya maduhuli kiasi cha Sh. 2,920,879,363.60 havikufahamika kwa sababu kumbukumbu hazikuandaliwa vizuri. Licha ya hayo, kiasi chote kiliingizwa kama maduhuli mbalimbali kinyume na utaratibu wa kihasibu wa kutambuliwa kama maduhuli yanayosubiri kurekebishwa.

- Makusanyo ya mrabaha wa mazao ya misitu katika daftari la maduhuli ilikuwa zaidi ya kiasi cha Sh 242,735,027 maduhuli yaliyopokelewa na kukatiwa stakabadhi. Tofauti hii haikuwa na maelezo na uthibitisho wa marekebisho haukuwasilishwa ukaguzi kwa uhakiki.
- Wizara haina mafunzo au maarifa kuhusu matakwa ya viwango vya kiamtaifa vya kihasibu katika sekta ya umma yenye misingi ya fedha tasilimu kuaandaa na kuonyesha taarifa za fedha. Kwa mfano, misaada kutoka nje ya nchi iliyopokelewa kwa mwaka kwenye Mfuko wa Mambo ya Kale hazikuonyeshwa kama inavyotakiwa na aya 1.10.8 ya IPSAS.
- Wizara ina vituo vya urithi wa utammaduni na mali za mambo ya kale ya kihistoria ambavyo viko chini ya udhibiti wa Wizara. Mali zote hazikuoneshwa kwenye Taarifa ya fedha ya wizara kama inavyotakiwa na aya 8&9 ya viwango vya kimataifa vya kihasibu katika sekta ya umma

### Masuala ya kuzingatia

- Wizara ilipokea fedha pungufu kiasi cha sh 13,158,440,624 katika fungu la maendeleo na kiasi cha Sh.5,430,733,361 fungu la kawaida.Ni dhahiri kwamba wizara haikutekeleza mipango yake ya mwaka.
- Wizara ilifanya maamuzi ya upendeleo kwa kutoa kiwango cha chini cha mrabaha wa mazao ya misitu kuliko kiwango cha sheria ya misitu (CAP 323) na Kanuni za misitu za mwaka 2007 bila kibali cha mamlaka husika.Hivyo, Serikali kupoteza kiasi cha Sh 874,853,564.
- Shamba la miti Sao Hill lilitoa mkopo wa kiasi cha sh 53,815,000 kwa Idara na Taasisi nyingine bila ruhusa ya Mlipaji Mkuu kinyume na Kanuni 105 ya sheria ya fedha ya umma ya mwaka 2001( iliyorekebishwa mwaka 2004) inayotaka mikopo yote kupata kibali cha Mhasibu Mkuu
- Afisa Masuuli alilipa posho ya samani ya kiasi cha Sh.18,830,539 kwa watumishi ambao hawakustahili wanaoishi kwenye nyumba zao kinyume na waraka wa Utumishi namba C/AC/134/213/01/G/69 wa tarehe 30 Januari 2006
- Kutokana na mfumo wa ndani wenye uthibiti hafifu, mishahara kiasi cha sh10,052,511.80 ililipwa kwa watumishi ambao ni wastaafu,waliokufa na walioacha ajira na kusababisha matumizi ya fedha za umma yasiokuwa na manufaa.

11	<b>Fungu 94: Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Taarifa za fedha (zikijumuisha akaunti za kawaida, maendeleo na maduhuli) zilikuwa na kasoro na dosari nyingi zilizokuwa zinahitaji marekebisho. Lakini mpaka ripoti hii inaandikwa, uongozi ulikuwa bado haujatoa maelezo na kusafisha dosari katika taarifa za fedha.</li> <li>• Katika mwezi Juni mwaka 2010 Ofisi ya Raisi Tume ya Utumishi wa Umma ililipa kiasi cha sh 80,000,000 kwenda Shirika la Utangazaji la Tanzania ikiwa ni gharama za matangazo dakika 15 kuhusu programu ya elimu. Kiasi cha sh 750,000 kilitoka katika kasima ya matumizi ya kawaida na kiasi cha 75,250,000 kilichobaki kilitakiwa kulipiwa katika kasima ya matangazo na uchapaji lakini kilitolewa katika kasima nyingine kimakosa</li> <li>• Malipo ya kiasi cha sh 94,712,958 yalikuwa na nyaraka pungufu.</li> </ul>
12	<b>Fungu 96: Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Wazabuni walichaguliwa bila kibali cha bodi ya tenda katika manunuzi ya kiasi cha Sh.20,285,000</li> <li>• Hakuna vielelezo vinavyoonyesha jinsi gani wazabuni walivyochaguliwa na Wizara katika kutoa huduma</li> <li>• Mapokezi ya maduhuli hayakuwa na kiambatanisho cha fomu za mgawanyo wa kiasi cha Sh.143,961,660 Meneja wa shirikisho la mpira wa mguu, muungano wa vyama vya mpira wa mguu na uwanja wa mpira wa Uhuru mara kwa mara wamekuwa wakiwasilisha Wizarani makusanyo ya viingilio vya mlangoni bila kuambatanisha fomu za mgawo ikiwa kama kielelezo cha makusanyo halisi.</li> <li>• Malipo yenye nyaraka pungufu ya kiasi cha shilingi 69,914,468</li> <li>• Bakaa ambazo hazijasuluhishwa katika ongezeko</li> </ul>

	<p>la mali za Wizara sh 399,380,530</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Vifaa ambavyo havijaingizwa kwenye leja Sh.27,250,000</li> <li>• Kiasi cha sh 32,936,299 kililipwa kama posho ya samani kwa watumishi ambao hawakusitahili hii ni kinyume na kanuni za Utumishi</li> <li>• Hapakuwa na vielezo vya makabidhiano kuhusu Mtunza fedha na matumizi ya kiasi cha 5,000,000 kilichokuwa Ofisi ya Mtunza fedha</li> <li>• Michango kwenda jumua za kimataifa kiasi cha 98,468,000 hazikuwa na nyaraka</li> <li>• Mapitio ya ada za Chuo cha Michezo Malya yamebaini kiasi cha shilingi 16,650,000 hazikukusanywa kwa wanachuo walio ingia mwaka wa masomo 2009/2010</li> </ul> <p><b>Masuala mengine</b></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Wizara haina sera na taratibu za habari na tekinolojia</b></li> <li>• <b>Chuo cha Michezo Malya:</b> <ul style="list-style-type: none"> <li>– Chuo hakina rejista ya mali</li> <li>– Chuo hakina hati miliki</li> </ul> </li> </ul>
13	<p><b>Fungu 71 Sekretarieti ya Mkoa wa Pwani</b></p>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Sekretarieti haikuandaa na haikuwasilisha taarifa za suluhisho za benki katika akaunti za Kawaida, Maendeleo, Amana na Maduhuli kwa mwaka wa fedha 2009-10. Hivyo, usahihi wa salio katika benki akaunti haukuthibitishwa.</li> </ul> <p><b>Masuala ya kuzingatia</b></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Gari la wagonjwa aina ya IVECO lenye thamani ya Euro 66,000 sawa na shilingi 123,750,000 lililoagizwa mwaka huu kutoka kampuni ya Incar Tanzania LTD ya S.L.B 20479 DSM lilikuwa bado halijapokelewa.</li> </ul>

	<p><b>Masuala mengine</b></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Mkataba ulioingiwa na Sekretarieti na mtoa huduma katika mwaka wa fedha 2008-09 umeonyesha mabadiliko ya bei makubwa katika eneo la mraba ikilinganishwa na bei za mwaka 2009-10 na hakuna maelezo yaliyotolewa kuhusu mabadiliko hayo.</li> <li>• Malipo ya kiasi cha shilingi 14,056,000 yalikuwa na nyaraka pungufu kama vile karatasi ya mahudhurio, fomu ya madai, taarifa za usimamizi na orodha ya walipwaji havikuambatanishwa.</li> </ul>
14	<p><b>Fungu 75: RAS Kilimanjaro</b></p>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>Matumizi yasiyokuwa na nyaraka Sh.17,441,417</b> Malipo ya kiasi cha sh 17,441,417 yalionekana kwenye daftari la fedha lakini hati za malipo hazikupatikana kinyume na Kanuni 86(1) ya sheria ya fedha ya umma mwaka 2001 inayotaka malipo yote ya fedha za umma kuwa na hati za malipo na viambatanisho vyote.</li> <li>• <b>Malipo ya fidia ya ardhi kutokuwa na jedwali la fidia Sh. 66,947,000</b>  Kwa mwaka wa fedha 2009-10 Ukaguzi ulibaini kwamba sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro ililipa kiasi cha Sh. 66,947,000 kwa wananchi ikiwa ni fidia ya ardhi ili kuruhusu ujenzi wa barabara Wilaya ya Rombo. Malipo haya hayakuwa na jedwali la wananchi waliofidiwa kinyume na Kanuni 95 ya sheria ya fedha ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004)</li> <li>• <b>Matumizi yaliyofanyika kwenye kasma isiyosahihi Sh.12,471,000</b>  Kanuni 115 ya sheria ya fedha ya mwaka 2001 inasema kwamba makisio yaliyopitishwa na Bunge ndio msingi wa mahesabu ya mwaka na mchanganuo wa maduhuli na</li> </ul>



matumizi lazima ufuatae makisio haya. Kinyume na hayo, matumizi ya posho ya malazi ya kiasi cha 14,971,000 yalifanyika kimakosa kwenye kasima ya mali, mitambo na vifaa na hivyo kusababisha kuandikwa kiasi kikubwa katika kasima hii.

- **Mishahara ambayo haikuchukuliwa na haijarejeshwa Hazina Sh.211,495,309**

Mishahara ambayo haikuchukuliwa kiasi cha Sh.211,495,309 iliyokuwa imepokelewa kutoka Halimashauri na Sekretarieti iliyohusu wastaafu, waliokufa na watumishi walioacha kazi ilikuwa haijarejeshwa Hazina kinyume na Kanuni 113(3) ya sheria ya fedha ya mwaka 2001 na waraka wa Wizara ya Fedha namba EB/AG/5/03/01VOL.VI/136 wa tarehe 31 Agost 2007. Zaidi ya hayo, Sekretarieti haitunzi rejista ya mishahara ambayo haichukuliwi.

- **Mabadiliko ya mkataba yasiyo na kibali Shs.13,349,000**

Katika maeneo mawili Sekretarieti ya Mkoa ilifanya mapitio ya muda wa mkataba, bei na kazi zilizoainishwa kwenye mkataba na kusababisha malipo ya ongezeko la kazi za thamani ya Sh 13,349,000 bila ya kupitishwa na mamlaka inayotoa kibali. Hii inaonyesha hapakuwa na usimamizi na uendeshaji mzuri wa mikataba.

- **Ukiukaji wa mkataba wa ununuzi wa gari la wagonjwa Sh.125,000,000**

Katika Mwezi Septemba mwaka 2009 kiasi cha sh 125,000,000 kililipwa kwa kampuni ya Incar Tanzania LTD kwa ajili ya ununuzi wa gari jipya aina ya IVECO kwa ajili ya Hospitali ya Mawenzi. Gari hilo lilitarajiwa kupokelewa kati ya wiki 8 hadi 12 tangu tarehe ya kukubali ununuzi. Hadi tuna fanya ukaguzi ilionekana kuchelewa kwa takribani mwaka mmoja na miezi mitatu kinyume na kanuni 87(1) (h) na 198 ya sheria ya manunuzi ya umma ya mwaka 2005.

- **Ununuzi wa vifaa vya hospitali nje ya Bohari ya Madawa Sh.55,536,000**  
 Malipo ya kiasi cha sh.55,536,000 yalifanyika kwenye akaunti ya amana kuwalipa wazabuni wa madawa na vifaa vya hospitali ambao hawakuwa wamepitishwa na Bohari ya Madawa kinyume na kifungu 51 cha sheria ya manunuzi ya umma namba 21 mwaka ya 2004.
- **Manunuzi yaliyofanywa nje ya wazabuni Sh.11,672,800**  
 Kifungu 35(b) cha sheria ya manunuzi ya umma ya mwaka 2004 kinataka kitengo cha manunuzi kusaidia utendaji kazi wa bodi ya tenda. Na kifungu 35(c) kinakitaka kitengo cha manunuzi kutekeleza maamuzi ya bodi ya tenda. Katika mwaka wa fedha 2009-10 ukaguzi ulibaini kwamba malipo ya kiasi cha Sh.11, 672,800.00 ikiwa ni manunuzi mbalimbali yalifanywa kwa wazabuni ambao hawakupitishwa na bodi ya tenda.
- **Matengenezo ya magari bila kupitia TEMESA Sh.13,833,969**  
 Kiasi cha sh.13,833,969.00 kililipwa kwa karakana mbalimbali ikiwa ni matengenezo ya magari ya Sekretarieti ya Mkoa bila ya kuwa na taarifa ya ukaguzi kutoka TEMESA ambao ndio wana wajibu wa kuthibitisha matengenezo ya magari ya Serikali kulingana na kifungu 59(4) cha sheria ya manunuzi ya umma namba 21 ya mwaka 2004.
- **Magari matatu hayajapokelewa Shs.329,877,640**  
 Ukaguzi wa hati za malipo umebaini kuwa Sekretarieti ya mkoa wa Kilimanjaro ililipa kwa Katibu Mkuu Wizara ya Miundombinu kiasi cha sh 329, 877,640.00 ikiwa ni malipo kwa ajili ya kuagiza magari matatu hata hivyo, magari hayo bado hayajapokelewa.

15	Fungu 84: RAS Singida
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Taarifa ya kupokea fedha na malipo na kielekezi namba 18 cha taarifa ya fedha vinaonyesha kiasi kilichohamishwa cha sh 59,826,434,600 badala ya sh 57,809,641,600 na hivyo kusababisha tofauti ya sh 2,016,793,000. Tofauti hii inahussisha:ujenzi wa hospitali ya rufaa Singida sh 1,977,435,999 bodi ya sheria sh 4,557,000 na mradi wa kujitegemea wa sh. 34,800,000 yaliyokuwa yanafanywa na Sekretarieti ya Mkoa</li> <li>• Kielekezi namba 19 cha taarifa za fedha kinaonyesha ununuzi/ujenzi unaofikia kiasi cha sh 652,323,326 badala ya sh.2,664,559,326 ambacho kimesababisha tofauti ya Sh.2,012,236,000.Manunuzi /ujenzi haukuhusisha kiasi cha Sh 1,977,435,999 zinazohusu ujenzi wa hospitali ya rufaa Singida na kiasi cha Sh 34,800,000 zinazohusu mradi wa kujitegemea ambavyo vimeonyeshwa kwenye kundi la uhamisho wa fedha.</li> <li>• Sekretarieti ya mkoa ilinufaika na huduma/vifaa mbalimbali kama vile vifaa vya hospitali, huduma za kitaalamu, madawa na huduma za kitabibu zilizonunuliwa na watu wengine kwa ajili ya Sekretarieti zenye thamani ya Dola za Kimarekani 4,703,714 na Sh.248,960,169.61 Lakini,taarifa ya mapokezi ya fedha na malipo haikuonyesha vifaa na huduma vilivyoununuliwa kwa niaba ya Sekretarieti kinyume na matakwa ya viwango vya kimataifa vya kahasibu katika sekta ya umma</li> </ul> <p><b>Masuala mengine</b></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Wizara ya Afya na Usitawi wa Jamii hupeleka fedha katika bohari ya madawa kwa ajili ya hospitali ya mkoa ili kununua madawa na vifaa vya hospitali. Ukaguzi ulibaini kwamba hospitali ya mkoa wa Singida haikuwa na kumbukumbu za fedha zilizoletwa na Wizara ya Afya na</li> </ul>

	<p>Usitawi wa Jamii kwenda hospitali ya mkoa kununua madawa na vifaa vya hospitali ingawa bohari ya madawa ilionyesha kiasi cha 248,990,169 katika taarifa za fedha.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Wakati wa kuhesabu mali iligundulika kwamba vifaa mbalimbali ambavyo vimepitwa na wakati na vilivyoharibika vya thamani ya sh 19,697,000 vilikuwa bado havijaondolewa kwenye vitabu kwa muda mrefu kinyume na Kanuni 252 ya sheria ya fedha ya umma ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004)</li> <li>• Kulikuwa na fedha pungufu iliyotolewa sh. 7,828,256,594 na Serikali mwaka wa fedha 2009-10 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2008-09 ambayo ilikuwa ni sh Sh.9,697,356,275.hii ni tofauti ya Sh 1,869,099,681 ambayo ni sawa na upungufu wa asilimia 19.3.Hali hii siyo nzuri kwa maendeleo ya Mkoa.</li> </ul>
16	<b>Fungu 87: RAS Kagera</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Mafuta yenye thamani ya Sh.3,400,000 yalinunuliwa lakini hayakuingizwa vitabuni.</li> <li>• Sekretarieti ilifanya matumizi ya Sh.48,452,500 bila nyaraka sahihi hivyo hatukuweza kuthibitisha kama matumizi hay yalikuwa halali.</li> <li>• Sekretarieti ina kulipwa Sh.21,662,551 kwa Ofisa ambaye alikaa muda mrefu nje ya nchi akiwa masomoni. Kwa vile faedha hizi zililipwa katika akaunti yake binafsi, hatukupata nyaraka za kuthibitisha kupokelewa kwa fedha hizo.</li> <li>• Malipo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za daraja A Shs.44,550,900 lakini hapakuwa na kumbukumbu za kuonyesha kama gharama zilizotumika ni halali</li> <li>• Mapendekezo ya wakaguzi kwa miaka ya nyuma ya Sh.8,981,298,491 hayakutekelezwa.</li> </ul>

	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Nyaraka za malipo ya mishahara ya Shs.47,858,234 hazikuwasilishwa kwa ukaguzi.</li> <li>• Mishahara ya jumla ya Sh.18,217,279 ilifutwa katika payrolls ya kompyuta. Hapakuwa na ushahidi kama fedha hizi zilihamishiwa Hazina.</li> </ul>
17	<b>Fungu 85: RAS Tabora</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kulikuwa tofauti katika taarifa ya mtiririko wa fedha ya Sh10,328,145 ambayo imetokana na kuzidisha makusanyo kwa Sh. 25,186,826 / 31 na malipo kwa Sh. 35,514,971. Tofauti hizi zilikuwa bado kusuluhishwa.</li> <li>• Mali na vifaa visivyohamishika vyenye thamani ya Sh. 12,233,800 ikiwa ni pamoja na jenereta, kompyuta, samani na friji, hazikuingizwa katika kumbukumbu za vitabu vya mali za kudumu. Taarifa za kifedha zimeandaliwa pungufu kwa kiasi cha Sh.12,233,800</li> <li>• Vifaa vyenye thamani ya Sh.19,693,560 vilinunuliwa lakini havikuingizwa vitabuni. Hatukuthibitisha kama vifaa hivyo vilipokelewa na kufanya kazi iliyokusudiwa.</li> <li>• Hapakuwa na ushahidi wa maandishi kuonyesha kuwa madeni ya Shs.309,129,360 ambayo hayakuonyeshwa vitabuni yalikuwa yamerekebishwa katika taarifa ya fedha.</li> <li>• Hati za malipo ya jumla ya Sh 11,793,000 hazikuletwa kwa ukaguzi, hivyo hatukuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.</li> <li>• Sekretarieti ilifanya matumizi ya Sh. 119,742,418bila nyaraka sahihi hivyo hatukuweza kuthibitisha kama</li> </ul>

	<p>matumizi hay yalikuwa halali.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Ukaguzi wa nyaraka za mkataba ulionyesha kwamba kazi hazikukamilika kwa wakati, hata hivyo, mkandarasi hakukatwa gharama za ucheleweshaji wa mkataba za Sh.196,453,008 kulingana na matakwa ya mkataba.</li> </ul>
<b>18</b>	<b>Fungu 89: RAS Rukwa</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Uhakiki wa bakaa za mwanzo wa mwaka katika taarifa ya mtiririko wa fedha ya Juni 30, 2010 ilibainisha kuwa, "Malipo mengine" katika taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka wa fedha 2008/2009 ilibadilika kuwa Shs.784,995,511.10 badala ya Shs.691,322,137.20 ambayo ilisababisha tofauti ya Sh. 93,673,373.90, tofauti ambayo ilipelekwa katika taarifa za mwisho wa mwaka wa fedha 2009/2010.</li> <li>• Taarifa ya mali ghalani ya Juni 30, 2010 ilionyesha kuwa na bakaa ya Sh.17, 655,450.00 hata hivyo hapakuwa na majedwali ya kuonyesha aina ya vifaa vilivyokuwepo ghalani.</li> <li>• Vifaa vyenye thamani ya Shs19,728,778 vilinunuliwa lakini havikupokelewa. Wadaiwa waliouza vifaa hivi hawakuingizwa katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka.</li> <li>• Kiasi cha Sh.11,340,000 kililipwa katika vifungu mbalimbali visivyohusika na aina ya malipo yaliyofanyika, hivyo usahihi wa tarakimu zilizoonyeshwa katika taarifa za fedha haukuweza kuthibitika.</li> <li>• Katika mwaka husika, ofisi ya Sekretarieti ilitoa vitabu 2,130 vya hati za pembejeo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga. Kwa ajili ya kusambazwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga na Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga lakini</li> </ul>

	<p>vitabu 10 vya DAP / MRP vyenye thamani ya Sh.25,000,000 havikupokelewa na Halmashauri yoyote kati ya hizi mbili. Na hivyo kuwa na wasiwasi kama mapato haya yalipokelewa na kuingizwa katika taarifa za fedha.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Malipo kufanywa bila ya mkataba wa makubaliano na hati ya mkandarasi kuthibitisha kama kazi imekamilika Sh.10,351,411</li> <li>• Sekretarieti haikumtoza mkandarasi gharama za kuchelewesha kukamilisha ujenzi wa ofisi ya katibu kata ya Inyonga Wilaya ya Mpanda katika Sh.3,712,601.79 na Jengo la Mkoa la kuhifadhi chanjo Sh.4,319,003</li> </ul>
<b>19</b>	<b>Fungu 92 TACAIDS</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Masurufu ya kiasi cha Shs.48, 245,000 hayakuonyeshwa katika taarifa za fedha. Hii ni kinyume na Kifungu.103 (1) cha Kanuni za Fedha za Umma ya 2001 (iliyorekebishwa mwaka 2004).</li> <li>• Malipo ya jumla ya Sh.1,044,265,701 yalifanywa bila nyaraka sahihi kinyume na kanuni na.95 (1) na (4) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001 ambayo inahitaji malipo yoyote ya fedha za umma yawe na nyaraka kamilifu.</li> <li>• Kulikuwa na upungufu wa fedha zilizopokelewa katika Akaunti ya Maendeleo kwa Sh.11, 481,564, 727 sawa na 50.9% ya bajeti iliyopitishwa. Hii inamaanisha kwamba shughuli zilizopangwa kutekelezwa hazikutekelezwa.</li> </ul>
<b>20</b>	<b>Fungu 95: RAS Manyara</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Baadhi ya mali na vifaa vya Sekretarieti vilivyoonyeshwa taarifa ya fedha bila kuonyesha thamani ya vifaa hivyo na hivyo kufanya takwimu</li> </ul>

	<p>katika taarifa za fedha kuwa pungufu ya zilizoonyeshwa.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2010 ulionyesha kuwa kiasi cha Sh.2,540,631,398.39 kama Manunuzi / au ujenzi wa mali za kudumu. Hata hivyo, kiasi cha taarifa ni tofauti na kiasi halisi cha manunuzi yaliyofanywa katika kipindi cha mwaka ambayo ilikuwa ni Shs.488,034,417.95 na hivyo kusababisha tofauti ya Sh.2,052,596,980.40.</li> <li>• Kulingana na kifungu na.25 (2) (b) cha Sheria ya Fedha za Umma na. 6 ya 2001 (iliyorekebishwa 2004) Sekretarieti haikuwasilisha taarifa ya mihadi ya Sh.1,779,066,159.</li> <li>• Mishahara isiyolipwa ya Shs.89,116,462.95 haikupelekwa Hazina kinyume na kanuni na..113 (3) ya Kanuni za Fedha za Umma 2001 (iliyorekebishwa 2004) na maelekezo ya Hazina yaliyotolewa kwa njia ya waraka Na. EB/AG/5/03/01/VOL .VI/136 wa tarehe 31 Agosti 2007.</li> <li>• Kiasi cha Sh.16,571,775 kililipwa kwa wadai kinazohusiana na miaka ya nyuma ingawa malipo haya hayakuuingizwa katika orodha ya wadai aliokuwepo mwanzo wa mwaka.</li> <li>• Malipo ya jumla ya Sh.83,562,240.56 yalilipwa kwa wafanyakazi mbalimbali na mashirika mengine bila ya kuwa na nyaraka kamilifu kinyume na Kanuni. 95 (4) ya Kanuni za Fedha za Umma ya 2001 (iliyorekebishwa 2004).</li> </ul>
<b>21</b>	<b>Ubalozi wa Tanzania - Bussels</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Ubalozi hakutayarisha taarifa za kila mwezi za usuluhishi wa hesabu kwa ajili ya akaunti ya matumizi ya kawaida mapato na akaunti za amana kwa mwaka</li> </ul>



	<p>mzima wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2010. Kutokana na kukosekana kwa taarifa ya usuluishi wa benki, usahihi taarifa za fedha haikuweza kuthibitika.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Kumbukumbu zilizopatikana kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa zilionyesha kuwa fedha iliyopelekwa Ubalozi wa Tanzania Brussels ilikuwa Sh.1,317,504,285.81 dhidi ya Sh.1,017,456,538.00 inayoonekana katika taarifa ya fedha ya Ubalozi hivyo kusababisha tofauti ya Shs.300, 047,747.81 ambayo haofasulishwa.</li> <li>• Datftari mapato na matumizi kwa ajili ya akaunti ya matumizi ya kawaida kilikuwa na kumbukumbu duni kwa vile malipo mengi yaliandikwa kimakosa au hayakuandikwa kabisa kinyume na Kanuni.126 (3) ya Kanuni za Fedha za Umma 2001 (iliyorekebishwa 2004). Aidha, datftari mapato na matumizi kwa ajili ya ukusanyaji wa maduuli halikuandaliwa kabisa. usahihi wa matumizi na mapato, na takwimu za fedha hazikuwezakuthibitika.</li> </ul>
<b>22</b>	<b>Ubalozi wa Tanzania - Kampala</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Mishahara ya kiasi cha Sh. 7,760,443.50 ililipwa kwa mmoja wa wafanyakazi wenyeji wa nchi hiyo bila kuwa na mkataba wa ajira na idhini ya ajira.</li> <li>• Ukaguzi alibainisha tofauti ya Sh. 3,448,189.38 kati fedha zilizopelekwa na kiasi kilichopokelewa .</li> <li>• Wakati wa mwaka wa ukaguzi, ubalozi ulitumia Sh.77,429,617.78 kwa matumizi ambayo hayakuwa katika bajeti ya mwaka iliyoidhinishwa na bunge.</li> <li>• Ubalozi ulikuwa na bakaa katika akaunti ya Amana ya shilingi 36,058,001 hata hivyo hapakuwa na maelezo ya kutosha kuhusu wamiliki wa fedha hizo.</li> </ul>

7.10. Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa zilizopewa hati yenye mbaya pamoja na sababu za maoni hayo.

1	Fungu 76: RAS Lindi
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Ukaguzi ulibaini kuwa bidhaa zenye thamani ya Shs.15, 258,153 zilinunuliwa lakini hazikuingizwa vitabuni kinyume na Kanuni. Namba 191 (1) na 192 ya Kanuni za Fedha za Umma 2001.</li> <li>• Ukaguzi wetu ulibaini kuwa jumla ya Sh.51,981,215 hazikuingizwa katika taarifa ya mapato na matumizi na hivyo kusababisha bakaa ya fedha taslimu kutolewa taarifa pungufu.</li> <li>• Wigo wetu wa ukaguzi ulizuiwa kwa vile hapakuwa hati za malipo pamoja na nyaraka husika za matumizi ya thamani ya Sh.1,687,462,267</li> <li>• Malipo ya jumla ya Sh. 173, 256,288 yalifanywa bila nyaraka sahihi kinyume na kanuni na.95 (1) na (4) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001 ambayo inahitaji malipo yoyote ya fedha za umma yawe na nyaraka kamilifu.</li> <li>• Sekretarieti ya Mkoa wa mwisho wa mwaka wa fedha ilikuwa na bakaa ya Shs.186, 595,182 katika akaunti ya matumizi ya kawaida. Hata hivyo, ukaguzi haukuweza kuthibitisha kama fedha hizo zilirudishwa kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali.</li> <li>• Taarifa ya mtiririko wa Fedha kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2010, ilionyesha mapato mengine ya Sh.1,887,697,417 na malipo mengine ya Shs.876, 829,334 katika Akaunti ya Amana. Hapakuwa na jedwali linaloonyesha jinsi fedha hizo zilivyopokelwa na kulipwa kwa watu mabalimbali hivyo kushindwa kuthibitisha usahihi wa malipo hayo.</li> </ul>

	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Katika mwaka wa ukaguzi, tulibaini madeni ya Shs.613,884,610 kwa mwaka uliomalizika Juni 30, 2010 ambayo hayakuwa na maelezo yoyote kuhusu nani anadai na kwa shughuli gani. Hatukuweza kuhakiki usahihi wake.</li> <li>• Mali na vifaa ghalani vyenye thamani ya Shs.78,923,570 havikuweza kuthibitishwa usahihi wake kwa vile hapakuwa na hati za kuhesabia zilizoidhinishwa na Afisa Masuuli, Mkaguzi Mkuu wa Ndani na mkuu wa Kitengo cha Manunuzi.</li> </ul>
2	<b>Hesabu za Majumuisho</b>
	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya Uhasibu - IPSAS 6, hesabu za majumuisho zinatakiwa kuhusisha taasisi zote za umma ambazo Serikali ina uwezo wa kutoa maamuzi ikiwa ni pamoja na Serikali za Mitaa, Wakala wa Serikali, sehemu ambayo Serikali imewekeza mitaji nk. Kanuni hizi hata hivyo haiyahasu makampuni yanayofanya kazi kwa ajili ya kupata faida.</li> </ul> <p>Taarifa za kifedha za mashirika haya hayakujumuishwa katika hesabu za taifa za majumuisho isipokuwa kwa asilimia ya uwekezaji katika taasisi hizo. Mali, madeni, mapato na matumizi ya taasisi hizi havikujumuishwa katika hesabu za majumuisho. Taarifa zilizoandaliwa ni sehemu tu ya hesabu za taifa na haitoi picha kamili ya hali ya kifedha na utendaji wa kifedha wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Hesabu za Taifa za majumuisho hazikujumuisha mizania yaani taarifa ya hali ya kifedha ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano ikiwa ni pamoja na mali yote ya Serikali kama vile majengo, madaraja, barabara,</li> </ul>

shule n.k na madeni kinyume na kifungu cha 25 wa Sheria ya Fedha ya Umma ya 2001 (iliyorekebisha 2004).

- Hatukupata ufafanuzi wa kina wa fedha zilizokuwa zinahamishwa kiasi cha Sh.13,475,072,714 kuonyesha jinsi fedha hizo zilivyopokelewa katika Akaunti ya Mlipaji mkuu wa Serikali (PMG).
- Wizara ya Fedha ilihamisha kiasi cha Shs.100 bilioni kwa kipindi kilichoishia Juni 30, 2010 kwenda TIB kwa ajili ya kuibadilisha TIB kuwa taasisi ya Maendeleo ya Fedha na pia kufungua benki kwa ajili ya shughuli za kilimo. Aidha, uwekezaji katika mashirika tisa (9) haukuonyeshwa katika hesabu za majumuisho.
- Hesabu za Taifa za majumuisho hazikuonyesha madeni ya thamani ya bilioni Shs.48.75. kiasi hiki kinajumuisha madeni yote ambayo Benki Kuu inaidai Serikali.
- Mali za kudumu zilizonunuliwa katika kipindi cha mwaka wa ukaguzi za Shs.118 bilioni, wakati Serikali ina amana ya kiasi cha Shs.143.09 bilioni vyote havikuonyeshwa katika hesabu za Taifa za majumuisho .
- Usuluishi wa benki wa hesabu za taifa za majumuisho zilionyesha maswala ambayo yalikuwa hayajasulushwa kwa muda mrefu mengine tangu mwaka 2000. Pia, katika orodha ya hundi ambazo hazikuwasilishwa kulikuwa na hundi ambazo hazijawasilishwa benki kwa zaidi ya miezi 6, na hivyo kuzifanya zichache. Hakuna marekebisho yaliyofanyika kuzifuta kutoka katika vitabu vya Serikali.

- Akaunti kuu ya malipo ya Serikali ilifungwa ikiwa na nakisi ya Sh.1,331,073,630,470.30 kutoka Benki Kuu ya Tanzania hii ni kutokana na jumla ya mapato ya Sh.7,928,122,248,611 dhidi ya matumizi ya jumla ya Sh.8,522,395,969,190 hivyo kusababisha nakisi ya jumla ya Sh.594,273,720,579. Mwisho wa mwaka, benki yalifikia jumla ya Sh.1,331,073,630,470.30. Nakisi hii haikujumuishwa katika taarifa ya deni la taifa kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2011.
- Hesabu za Taifa za majumuisho zilionyesha madeni ya thamani ya Sh.160,756,067,190 tarehe 30 Juni, 2010. Kwa kuzingatia ukweli kwamba Serikali inafanya malipo kwa misingi ya fedha taslimu, na kwa vile mfumo wa kompyuta wa uhasibu (IFMS) una uwezo wa kuzuia hati za malipo ambapo hakuna bajeti katika vifungu husika, hatukuweza kufahamu ni vipi madeni haya yalijitokeza.
- Serikali ilikuwa na kesi mahakamani katika mafungu kumi na mawili ya jumla ya Shs.26, 276,785,317 kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni, 2010. Matokeo na hatima ya kesi hizi hayakuweza kufahamika. Kama Serikali ikishindwa katika maamuzi ya mahakama, inaweza kulazimika kulipa kiasi kikubwa cha fedha.
- Kulikuwa na ongezeko la malimbikizo ya mapato kutoka Sh.10,020,246,900 mwaka 2008/09 hadi Shs.116, 320,437,345 kwa mwaka wa ukaguzi. Serikali inapswa kuongeza juhudi za kukusanya mapato yake.
- Kumekuwa na ongezeko kubwa la deni la taifa katika kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2010 kutoka Sh.7,621,286,730,034 mwishoni mwa mwaka wa fedha 2008/09 hadi kufikia Sh.10,503,806,011,885 ongezeko la zaidi ya 38%. Mwenendo huu kama hautadhibitiwa unaweza kuitia Serikali katika mzigo

mkubwa wa kulipia madeni. Ongezeko hilo ni la kutisha licha ya ukweli kwamba Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizopokea kiasi kikubwa cha misamaha ya madeni ya Nchi Masikini zenye Madeni Makubwa (HIPC) na MDRI.

- Serikali imeshindwa kukusanya mikopo ya jumla ya Shs.424,087,766,124 mikopo iliyotolewa na Serikali kwa M / s. Ginaac Industries Ltd na M/s. Mansons Ltd na taasisi nyingine. Kati ya kiasi hiki kiasi cha Shs.325, 927,756 kilitangazwa kama kisichoweza kukusanywa kwa vile kampuni hizi hazipo. Hakuna ushahidi kwamba makampuni haya yalikuwa na dhamana yoyote wakati wa kupata mikopo hiyo.
- Uwekezaji katika Ushirika wa Serikali na taasisi binafsi (PPP) si mathubuti unaweza kuisababishia Serikali kubeba mzigo mzito wa gharama kubwa ambazo zingeweza kuepukika. Serikali imekuwa ikibeba mzigo mkubwa kama kulipa mishahara ya wafanyakazi wa wawekezaji binafsi na kulipa mikopo ya iliyochukuliwa na wawekezaji binafsi, mifano ni pamoja na Songas, TRL Ltd, IPTL Ltd, Kiwira Coal Mines Ltd, n.k
- Hesabu za Taifa za majumuisho zilionyesha kuwa Serikali imetoa dhamana za jumla ya Shs.711.804, 989,096. Hakuna ushahidi kwamba dhamana hizi ziliwekewa mali ya kudumu kama kinga wakati wakopaji wanaposhindwa kulipa mikopo yao. Hii ni kinyume na sehemu ya 13 na 14 ya sheria ya Mikopo ya Serikali, Dhamana na Misaada ya (1974). Serikali inakabiliwa na vihatarishi vya kulipa madeni haya wakati wakopaji wanaposhindwa kulipa madeni yao.



## SURA YA 8

### TATHMINI YA MFUMO UNGANIFU WA USIMAMIZI WA FEDHA (IFMS)

#### 8.1. Utangulizi

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilitoa zabuni kwa Kampuni ya Ukaguzi na Ushauri ya KPMG kufanya tathmini ya ufanisi wa Mfumo Unganifu wa Usimamizi wa Fedha (IFMS) katika Wizara, Idara, Wakala na Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

KPMG ilifanya tathmini ya kiwango cha juu ikihusisha shughuli na ufanyaji kazi, utekelezaji wa mradi na udhibiti kwa ujumla katika matumizi ya Teknolojia ya Mawasiliano inaouzunguka mfumo wa IFMS. Aidha, KPMG walifanya tathmini ya kama Serikali ya Tanzania ilikuwa inapata thamani kamili ya fedha kwa kuwekeza katika mfumo huo wa IFMS

Mfumo wa IFMS una umuhimu mkubwa kwa Serikali ya Tanzania kuweza kudumisha imani kwa umma kwa kutoa huduma zenye ufanisi ikiwa ni pamoja na usimamizi na udhibiti wa mapato na matumizi ya Serikali. Taasisi mbili kuu za Serikali zenye wajibu mkubwa wa kusimamia uendeshaji wa shughuli za Mfumo wa IFMS katika Serikali ni Mhasibu Mkuu wa Serikali (ACGEN) kwa upande wa Wizara, Idara na Wakala na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa upande wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa (LGAs).

Serikali ya Tanzania kama ilivyo kwa serikali nyingine yoyote inakabiliwa na shinikizo la kuwajibika kutoa huduma zenye ubora kwa gharama nafuu kwa wananchi wake. Mara nyingi, maboresho makubwa katika mfumo wa teknolojia ya mawasiliano kama yale yanayohusiana na utekelezaji wa 'integrated term efficiencies' na upunguzaji gharama. IFMS imewagharimu walipa kodi/wananchi mamilioni ya



dola za Kimarekani na hivyo, wana mategemeo makubwa ya kuona thamani ya fedha inapatikana.

Tathmini iliyofanywa na KPMG ililenga kulinganisha shughuli za mfumo wa IFMS na viwango kubalifu vilivyotolewa au kutangazwa, ikiwa ni pamoja na vile vya ndani na uzoefu wa KPMG wenyewe; uelewa wa Serikali kuhusu mfumo hii na uzoefu katika taasisi nyingine. Kazi ya KPMG ilihusisha majadiliano na Wizara, Idara na Wakala wa Serikali, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, watumishi wa Kampuni ya Soft-Tech pamoja na kupitia nyaraka zilizowasilishwa na taasisi hizo.

## 8.2. Madhumuni ya Tathmini iliyofanyika

Madhumuni ya tathmini iliyofanyika kuhusu ufanisi wa Mfumo wa IFMS ilikuwa kujiridhisha kama:

- i. Mfumo una uhibitaji wa ujumla na wa programu mbalimbali zinazotumika kwa lengo la kujihakikishia usiri na uhakika wa upatikanaji wa taarifa za mtandao pale zitakapohitajika
- ii. Mfumo wa IFMS unaendeshwa kwa ufanisi na kwa manufaa ikilinganishwa na viwango/vigezo kubalifu vilivyowekwa.
- iii. Rasilmali fedha katika utekelezaji wa mfumo wa IFMS zimetumika kwa ufanisi na kuleta matokeo yaliyokusudiwa na kwamba matumizi yote yalizingatia sheria na kanuni;
- iv. Mfumo wa IFMS unakidhi mahitaji yote ya utoaji taarifa kwa watumiaji wa mfumo huu ikiwa ni pamoja na Wizara, Idara na Wakala wa Serikalis na Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

### 8.3. Muhtasari wa Matokeo ya ukaguzi

#### 8.3.1 Udhhibiti dhaifu wa habari na Usalama

Imebainika kuwepo usimamizi dhaifu katika matumizi ya mfumo wa IFMS na udhibiti mdogo usioweza kuhakikisha usiri wa taarifa zilizoko katika mtandao. Imeonekana pia kuwa wasimamizi wa anwani za IFMS wameweza kufanya mabadiliko yoyote pasipo kutumia programu ya IFMS. Aidha, mfumo wa IFMS unaruhusu waingiza 'data' kubadili na kuidhinisha maelezo yaliyoko katika fomu ya kuagiza mali (LPO) na maelezo ya wateja. Udhaifu huu umefanya waingiza 'data' waweze kuandaa na kuidhinisha LPO pasipo Mhasibu Mkuu kujua; utaratibu ambao sio kubalifu.

Imebainika kuwa hakuna mpango wowote wa kuhakikisha kuwa taarifa zilizopo katika mfumo wa IFMS zinapatikana endapo janga litatokea. Hapakuwa na chapisho lolote rasmi linaloeleza jinsi ya kurejesha shughuli za mtandao baada ya maafa kutokea. Aidha, hapajawahi kufanyika majaribio ya kujihami (simulation) ili kujenga uelewa wa namna ya kujihami endapo maafa yatatokea. Vilevile, KPMG waligundua kuwa Mhasibu Mkuu wa Serikali aliingia katika mkataba na Benki Kuu ya Tanzania wa kuwa na eneo katika Jiji la Dare es Salaam kwa ajili ya kuweka kituo cha pamoja cha kuchakata 'data' wakati wa majanga yanayoweza kutokea katika mfumo wa IFMS. Hata hivyo, kituo hicho hakijawahi kutumika katika shughuli za majanga tangu kuanzishwa kwake.

- 8.3.2. Kukosekana kwa Mkakati wa Teknolojia ya Mawasiliano
- Uchunguzi wa KPMG ulibaini kuwa hapakuwa na mkakati wa ujumla wa Teknolojia ya Mawasiliano unaoenda sambamba na malengo ya Serikali ya muda mrefu. Mkakati wa aina hii unatakiwa kupanga mapema mahitaji mbalimbali ya kiteknolojia kwa Serikali katika ngazi mbalimbali za Wizara, Idara na Wakala wa Serikali, Mamlaka ya Serikali za Mitaa n.k., na kuamua ni mfumo gani unapaswa kuendelezwa

katika kila moja ya ngazi hizo hapo juu (Wizara, Idara na Wakala wa Serikali, Mamlaka ya Serikali za Mitaa).

Pia, KPMG walibaini kuwepo kwa sera ya usalama wa Teknolojia ya Mawasiliano isiyokuwa kamilifu na inayobadilika badilika katika Wizara, Idara na Wakala wa Serikali na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Inaaminika kuwa sera hii ilipaswa kuwa ndani ya Mkakati wa Sera ya Taifa ya Mawasiliano ili kuhakikisha kuwa hakuna mabadiliko ya mara kwa mara kwa watumiaji wa teknolojia hii katika Serikali yote.

### **8.3.3 Rasilmali za IFMS zilizolipiwa lakini hazitumiki kikamilifu**

Mwaka 2007, Mhasibu Mkuu wa Serikali alilipa kiasi cha Dola za Kimarekani 428,829 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kujikinga endapo maafa yatatokea katika mfumo wa mawasiliano ya habari. Aidha, kiasi cha Dola za Kimarekani 224,532 kililipwa mwaka 2009 kwa ajili ya huduma ya kutunza 'data'. Ijapokuwa huduma hii ililipiwa, ilibainika kuwa haitumiwi. Kwa sasa, italazimu kufanya tathmini ili kuona kama baadhi ya sehemu za huduma hiyo ya kutunza 'data' zinafaa kutumika au zimekwishapitwa na teknolojia mpya.

Pia dawati la msaada kwa huduma za Mawasiliano ya Habari halitumiwi kikamilifu na hakuna taarifa zozote ambazo zingesaidia kuhakikisha kuwa manufaa yanapatikana katika rasilmali zilizowekezwa ikiwepo rasilmali watu. Mapitio yaliyofanyika katika mfumo wa IFMS yalibaini kuwa leseni 55 za programu itumikayo katika dawati la huduma kwa mteja zilinunuliwa mwaka 2004/05 ili kusaidia kutatua matatizo ya watumiaji wa mtandao. Hata hivyo, ni watumiaji 27 tu ndio wanaotumia leseni hizo kikamilifu.

Kuna jumla ya leseni za IFMS 225 katika Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali (ACGEN). Kwa mwaka wa fedha husika, ACGEN alilipia AMC kwa ajili ya leseni 554. Zaidi ya hapo,

kuna jumla ya watumiaji 191 wa mfumo wa 'Active Planner' dhidi ya leseni 233 za mfumo huo zilizolipiwa.

Pia ilionekana kuwa gharama za AMC kwa 'module' zote 12 za IFMS ni sawa na gharama ya leseni moja ya 'Active Planner' na pia ni sawa na gharama ya leseni moja ya mfumo wa huduma katika dawati la wateja. Kwa kawaida, utaratibu huu wa kutoza gharama za leseni kwa mfumo yote mitatu hauwezi kuwa sawa na hivyo unapaswa kuchunguzwa.

#### **8.3.4. Umiliki wa Mtandao, 'Data' na Mikataba**

Imeonekana kuwa baadhi ya maboresho yaliyofanyika katika mfumo wa IFMS hayakuhitaji uingiwaji mkataba. Hata hivyo kuna marekebisho yanayoendelea au yaliyokamilika katika maeneo mawili (EFT interface na GFS 2001) ambayo hayakuingiwa mkataba rasmi.

Bila kuwepo mkataba rasmi wa maboresho yanayofanyika katika mtandao, itakuwa vigumu kupima uwezo wa mtoa huduma katika kutekeleza jukumu hilo. Vilevile, upo uwezekano wa kuongezeka kwa mawanda ya kazi na gharama kusikotarajiwa.

Pia, kutokana na ukweli kuwa orodha kamili ya watumiaji wa toleo lolote la IFMS katika taasisi za Kiserikali haiwezi kupatikana, inaleta mkanganyiko na kuruhusu tofauti za kila wakati kati ya kilichopangwa kufanyika na hali halisi ya matumizi ya 'modules' na leseni za watumiaji mtandao. Vilevile, ni jambo lisilokubalika kuwa taarifa zote zihusuzo watumiaji wa IFMS inabidi zipatikane kutoka Soft-tech na kutumika kufanya maamuzi ya malipo.

#### **8.3.5. Mikataba ya leseni za Progamu za IFMS**

Imeonekana kuwa mazingira ya mfumo wa IFMS yamegubikwa na kutoingwa mikataba au kuwepo kwa mikataba dhaifu kati ya Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali (ACGEN) na muuzaji programu za mtandao huu.

Kwa mfano, haikuwezekana kupata mikataba ya ununuzi wa programu za IFMS. Kilichoweza kupatikana ni makubaliano ya mradi huu yaliyotolewa na Soft-tech kwa Serikali (toleo la 1.0 la tarehe 12/02/98) ambayo yalikuwa hayajaidhinishwa rasmi. Makubaliano hayo yanajumuisha bajeti ya leseni za programu za IFMS, huduma za ushauri na mafunzo lakini makubaliano hayo hayajawekwa kama mkataba rasmi wa leseni za programu za mtandao huu.

Mikataba isiyosimamiwa vyema inaweza kusabisha kuwepo kwa ongezeko la gharama za uendeshaji wa mtandao kwa Serikali. Aidha, Serikali haitakuwa na namna nzuri ya kupima ubora wa huduma wanayotoa wataalam wa mtandao huu jambo ambalo linaweza kusababisha hasara zaidi na mahusiano hafifu kati ya watumiaji wa mtandao na mtaalam mshauri.

#### **8.3.6. Mapungufu katika huduma zitolewazo na mtandao wa IFMS**

Mtandao wa IFMS haujafanyiwa marekebisho (Customization) ya kutosha kuufanya utumike kwa shughuli za kiuhasibu Serikalini. Marekebisho ambayo hayajafanyika ni kutoongeza eneo litakaloshughulika na udhibiti wa mihadi (commitment accounting) na utayarishwaji wa taarifa zinazozingatia matakwa ya viwango vya kimataifa vya kiuhasibu katika sekta ya Umma (IPSAS)

Tathmini iliyofanyika kuhusu matumizi ya IFMS imeonyesha kuwa Mtandao huu unatakiwa kufanyiwa maboresho kuufanya uwe wa kisasa zaidi ili uweze kukidhi mahitaji makubwa zaidi ya kiuhasibu ambayo ni pamoja na michakato muhimu katika utayarishaji wa bajeti ambapo kwa sasa Serikali hutumia mifumo mbalimbali isiyo jumuiifu katika kutayarisha bajeti ya Taifa kama vile SBAS, PlanRep na 'ActivePlanner',.

Mifumo hii ya bajeti isiyo jumuiifu hutumiwa zaidi kama nyenzo ya kuingiza 'data' za bajeti katika EPICOR kuliko

nyenzo ya kupanga na kutayarisha bajeti na hivyo kusababisha kulipwa kwa gharama kusikozingatia matumizi kamili ya huduma zote zinazopatikana katika mtandao wa IFMS. Bajeti ya matumizi ina changamoto zake ikiwa ni pamoja na mtandao kutakiwa kuwa na eneo la ukokotoaji wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na maombi ya manunuzi. Shughuli za kila siku kama usimamizi wa masurufu kunakohitaji marekebisho katika mfumo kufanyika ili kuweza kufanya usuluhisho wa taarifa za benki ambazo hazifanyiki kabisa.

#### **8.3.7. Usuluhisho wa Benki**

Kulikuwa na kadhia nyingi za benki zisizosuluhishwa za tangu mwaka wa 2000. Hii ilisababishwa na mtandao kutokuwa na uwezo wa kubeba kiasi kikubwa cha tarakimu rejea (reference number) katika fomu yake ya mapokezi ya fedha taslim itumikayo kusuluhisha kadhia hizo na zile za Benki Kuu. Pia kulikuwa na tarakimu rejea zilizoingizwa kimakosa na watumiaji wa mtandao na hivyo kuchangia kuwepo kwa kadhia zisizosuluhishwa.

Imeonekana kuwa, wakati wa kuhama kutoka 'Platinum SQL' kwenda EPICOR mwaka 2000, daftari la fedha lililopo katika toleo la Platinum SQL halikuhamishwa kwenda EPICOR. Matokeo yake, kumekuwepo malipo katika vitabu vya benki ambayo hayapo katika daftari la fedha kwa kipindi cha kuanzia Julai hadi Disemba, 2000. Malipo hayo hayajasuluhishwa hadi wakati wa kuandika taarifa hii. Mchakato wa usuluhisho wa benki umesisitizwa katika taarifa hii kwani ninaamini kuwa unaweza kuwa na athari kwa taarifa za fedha kwa Serikali na kwa hali hiyo, hatua za haraka zinapaswa kuchukuliwa.

#### **8.3.8. Mafunzo ya IFMS na huduma za kiufundi kwa watumiaji wa mtandao**

Kwa upande wa utoaji wa huduma za kiufundi kwa watumiaji mtandao wa IFMS, ukaguzi na ziara katika Mamlaka za Serikali za Mitaa vinaonyesha kuwa Soft-tech

hawana uwezo wa kutoa huduma ya ushauri na utaalam unaohitajika kwa nchi nzima. Kwa hali hiyo, mafunzo kwa watumiaji mtandao na ushauri kwa masuala ya kiufundi vinakosekana na kupunguza matumizi ya IFMS kama mfumo wa kuingiza na kuchakata 'data'. Hali hii ya kukatisha tamaa imesababisha Mamlaka za Serikali za Mitaa zirudi katika mfumo wa zamani (manual system). Eneo linalowasumbua watumiaji wa mtandao wa IFMS ni kukosekana kwa msaada wa kiufundi ambao unatolewa kutoka Dar es Salaam kwa ajili ya Wizara, Idara na Wakala wa Serikali na Hazina Ndogo zilizoko mbali.

Utaalam wa masuala ya EPICOR katika Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ni wa chini sana. Pamoja na kuwepo kwa kitengo cha uendelezaji ujuzi huu chenye watu 18, wakati mwingine huduma za kiufundi zitolewazo na Soft-tech zimeelekezwa zaidi katika maboresho madogo madogo ya IFMS ikiwa ni pamoja na vifaa na miundombinu ya mtandao.

## SURA YA 9

### MAJUMUISHO NA MAPENDEKEZO

#### 9.1 Majumuisho

Matokeo ya ukaguzi katika ripoti hii yaliwasilishwa kwa Maafisa Masuuli wote kwa ajili ya utekelezaji. Maafisa Masuuli wanatakiwa kuandaa taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo na kuyawasilisha kwa Mlipaji Mkuu-Wizara ya Fedha.

Katika ripoti hii nimebainisha dosari na mapungufu mengi katika mfumo wa udhibiti wa ndani yaliyosababishwa na kuwepo mianya ya usimamizi dhaifu wa mifumo ya ndani. Masuala haya yanatakiwa kushughulikiwa na Maafisa Masuuli kwa kuweka udhibiti wa ndani ulio imara na unaolenga kupunguza au kuzuia kabisa kutokea tena mapungufu haya.

Nimewajibika kutoa tena mapendekezo yangu kuhusu dosari nilizobaini katika ukaguzi, ambayo kama yatatekelezwa, yataweka usimamizi bora wa masuala ya fedha ndani ya Serikali.

#### 9.2 Mapendekezo

##### 9.2.1 Masuala ya miaka ya nyuma yasiyoshughulikiwa

Mapendekezo yangu kwa kaguzi za miaka ya nyuma yameonekana kutotekelezwa na baadhi ya maafisa Masuuli, hii inaashiria kuwa Serikali haitilii mkazo na haijali mapendekezo yangu. Katika hili, masuala yaleyale yamekuwa yakijirudia kila mwaka.

Katika ukaguzi wa mwaka huu, kulikuwa na Wizara/Idara/Wakala za Serikali 46 zilizokuwa na masuala ya miaka ya nyuma yasiyoshughulikiwa ya kiasi cha



sh.468,627,883,842, sehemu kubwa ikiwa ni Wizara ya Fedha ambayo ina kiasi cha sh.361,327,312,329.79 ikifuatiwa na Idara ya Huduma ya Magereza yenye sh. 19,261,840,595 na Sekretarieti ya Mkoa wa Lindi ikiwa ni ya tatu yenye kiasi cha Sh.10,146,855,167

Ninaikumbusha Serikali kutimiza wajibu wake katika kutekeleza mapendekezo ninayotoa kwa wakati ili kuzuia kutokea tena mapungufu au dosari za aina hii.

Hazina inatakiwa kutoa maelekezo/mwongozo kwa Maafisa Masuuli wote wachukue hatua muafaka katika kuboresha mifumo ya kutunza kumbukumbu na nyaraka, suala ambalo ndio chanzo cha hoja za ukaguzi. Ukosefu wa viambatanisho husababisha kushindwa kutekeleza mapendekezo yangu.

#### **9.2.2 Matokeo ya ukaguzi wa awali wa mafao ya wastaafu**

Kama nilivyotoa taarifa yangu mwaka uliopita, ukaguzi wa awali wa mafao ya wastaafu ni moja ya majukumu yangu ya uhibititi wa rasilimali za Umma. Kutokana na mambo yaliyojitokeza katika ripoti hii, inanifanya nijumuishe kwa kutoa taarifa kuwa, ulipaji wa mafao kwa wastaafu bado haufanywi kwa ufanisi. Kumekuwa na kutokufuata Sheria zinazosimamia stahili na ulipaji wa mafao ya wastaafu na utumiaji wa taarifa za wastaafu ambazo sio sahihi katika kutafuta stahili zao.

Ninapendekeza kwa Maafisa Masuuli wahakikishe kwamba kabla ya kuleta majalada ya mafao ya uzeeni kwangu kwa ajili ya ukaguzi lazima usahihi wa taarifa za watumishi na viambatanisho vya kumbukumbu vyote viwe vinawasilishwa pamoja kwa kuzingatia sheria na mashariti ya ajira, sheria za mafao ya uzeeni na kanuni zake

Serikali ihakikishe kwamba watumishi wa umma ikiwa ni pamoja na wanajeshi wanapoteuliwa kushika nyadhifa za kisiasa kwanza walipwe mafao yao katika utumishi wa awali kwa kipindi walichotumikia umma katika masharti ya utumishi huo. Hii itasaidi kulipwa mapema mafao ya uzeeni na pia

kuepuka kulipa mafao mara mbili. Vyeo vya kisiasa vinakuwa na masharti ya mkataba na hustahili mafao ya kiinua mgongo

**9.2.3 Manunuzi yaliyofanywa nje ya mpango wa mwaka manunuzi Sh. 50,685,371,565.58**

Mamlaka zinazofanya manunuzi zinatakiwa kuzingatia mpango ulioandaliwa wa manunuzi wa mwaka kuepuka gharama zisizo za lazima na manunuzi yasiyotakiwa au kufanya manunuzi holela kama inavyoelekezwa na kifungu namba 45 cha sheria ya manunuzi ya umma ya mwaka 2004

**9.2.4 Matengenezo ya magari ambayo hayakupitia EMESA Sh. 176,722,089**

Katika mwaka huu, tumegundua kwamba Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala wa Serikali tano zimelipa kiasi cha sh.176,722,089 ikiwa ni matengenezo ya magari katika karakana binafsi bila kupitia Karakana Kuu ya Serikali zilizo chini ya Wakala wa Ufundi Umeme na Mitambo(TEMESA).

Ninashauri taasisi za Serikali kuzingatia kanuni namba 59(1) na (2) ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2005 kwa kuhakikisha kuwa matengenezo ya magari lazima yaidhinishwe na Wakala wa Ufundi, Umeme na Mitambo (TEMESA) kabla na baada ya matengenezo.

**9.2.5 Malipo ya mishahara kwa watumishi waliostaafu, waliokufa, na watoro kazini Sh.1,842,607,565.29**

Jumla ya Sh. 1,842,607,565.29 zililipwa kama mishahara kwa wastaafu, watumishi walioacha kazi na watu wengine wasiostahili kulipwa mishahara.

Ili kuepuka hasara katika siku zijazo, nina washauri Maafisa Masuuli wa Wizara wote kuangalia na kupitia mara kwa mara kumbukumbu za watumishi walio bado kwenye ajira ili kuthibitisha uhakika wa uwepo wao katika ajira.

Pia, kuwepo mawasiliano kati ya Wizara, Hazina na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili kuhakikisha kwamba majina ya wastaafu, watoro au watumishi ambao

ajira zao zimekoma wawe wamefutwa mara moja kusitisha ajira.

Hili litawezekana endapo kasoro za kimfumo, utendaji na usimamizi wa mishahara ya watumishi litaondolewa kwa kuwa na mfumo na programu ya kompyuta wa kisasa unaoruhusu kutoa na kuingiza kumbukumbu za watumishi.

**9.2.6 Malipo ya posho ya samani kwa maafisa wasiostahili Sh. 650,714,800.34**

Maafisa Masuuli wanatakiwa kuzingatia mwongozo wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma (UTUMISHI) No.C/CA/134/213/01/G/69 ya Januari 30, 2006 juu ya malipo ya posho ya samani kwa maafisa wa serikali.

Katika suala hili, Wizara na Idara kumi(10) zilifanya malipo ya jumla ya shilingi 650,714,800.34 kwa kuwalipa posho za samani watumishi wanaoishi katika nyumba zao binafsi bila kuzingatia mwongozo wa Utumishi uliotajwa hapo juu.

Ninashauri fedha hizi zirejeshwe Serikalini. Kwani zimetumika kimakosa kulipia posho ya samani

**9.2.7 Malipo yenye nyaraka pungufu Sh 4,303,339,515**

Ukaguzi umebaini malipo yenye nyaraka pungufu ya kiasi cha Sh. 4,303,339,515.

Ninaishauri Serikali kwamba hati za malipo yanayofanywa na Maafisa Masuuli yawe yameambatanishwa na nyaraka sahihi kulingana na Kanuni 95(4) ya Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004)

**9.2.8 Vifaa vilivyolipiwa bado havijapokelewa Sh 13,865,874,762**

Ukaguzi ulibaini malipo ya kiasi cha sh. 13,865,874,762 kwa wazabuni mbalimbali kabla ya vifaa hivyo kupokelewa.

Ninawashauri Maafisa Masuuli wanaohusika kufuatilia kwa karibu vifaa hivyo na kuhakikisha kwamba vinapokelewa na kuandikwa kwenye vitabu vya Serikali

#### 9.2.9 Malipo yaliyofanyika katika kasma isiyosahihi Sh. 4,953,226,683

Malipo ya kiasi cha sh. 4,953,226,683 yalilipwa na Maafisa Masuuli bila kuzingatia makisio katika kasma husika.

Ninawashauri Maafisa Masuuli kutumia fedha za umma kama ilivyoainishwa kwenye kasma na inapotokea kwamba kasma imekwisha utaratibu ufuatwe wa kuomba kibali toka Wizara ya Fedha kama ilivyo elekezwa kwenye kanuni 51(1-8) ya Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebisha 2004)

Kutumia zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge ni kukiuka Sheria ya Fedha za umma ya mwaka 2001 na hivyo hatua za kinidhamu zinapaswa kuchukuliwa dhidi ya Maafisa Masuuli wanaoshindwa kuzingatia Mfumo wa bajeti ya Serikali unaosisitiza dhana ya fedha taslimu.

#### 9.2.10 Malipo yenye shaka Sh 15,595,054,755

Wizara mbili, yaani Wizara ya Fedha -fungu 50 na Wizara ya Sheria fungu 40 zilifanya malipo ya kiasi cha sh 15,595,054,755 ambayo kwa mtizamo wa ukaguzi hayakuwa na maelezo na viambatanisho halisi na vya kutosha kuhalalisha matumizi hayo ya fedha za umma.

Serikali inashauriwa kuchunguza sababu zilizofanya malipo haya yenye utata na kuwasilisha maelezo ya kina ili kuondoa utata.

### 9.2.11 Usimamizi wa manunuzi ya umma

Katika taarifa zangu zilizowasilishwa kwa Maafisa Masuuli nilieleza bayana kuwa Wizara/Idara/Wakala na Sekretarieti za Mikoa hazikuzingatia kikamilifu Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.21 ya mwaka 2004 na kanuni zake za mwaka 2005.

Mapitio ya taratibu za manunuzi yalibaini kwamba kuna kazi kubwa ya kufanya ili kuhakikisha kwamba sheria ya manunuzi inafuatwa. Nilitoa taarifa kwamba karibu Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa yote hazikufuata kikamilifu Sheria ya manunuzi. Ingawa matumizi katika manunuzi mwaka huu yamepungua kutoka asilimia 70 miaka ya nyuma hadi asilimia 52, bado Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.21 ya mwaka 2004 na kanuni zake za mwaka 2005 haizingatiwi kikamilifu.

Hivyo, ninapendekeza mamlaka zinazofanya manunuzi ziwezeshe kwa kuwa na wataalamu katika fani ya manunuzi, kuimarisha vitengo vya manunuzi, kujengea uwezo bodi za manunuzi na kitengo cha ukaguzi wa ndani za Wizara/Idara/Wakala na Sekretarieti za Mikoa

### 9.2.12 Madeni na Mihadi ya Serikali Sh. 254,616,874,180

Serikali ilikuwa na madeni na mihadi inayofikia Sh. 254,616,874,180 ikijumuisha deni la Taifa kiasi cha Sh.93,860,806,990 na madeni mengine na mihadi ambayo kwa pamoja yalikuwa na thamani ya Sh. 39,916,624,968 yahusuyo vifaa na huduma pamoja na madai ya watumishi.

Kutokana na ukweli kuwa madeni haya pamoja na mihadi yalikuwepo katika mwaka wa fedha ninaoutolea taarifa, hali hii inakinzana na Mfumo wa Uhasibu wa Kimataifa katika Sekta ya Umma unaotambua mapato yapokelewapo na matumizi kufanyika kwa fedha taslimu.

Kutumia zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa ni kukiuka Sheria ya Matumizi ya Umma na hivyo hatua za kinidhamu zinapaswa kuchukuliwa dhidi ya Maafisa Masuuli wanaoshindwa kuzingatia Mfumo wa bajeti ya Serikali unaosisitiza dhana ya fedha taslimu.

Serikali ijiepushe kuingia katika mihadi huku ikijua hakuna fedha zilizotengwa kwa ajili matumizi hayo. Aidha, ni muda muafaka sasa kwa Serikali kufikiria kuchukua hatua kali kwa Maafisa Masuuli watakaoshindwa kuzingatia mfumo wa bajeti unaosisitiza dhana ya fedha taslimu

Madeni yasiyolipwa ya Sh. 254,616,874,180 yajumuishwe katika Hesabu za Taifa.

#### 9.2.13 Misamaha ya kodi

Kwa mwaka wa fedha 2009/2010, ukaguzi ulibaini kupungua kwa misamaha ya kodi kutoka sh. 752,398,800,000 mwaka 2008/09 na kufikia sh 680,667,900,000 katika mwaka 2009/10. Katika utoaji wa misamaha ya kodi, yafuatayo yanafaa kuzingatiwa na Serikali:

- Serikali inashauriwa kupitia upya sera yake ya misamaha ya kodi kwa lengo la kupunguza misamaha hiyo kwa kiwango cha chini kadri itakavyowezekana.
- Vile vile, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) wafanye mapitio yenye umakini katika bajeti zake za makusanyo ya mapato kwa lengo la kuzifanya ziwe na uhalisi zaidi.
- Mfumo wa uangalizi na udhibiti wa ndani katika Mamlaka ya Mapato unapaswa kuimarishwa ili kuhakikisha kuwa marejesho ya mapato na malipo ya kodi vinapitiwa kwa makini ili kubaini udanganyifu na mianya ya ukwepaji kodi kwa lengo la kuongeza mapato yatokanayo na kodi na kuzuia matumizi mabaya ya fedha za Serikali.

- Serikali ifikirie kuongeza wigo wa kodi kwa kuhusisha sekta isiyo rasimi.

#### **9.2.14 Misaada kutoka nje ya nchi Sh. 393,256,357,651**

Taarifa ya misaada kutoka nje ya nchi inaonyesha kiasi cha Sh.3,932,474,455,117 kikiwa ni makadirio ya misaada iliyotarajiwa kupokelewa kutoka vyanzo mambalimbali nje ya nchi kwa mwaka wa fedha 2009/10. Hata hivyo, kiasi halisi kilichopokelewa ni Sh.2,393,256,357,651 ikiwa ni sawa na asilimia 61 ya makisio yote. Hii inaonyesha kwamba masharti ya misaada hayakuzingatiwa au misaada hiyo haikuletwa na wahisani.

Ninaishauri Serikali kuandaa makisio ya matumizi yanayoendana na hali ya uhakika ya kupokea misaada kutoka nje ya nchi. Aidha, kuwe na uhakika wa kupokea fedha za misaada kutoka nje ya nchi ili kusiwe na matatizo au usumbufu katika kutekeleza bajeti ya Taifa. Misaada ya nje inatakiwa kuoneshwa kwenye taarifa jumuiifu endapo kuna uhakika wa kuzipokea kulingana na Mwongozo wa Kimataifa Kihisibu wa kuandaa taarifa za fedha, IAS 20.

#### **9.2.15 Maduhuli yasiyokusanywa kwa wakati**

Hesabu Jumuiifu za Taifa zimeonyesha maduhuli yasiyokusanywa yameongezeka kutoka Sh. 10,020,246,900 kwa mwaka 2008/2009 hadi kufikia Sh. 116,320,437,345 kwa mwaka 2009/10 ikiwa ni ongezeko la asilimia 16.30. Hii inaonyesha kuwa kulikuwa na udhaifu katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali katika mwaka wa fedha 2009/2010.

Katika eneo hili, Serikali inashauriwa kuongeza juhudi kubwa katika kukusanya maduhuli kwa kutumia sheria za nchi na kuhakikisha kuwa kiasi chote kilichotakiwa kukusanywa kinakusanywa. Wale wote walio husika na kutokusanywa kwa maduhuli wachukuliwe hatua za kisheria

#### **9.2.16 Taarifa ya madeni ya taifa Shs.0,613,868,673,604**

Taarifa jumuiifu za fedha za Taifa zinaonyesha kwamba deni la taifa limeongezeka kwa asilimia 38 kutoka

sh7,621,286,730,033.80 mwaka 2008-09 hadi kufikia sh. 10,503,806,011,884.90 mwishoni mwa mwaka 2009-10. Kulingana na taarifa za fedha,deni landani limeongezeka kutoka sh 43,373,690,323 na sh.358,846,010,303 kwa mwaka 2007-08 na 2008-09 ikiwa ni ongezeko la silimia 2 na asilimia 19 na baadaye ongezeko likawa sh 521,261,841,212 sawa na asilimia 23 kwa mwaka 2009-10.

Deni la ndani limeongezeka kidogo ukilinganisha na deni la nje, lakini kwa ujumla wake utaona kuwa Serikali ilikopa kiasi kikubwa cha fedha kutoka katika taasisi mbalimbali za nje kuliko kiasi kilichokopwa katika taasisi za ndani ya nchi. Hii inamaanisha kuwa Serikali ina dhima kubwa katika kuwalipa wadai wa nje kuliko wadai wa ndani, na hii kiuchumi ina maana kuwa kiasi kikubwa cha mtaji katika fedha za kigeni kitalipwa nje ya nchi.

Katika mwelekeo huu wa deni la Taifa, Serikali inakumbushwa kuwa makini katika shughuli zake za kiuchumi kwa kuweka uwiano wa kukuza uchumi ambao utaweza kuleta tija kwa taifa na kulipa madeni yote kwa wakati yanapofikia muda wa kulipwa.

Pia kuna haja ya kuongeza mbinu nyingine za vyanzo vya kodi na kuwa makini katika kutumia fedha za umma kwa kukwepa matumizi ambayo siyo ya lazima.

#### **9.2.17 Taarifa ya mihadi Sh. 93,860,806,990**

Taarifa jumuiifu ya mihadi isiyoshuhulikiwa inaonyesha kufikia Sh. 93,860,806,990 kama ilivyokuwa tarehe 30 Juni, 2010 ikiwa ni pungufu ya Sh. 275,883,320,206 au asilimia 75 ikilinganishwa na ile ya mwaka 2008/09 ya kiasi cha Sh. 369,744,135,196.

Ninarudia kusesitiza ushauri wangu niliotoa mwaka uliopita, Serikali inabidi iwe na tahadhari kubwa katika kujiingiza katika mihadi ambapo hakuna fedha ya kugharamia matumizi hayo. Hali kadhalika pale Serikali inapokuwa na



bakaa ya fedha ambazo hazina mihadi ni vyema zikarudishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

#### **9.2.18 Taarifa ya mikopo inayotolewa na Serikali Sh.424,087,766,124**

Kuna haja ya kudhibiti na kusimamia kwa karibu zaidi fedha za Serikali zinazotolewa kama mikopo kwa umma kwa kuhakikisha kuwa ukiukwaji wa Kanuni za Fedha unaosababisha matumizi mabaya ya fedha zilizokusudiwa kuimarisha hali ya ulipaji mikopo unadhibitiwa.

Taratibu za sheria zitazamwe kuhusu Sh.416,463,228,145 ambazo makampuni hayapo tena na uwezekano wa kulipwa ni mdogo au hakuna.

#### **9.2.19 Taarifa ya madeni yasiyotarajiwa Shs.26,276,785,317**

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2010, Serikali ilikuwa na madeni yasiyotarajiwa yaliyofikia kiasi Sh.26,276,785,317 yaliyohusisha mafungu kumi na mawili ambayo asili yake haikuonyeshwa kwenye vitabu.

Madeni yasiyotarajiwa kama haya ni mzigo mkubwa kwa Serikali hasa pale yanapoiva na kuhitajika kulipwa, hivyo ningependa kuishauri Serikali kujiepusha katika kufanya maamuzi ambayo yatasababisha kushamiri kwa madeni yasiyotarajiwa. Na endapo kuna kesi zinazoendelea mahakamani jitihada zifanyike za kukamilisha hukumu za kesi hizo.

#### **9.2.20 Taarifa ya Udhadini wa Serikali Sh 711,804,989,096**

**(i) Kutoa udhamini zaidi ya kiwango kilichowekwa na sheria**

Serikali ilidhamini kampuni tatu zaidi ya kiwango cha mkopo kwa sh 60,864,285,978 kinyume na Kifungu Na. 13 (1)(b) cha Sheria ya Mikopo ya Serikali, Misaada na

Udhamini ya Mwaka 1974 kama ilivyorekebisha mwaka 2004 kinasema hivi:

“.....Kiwango cha juu kabisa ambacho Serikali inaweza kudhamini deni hakitazidi asilimia 70 ya fedha zilizokopwa.....”

Pia Serikali ilitoa udhamini katika mashirika ya umma manne. Vile vile, taarifa ya udhamini wa Serikali inatofautiana katika Hesabu Jumuifu za Taifa na ile ya Msajili wa Hazina kwa tofauti ya Sh. 3,940,266,366

Katika hali hii, Serikali inajikuta ikidhamini madeni makubwa zaidi ya kiwango kilichowekwa kisheria, hali ambayo inaiweka Serikali katika mazingira hatarishi ambapo mwisho wake Serikali itahitajika kutumia kiasi kikubwa cha fedha kugharamia madeni ambayo yameshindikana kulipwa na taasisi zilizodhaminiwa kulipa madeni hayo na gharama nyinginezo.

Tofauti kati ya taarifa hizi mbili zinahitaji kufanyiwa ulinganisho ili kupata usahihi wake.

Vilevile, Kifungu Na.13 (b) cha Sheria ya Mikopo ya Serikali, Msaada na Udhamini ya Mwaka 1974 kimeonyesha kuwa ili taasisi yoyote au kampuni inufaike na udhamini wa Serikali kwa deni lake, taasisi au kampuni hiyo italazimika kutoa dhamana au rehani itakayolingana na kiasi kile ambacho Serikali imedhamini ili pale taasisi au kampuni hiyo itakaposhindwa kulipa, Serikali iweze kurudisha fedha zake kwa kutumia dhamana iliyowekwa kama kinga kuepuka hasara. Hata hivyo, hapakuwepo na ushahidi wowote kama taasisi au makampuni yalidhaminiwa na Serikali yaliweka dhamana au hati za rehani kwa Serikali.

Katika maswala yote mawili hapo juu, naishauri Serikali yafuatayo:

- Kuwepo aina za rehani zinazoeleweka kwa kila anayechukua mkopo
- Wale wote wanaoidhinisha dhamana zaidi ya kiwango kinachotakiwa wawajibishwe

- Serikali izingatie sheria za utoaji dhamana na ziwe ndani ya kiwango kilichoidhinishwa cha asilimia 70 ya mkopo
- Tofauti zinazojitokeza kati ya taarifa za Msajili wa Hazina na hesabu jumuiifu za fedha za Taifa isuluhishwe.
- Kuna haja ya Waziri wa Fedha kutoa mwongozo unaodhibiti kikomo cha utoaji wa dhamana katika kiwango cha asilimia 70

#### 9.2.21 Salio katika mpango wa mfuko wa kubadilisha madeni Shs. 2.099 billion

Katika ukaguzi wa Benki Kuu ya Tanzania ilibainika kwamba mpango wa mfuko ya Serikali ya kubadilisha madeni ulikuwa na salio la kiasi cha Sh2.099 bilioni. Hata hivyo, haikudhihirika wazi kama bado kuna madai halali katika mfuko huo.

Ipo haja ya kurejesha fedha kutoka mfuko wa mpango wa kubadilisha madeni kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali pale lengo lake linapokuwa limekwisha.

#### 9.2.22 Kutoonyesha madai na amana za Serikali kwenye taarifa za fedha

Taarifa ya fedha iliyochapishwa ya Benki Kuu ya Tanzania kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2010 imeonyesha kwa ujumla kiasi cha sh 134.46 bilioni kama fedha zilizotazamiwa kupokelewa na benki kuu kutoka Serikalini. Hata hivyo, kiasi hiki hakikuonyeshwa kwenye hesabu jumuiifu za Taifa kama madai ya benki kuu Serikalini.

Ninaishauri Serikali kutambua na kuonyesha kwa uwazi amana na madeni/madai yote kwenye taarifa jumuiifu za Taifa.

Vile vile, madai yaliyolipwa baada ya kufunga hesabu za mwaka yaonyeshwe katika kidokezo cha taarifa za fedha.

**9.2.23 Madeni ya vifaa na huduma ambayo hayakulipwa Shs. 160,756,067,190**

Serikali inafuata mwongozo wa kimataifa wa sekta ya umma katika kuandaa taarifa za fedha za mwaka unaozingatia malipo na mapokezi fedha taslimu katika kulipa na kupokea fedha.

Hata hivyo, imeonekana kwamba mwongozo huo haufuatwi na watendaji Serikalini kwani mwisho wa mwaka kuna madeni yahasuyo vifaa na huduma mbalimbali ambayo hayakulipwa kinyume na makisio yanayofuata mfumo wa fedha taslimu.

Ninasisitiza ushauri wangu nilioutoa mwaka ulipita kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali kuonyesha madeni na amana zote katika taarifa za fedha jumuiifu za taifa. Pia, manunuzi ya vifaa na huduma yafanyike kwa kufuata makisio yaliyoidhinishwa na Bunge

**9.2.24 Vitega uchumi vya Serikali Sh. 8,718,182,145,310**

Serikali inashauriwa kuwa na kumbukumbu kamili kuhusu vitega uchumi vyake ili kurahisisha uandaaji wa taarifa jumuiifu za fedha za Taifa

Serikali ifanye mapitio ya sera ya uwekezaji wa nje na ikibidi kuuza vitega uchumi ambavyo havina manufaa kwa Taifa

**9.2.25 Taarifa ya mali za Serikali Sh.7,981,954,338,324**

